Hii ni nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA TATU

**Kikao cha Tano - Tarehe 10 Novemba, 2003**

*(Kikao Kilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Eliachim J. Simpasa) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):** Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Benki ya Raslimali Tanzania *(TIB)* kwa Mwaka Ulioishia tarehe 31 Desemba, 2002 *(The Annual Report and Accounts of the Tanzania Investment Bank for the Year Ended 31st Desember, 2002).*

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma *(PPF)* kwa Mwaka 2002 *(The Annual Report and Accounts of the Parastatal Pensions Fund for the Year 2002).*

## MASWALI NA MAJIBU

Na.60

### Vituo Maalum kwa Shughuli za Uwekezaji Nchini

**MHE. NAZIR M. KARAMAGI (k.n.y. MHE. STEPHEN M. KAZI)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imetangaza kuanzisha Vituo *One Stop Centre* ambavyo vitavutia na kuwawezesha wawekezaji na wafanyabiashara kukamilisha shughuli zao hapa nchini kama vile upatikanaji wa leseni, vibali, maeneo na viwanja bila usumbufu wowote:-

(a) Je, ni Vituo vingapi vya aina hiyo vimeshaanzishwa na viko wapi?

(b) Je, Serikali inatoa taarifa gani ya mafanikio na matatizo ili kuisaidia Serikali kutoa maamuzi ya kuendelea au kutoendelea na uanzishwaji wa Vituo hivyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Stephen Kazi, Mbunge wa Mwanza Mjini, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Serikali ilianzisha utaratibu wa *One Stop Centre* kwa lengo la kuongeza ufanisi katika kuwahudumia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Kuanzishwa kwa utaratibu huu kulitokana na kuchukua muda mrefu kwa wawekezaji kupata leseni, vibali maeneo na viwanja kutoka katika Wizara, Idara na Taasisi mbalimbali za Serikali. Ili kurekebisha mfumo wa uwekezaji nchini, Serikali ilifanya utafiti unaojulikana kama *Investors Road Map Study* kwa lengo la kubaini matatizo yanayowakabili wawekezaji na kuweka utaratibu utakaosaidia wawekezaji kupata leseni, vibali, maeneo na viwanja bila usumbufu wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya utafiti huu yaliwezesha kurekebishwa kwa Sheria ya Uwekezaji ya Mwaka 1990 na kuundwa kwa Sheria Mpya ya Uwekezaji Mwaka 1997. Sheria hii iliwezesha kuanzishwa kwa Kituo cha Uwekezaji Raslimali Tanzania yaani *Tanzania Investment Centre (TIC)* kwa utaratibu wa *One Stop Centre* ili kuwahudumia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi mahali pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Kazi, Mbunge wa Mwanza Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mpaka hivi sasa Serikali imeanzisha Kituo kimoja cha Uwekezaji kilichopo Dar es Salaam ambacho kina maafisa kutoka katika Wizara na Taasisi mbalimbali hususan Viwanda, Ardhi, Uhamiaji, *TRA,* Idara ya Kazi na Wakala wa Kusajili Leseni za biashara kwa lengo la kutoa huduma kwa wawekezaji mahali pamoja na kwa ufanisi. Kwa kuzingatia gharama kubwa za kuanzisha na kuendesha *One Stop Centre,* Vituo vingine vya Mikoa bado havijaanzishwa.

Hata hivyo katika jitihada za kuongeza kasi ya uwekezaji nchini, Serikali ina mpango wa kuanzisha Vituo vya Kanda (hususan katika Mikoa ya Arusha na Mwanza na kadhalika), hatua kwa hatua kulingana na uwezo wa Serikali kifedha.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa zilizopo zinaonesha mafanikio makubwa tangu utaratibu huu uanzishwe. Mafanikio hayo ni pamoja na kupunguzwa kwa muda wa kupata vibali na leseni za uwekezaji hapa nchini kutoka siku 100 hadi kufikia siku 14, kuongezeka kwa miradi inayosajiliwa na Kituo kutoka miradi 82 mwaka 1995 hadi kufikia miradi 311 mwaka 2002 na kuongezeka kwa huduma zinazotolewa kwa wawekezaji katika masuala ya kodi, uanzishwaji wa makampuni na leseni za biashara pamoja na kuongezeka kwa vibali vya kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea na utaratibu huu wa *One Stop Centre* kwa lengo la kuongeza kasi ya uwekezaji nchini na hatimaye kuinua uchumi wa Taifa. Aidha, Serikali itaweka mkazo katika kuanzisha Vituo vya uwekezaji katika Mikoa mbalimbali nchini ili kuwasaidia wawekezaji kupata huduma kwa urahisi.

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu yaliyotolewa na Waziri ambayo yanatosheleza ningeomba tu nifahamu kwamba katika mpangilio huu, pamoja na kwamba pia hata wananchi wangeweza kufaidika kutokana na hivi Vituo kama vingeweza vikaanzishwa vingi na vya kutosha katika maeneo yote; Serikali sasa ina mkakati gani hasa wa kuridhisha ambao ungeweza ukawashawishi wananchi na kuwaridhisha kwamba inashiriki na Vituo hivi vinaweza vikawa vinashirikiana na Halmashauri na vikaanzishwa kwa wingi na kwa urahisi katika maeneo mengi nchini hapa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi ni kwamba uanzishwaji wa Vituo hivi vya *One Stop Centre,* unahitaji fedha nyingi sana. Kwa hiyo, jinsi fedha zitakavyopatikana, ndivyo tutakavyoweza kuanzisha Vituo hivi katika maeneo husika. Lakini vile vile niseme kwamba kwa sababu nia ya *One Stop Centre* ni kupunguza urasimu, kupunguza gharama za kiutawala na gharama za kufanyia kazi hasa kwa wawekezaji, tuna hakika kabisa Maafisa wa Halmashauri za Wilaya wanahusika aidha na vibali au na Uhamiaji watahusishwa katika Vituo hivi ili kuwarahisishia wawekezaji kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi.

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa vile kinachoitwa *One Stop Centre* katika nchi yetu siyo chochote wala sio lolote kwa maoni ya wawekezaji na *TCIA* kwa vile kuna urasimu na dalili ile ya rushwa; je, Waziri haoni kwamba wakati umefika wa kuiga nchi ya Botswana ambapo Rais wake ameagiza kwamba kama mwekezaji anazungushwa kwa muda wa wiki moja ampigie Rais moja kwa moja.? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa, wakati ambapo Serikali ilikuwa haijaanzisha utaratibu wa *One Stop Centre,* yalitokea malalamiko mbalimbali baina ya wawekezaji, kwanza kutokana na urasimu mrefu, halafu pili, kudaiwa rushwa, lakini tatu kuchelewa kwa mipango ya uwekezaji ya wawekezaji hawa.

Kama nilivyojibu swali langu la msingi, zamani ilikuwa mwekezaji anapata kibali katika muda wa siku 100. Sasa siku hizo zimeteremshwa mpaka kufikia siku 14. Kwa vyovyote, hiyo ni dalili ya tija na ufanisi. *(Makofi)*

Lakini vile vile kutokana na utaratibu huo, Mheshimiwa Philip Marmo atakumbuka zamani kwamba hata wawekezaji wanapofika *Airport* kabla hawajaingia nchini, wengine walikuwa wanadaiwa rushwa hata za kalamu. Lakini hilo sasa limekwisha na taarifa tulizonazo, wawekezaji wengi sasa wanavutiwa kuwekeza

Tanzania kwa sababu ya kupunguza gharama za utawala, gharama za kazi na kupungua kwa rushwa ambayo inapigiwa kelele si na Mheshimiwa Rais peke yake, bali Watanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI:** Swali la mwisho la nyongeza Mheshimiwa Thomas Ngawaiya.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nia ya Serikali katika uwekezaji wa namna yoyote ni kuongeza ufanisi wa shughuli yenyewe na kuleta kipato katika Taifa hili na ajira vile vile kwa wananchi wetu, Serikali ina mpango gani sasa kwa hao wanaonunua viwanda kama Kiwanda cha Magunia Moshi, Kiwanda cha Bia Moshi halafu wanafunga bila kufanya chochote na ajira hakuna? Serikali ina mpango gani na jambo kama hilo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba Kiwanda cha Magunia Moshi na viwanda vinginevyo vilivyopo Moshi, havifanyi kazi kutokana na matatizo mbalimbali na hii imetokana na uthibitisho wa mimi mwenyewe kutembelea sehemu hizo na kuona viwanda hivyo.

Baadhi ya viwanda hivyo, vimekuwa vikisumbuliwa na utaratibu wa kisera, kwa mfano Kiwanda cha Magunia kinapata matatizo ya kuzalisha kwa sababu tunaagiza kwa wingi magunia aina ya *jute* badala ya kununua magunia yanayotengenezwa na mkonge. Lakini hilo sasa hivi Serikali inalifanyia kazi kuona ni jinsi gani tutaweka mikakati ambayo itawafanya waagizaji kutoka nje kupunguza kasi na ari ya kununua magunia ya jute na badala yake kutumia magunia yanayotengenezwa na katani.

Vile vile lazima tukubaliane kwamba uwekezaji wa viwanda katika maeneo kadhaa hapa nchini wakati mwingine ulikuwa haufuatilii uwezo wa maeneo husika, viwanda vilikuwa vinawekwa tu kwa sababu viende mahali fulani. Hilo linaweza likawa ni tatizo baadaye viwanda hivyo vikafanya kazi bila ya ufanisi. *(Makofi)*

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI:** Maswali kwa Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Issa Mohamed Suleiman.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI:** Tunaendelea na kujibu maswali.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mwongozo, Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI:** Kaa kwanza. Haya, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hakuna Mamlaka ijulikanayo kama Serikali ya Tanzania Bara na kwa kuwa Mamlaka hiyo ambayo haipo inaonekana kama inaambiwa imevaa joho la Serikali ya Muungano, isingekuwa vyema swali hili ambalo linabeza Serikali ya Muungano likasahihishwa kabla halijajibiwa? *(Makofi)*

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI:** Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, jibu hii. *(Kicheko)*

Na. 61

**Tume ya Pamoja ya Fedha**

**MHE. ISSA MOHAMED SULEIMAN** aliuliza:-

Kwa kuwa kwa karibu miaka 39 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikipokea misaada mbalimbali kama vile fedha, vyakula dawa, magari, pembejeo na kadhalika na kwa kuwa kwa kipindi chote hicho Serikali ya Tanzania Bara imekuwa ikivaa Joho la Mamlaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Taasisi zake kupata misaada hiyo kwa sababu hakuna njia nyingine ya kukwepa hali hiyo kwa mujibu wa Katiba ya Nchi:-

(a) Je, Tume ya Pamoja ya Fedha chini ya Mwenyekiti wake wa sasa, Mheshimiwa William Shellukindo, itafanya kazi kwa kulijua hilo?

(b) Je, utekelezaji wa shughuli za Tume hiyo unaanzia wapi?

(c) Ili kulifanya jambo hilo liwe wazi; je, Serikali iko tayari kutuletea taarifa za aina ya misaada iliyotolewa kila mwaka na kuigawa kwa Wabunge kama zinavyotolewa taarifa nyingine Bungeni kwa kuzingatia maelezo ya sehemu ya (a) ya swali hili?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Issa Mohamed Suleiman, Mbunge wa Magomeni, lenye sehemu (a), (b) na (c) naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ambayo kila Mheshimiwa Mbunge ameapa kuilinda, kuihifadhi na kuitetea, mfumo wa Muungano ni Serikali mbili yaani Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa mwuliza swali atapenda kurejea Ibara ya 4(2) ya Katiba ya Nchi. Serikali ya Tanzania Bara anaiyoitamka Mheshimiwa Mbunge wa Magomeni katika

swali lake haimo katika vyombo, asasi au Mamlaka zilizopo kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mambo yote yanayohusiana na mchango wa mgawanyo wa mapato ya Jamhuri ya Muungano, yamefafanuliwa katika ibara 133 na 134 za Katiba ya Nchi zikisomwa pamoja na sheria Na.14 ya mwaka 1996.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kunukuu ibara ya 133 ya Katiba. Ninanukuu. "Serikali ya Jamhuri ya Muungano itatunza akaunti maalum itakayoitwa Akaunti ya Fedha ya Pamoja na ambayo itakuwa ni sehemu ya Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano ambamo kutawekwa fedha yote itakayochangwa na Serikali mbili kwa kiasi kitakachoamuliwa na Tume ya pamoja ya Fedha kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge kwa madhumuni ya shughuli za Jamhuri ya Muungano kwa mambo ya Muungano."

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Issa Mohamed Suleiman, Mbunge wa Magomeni kama ifuatavyo:-

(a) Tume ya Pamoja ya Fedha chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa William Shellukindo, itafanya kazi zake kwa kuzingatia Katiba na Sheria ya Tume ya Pamoja na Fedha Na.14 ya mwaka 1996.

(b) Tume ya Pamoja ya Fedha itafanya kazi kwa kuzingatia misingi ya ibara 134 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Sheria Na.14 ya 1996.

Aidha, katika kutekeleza kazi zake, Serikali inatarajia Tume itafaidika na uzoefu uliotokana na utekelezaji wa makubaliano ya Serikali zetu mbili kabla ya Tume kuundwa rasmi.

(c) Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali ikishirikiana na Tume ya Pamoja ya Fedha baada ya Tume hiyo kujizatiti ipasavyo, Serikali hatakuwa na sababu ya kutotoa taarifa Bungeni si tu kuhusu misaada mbalimbali itakayotolewa na jinsi itakavyogawanywa kila itakapotakiwa kufanya hivyo, bali pia mchango wa kila Serikali katika kugharamia shughuli za Muungano.

**MHE. ISSA MOHAMED SULEIMAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Pamoja na nia nzuri ya Mbunge aliyetaka mwongozo, naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa katika Ibara hiyo hiyo aliyoieleza Mheshimiwa Waziri ya 134 inajitokeza kwamba suala hili limeanza kujulikana mwaka 1984 kwa sheria inayoelezwa ndani ya Katiba, je, Mheshimiwa Waziri atanijulisha kwamba ni lini fedha za mgao asilimia 4.5 zitaanza kutolewa? Pia kwa mujibu wa suala hilo hilo, atakubaliana nami kwamba ni busara mgao huo uanze kama Katiba ilivyoonesha mnamo mwaka 1984?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza kuhusu ni lini asilimia 4.5 ya

mgao kwa upande wa mapato yanayohusika katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano, yameanza kutolewa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, nina hakika Mheshimiwa Mbunge, kama hakuwa Mbunge, alikuwa hapa mezani wakati tulipojadili taarifa ya Mheshimiwa William Shellukindo na uamuzi ule ulitokana na uamuzi wa Bunge hili baada ya kujadili taarifa hiyo. Kwa hiyo, utekelezaji nina hakika, ninakumbuka ulianza lini. *(Makofi)*

Pili, anapozungumzia juu ya suala la kwamba, kwa sababu Katiba ni ya mwaka 1977 na kwa maana hiyo mgao huu angependa urudi kwenye tarehe ya Katiba, ningependa niseme kwamba tusitazame mgao tu, ni vizuri tukazingatia ni mchango kwa sababu hapa tunazungumzia Serikali mbili kuchangia gharama za kuendesha Muungano. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa katika majibu ya msingi ya Mheshimiwa Waziri amesema kuna Mfuko wa Pamoja wa Fedha kwa mambo ya Muungano na kwa kuwa Wafadhili huwa wanatoa pesa kwa Tanzania lakini hawatambui kwamba kuna mfuko wa Muungano, je, ni lini itajulikana kwamba hela hizo zilizotolewa na Wafadhili ni kwa ajili ya mambo ya Muungano na Mfadhili akajua hivyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, wahisani walio na nia njema ya kusaidia juhudi za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kujiletea maendeleo, wanafanya hivyo katika misingi ya ushirikiano wa Kimataifa kwa maana ya kuitambua Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini vile vile na sisi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunatambua kwamba kuna nchi mbili zilizoungana na tuna dola moja yenye mfumo wa Serikali mbili na ndiyo maana katika lile swali la nyongeza lililopita, tumezungumzia suala la mgao tulipokubaliana asilimia 4.5 iende kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hii ni uamuzi wetu sisi tunapokuwa tumepata misaada na michango ya kusaidia juhudi zetu za kujiletea maendeleo tukizingatia na upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, maelezo ya ziada.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri sana kuhusu suala hili. *(Makofi)*

Lakini napenda niongezee tu kwamba katika fedha ambazo tunapewa na Wahisani, kuna fedha za aina mbili. Kuna fedha ambazo tunapewa kama kusaidia shughuli yoyote ya Serikali lakini kuna fedha ambazo zinaletwa kwa ajili ya mradi fulani. Zile ambazo zinakuja kwa shughuli maalum, hazigawanyiki. Zinazogawanyika ni zile ambazo zimekuja katika kusaidia shughuli za ujumla tu za Serikali.

Napenda kabisa niwahakikishieni Waheshimiwa Wabunge, kwa wale ambao labda hawafahamu, pande zetu mbili za Muungano zinashughulikia jambo hili na

tunalitekeleza vizuri sana. Kwa upande wa Zanzibar pale ambapo wamepata matatizo labda ya upungufu wa fedha au upungufu wa jambo lolote, Serikali ya Muungano imekuwa ikisaidia sana na wala hatuna ugomvi.

Kwa hiyo, lisije likaonekana kwamba hakuna lolote linalofanyika katika kugawa hizi fedha za misaada na Tume yetu ya Fedha ambayo sasa inafanya kazi chini ya Mheshimiwa William Shellukindo, nina hakika wanalifanyia kazi jambo hili vizuri sana, wanalisimamia vizuri na nina hakika tungemwambia alizungumzie angeeleza vizuri zaidi. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali linalofuata. Mheshimiwa Ali Mussa.

Na. 62

**Umaskini Uliokithiri katika Nchi Yetu**

**MHE. ALI MACHANO MUSSA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeanza kuchukua hatua za kukabiliana na umaskini uliokithiri katika nchi yetu na kwa kuwa hali ya umaskini uliokithiri iko zaidi katika Visiwa vya Tumbatu, Mafia, Kojani, Visiwa vilivyoko katika Ziwa Victoria na kadhalika:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi wa maeneo hayo ili nao waondokane na umasikini huo?

(b) Je, ni mara ngapi Serikali imetoa msaada kwa wananchi wanaoishi Visiwani hususan Kisiwa cha Tumbatu?

(c) Endapo Serikali imeshindwa kuwasaidia wananchi wanaoishi katika Visiwa nilivyovitaja, je, ni mara ngapi imeshawahi kufika katika Visiwa hivyo angalau kuwapa maelekezo ya kitaalam ya jinsi ya kukabiliana na hali ya umaskini huo uliokithiri?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumjibu Mheshimiwa Ali Mchano Mussa, Mbunge wa Tumbatu, swali lake lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inao mpango wa kutekeleza mkakati wa kuunguza umaskini nchini unaolenga maeneo yote hususan yale yenye umasikini uliokithiri, ikiwa ni pamoja na Visiwani. Katika kufanya hivyo, Serikali inahimiza Viongozi katika ngazi zote kuhamasisha wananchi ili washiriki kikamilifu katika kujiletea maendeleo yao. Jukumu la Serikali ni kuweka mazingira mazuri, ikiwa ni pamoja na kuimarisha miundombinu.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu la kimsingi la kuondoa umaskini hususan wa kipato, linabaki mikononi mwa wananchi wenyewe. Kama nilivyoeleza kwenye sehemu (a) hapo juu, jukumu la Serikali ni kuweka mazingira mazuri ya utendaji. Serikali imekuwa ikitoa huduma hizo na wala siyo kutoa misaada ya moja kwa moja kwa wananchi wanaoishi kisiwani Tumbatu. Huu ni utaratibu unaotumika nchini kote.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kupitia Serikali za Mitaa inafika katika kila kona ya nchi yetu. Aidha, wataalam wa sekta za kipaumbele katika vita dhini ya umasikini yaani elimu, afya, maji, kilimo, ujenzi na utawala bora wanafanya kazi katika kila Wilaya ya nchi yetu kwa kushirikiana na wananchi. Wataalam hawa wanapeleka huduma za kitaalam kwa kila kona ya nchi yetu vikiwemo Visiwa vyote vilivyotajwa hapo juu. Kwa sasa umuhimu umewekwa pia wa ushiriki wa asasi za jamii na sekta binafsi katika kuunga mkono juhudi za Serikali kuleta maendeleo nchini. Napenda nichukue nafasi hii kuwapongeza wananchi kote nchini kwa kushiriki kwao kikamilifu katika kutekeleza miradi ya maendeleo yao.

Hata hivyo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushirikiano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inaendelea kuwaelimisha wananchi wanaoishi visiwani kuhusu mbinu mbalimbali za kuondokana na umasikini. Hayo hufanyika pia katika sehemu nyingine nchini. Utaratibu huu utaimarishwa zaidi na mpango wa *Poverty Reduction Strategies Extension Services* unaoandalia na ambao tunatarajia kuanza kutekeleza karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa taarifa pia kuwa kama ilivyo kwa Tanzania Bara, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeandaa kuzindua mpango wa kupunguza umaskini Zanzibar, yaani *Poverty Reduction Plan* ambao umebainisha maendeleo ya kipaumbele kwa upande wa Visiwani. Kwa sasa mpango wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa mpango huo unaandaliwa.

Aidha, miradi ya *TASAF, SELF* na *NIGP* iliyobuniwa na Serikali inaunga mkono juhudi za wananchi katika kujiongezea kipato chao na kuleta maendeleo yao kwa ujumla. Kwa kuzingatia hilo Mheshimiwa Makamu wa Rais alifanya ziara Pemba ili kukagua na kuzindua miradi ya *TASAF*.

Aidha, Mheshimiwa Makamu wa Rais alifanya ziara ya aina hiyo Zanzibar (Unguja) ambako alikagua na kuzindua miradi ya kuondoa umaskini ikiwepo ya *TASAF* na mingineyo. Aidha, Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Makamu wa Rais (Kuondoa Umaskini) alipata bahati ya kufuatana na Mheshimiwa Makamu wa Rais kwenye ziara hiyo. *(Makofi)*

**MHE. ALI MACHANO MUSSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na swali ambalo nitaendelea kuliuliza, nampongeza Makamu wa Rais kwa kutembelea Tanzania nzima. Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kama Makamu wa Rais alivyotembelea Tanzania nzima kutembelea Kisiwa cha Tumbatu Zanzibar ili aone hali halisi ilivyo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafurahi kusikia kwamba yeye kwa maoni yake ya kweli kabisa kwamba amempongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais kutembelea nchi nzima na bila shaka pongezi hizo zitamfikia. Ya pili kwamba na mimi niende Tumbatu ninakubali mwaliko wake, lakini nafasi ya Makamu wa Rais kutembelea nchi nzima ni kubwa zaidi kuliko ya Waziri. Asinilinganishe mimi na Makamu wa Rais, mimi nitakuwa chini hapo na nitafanya ziara hiyo. *(Makofi)*

Na. 63

**Dagaa Kutofaa kwa Chakula cha Kuku**

**MHE. JAMES P. MUSALIKA (k.n.y. MHE. DR. CHEGENI R. MASUNGA)** aliuliza:-

Kwa kuwa wakati wa mkutano wa Bajeti 2002/2003 Serikali ilitamka kwamba dagaa hawafai kwa chakula cha kuku, na kwamba kuku wanaokula dagaa hutoa harufu isiyowafurahisha walaji wa nyama ya kuku hasa katika soko la kuku kwa sasa na kwamba Serikali imeamua kufuta kodi na ushuru kwa zao la soya ili kutoa nafasi kwa wafugaji wa kuku kuingiza zao hilo nchini kwa bei nafuu:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba kauli kama hiyo imekuja katika muda usio muafaka kwani wapo Watanzania wengi wanaoendesha maisha yao kutokana na uvuvi wa dagaa katika maeneo ya Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika, ambao wanatumika kama chakula na kwa biashara na kwamba sasa watakosa soko?

(b) Je, Serikali haioni kwamba ingekuwa vyema kuweka kwanza mikakati ya kuwasaidia wananchi ili waweze kulima soya hapa nchini ili manufaa yaliyotangazwa yaweze kutimizwa pasipo kuathiri soko la dagaa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Chegeni Masunga, napenda kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Dagaa ni chakula chenye protini yenye asili ya nyama ambayo ni muhimu sana kwenye kutengeneza mchanganyiko wa chakula cha kuku. Hata hivyo, sehemu ya dagaa katika mchanganyiko huu ni muhimu pale isipozidi asilimia tano. Tatizo ni kwamba wafugaji walio wengi wanaochanganya vyakula vya kuku huweka dagaa zaidi ya kiwango cha asilimia tano na hivyo kusababisha harufu ya dagaa kwenye nyama ya kuku na mayai yanapoliwa na binadamu.

Baada ya utangulizi huo sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Chegeni Masunga, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kauli ya Serikali haikuwa na maana ya kuwazuia wafugaji wasitumie dagaa kwenye chakula cha kuku. Lengo lilikuwa ni kuwatahadharisha wafugaji na wasindikaji wa vyakula vya kuku kuzingatia viwango vinavyopendekezwa na wataalam ili kuku wao wasikose soko kwa wateja ambao hawapendi harufu ya dagaa kwenye nyama na mayai. Ni dhahiri kwamba kama wateja wa nyama ya kuku na mayai wataacha kununua bidhaa hizo, wafugaji pia hawatanunua chakula chenye mchanganyiko wa dagaa. Hivyo hivyo wazalishaji wa chakula nao wataacha kununua dagaa, matokeo yake ni kwamba soko la dagaa litashuka, jambo ambalo tusingependa litokee.

(b) Serikali imekuwa ikihamasisha kilimo cha soya hapa nchini na tayari kimeshamiri hasa kwenye Mikoa ya Morogoro, Lindi, Mtwara na Ruvuma. Hata hivyo, uzalishaji wa soya hapa nchini bado hautoshelezi mahitaji ya binadamu pamoja na mifugo. Kwa hiyo, utoaji wa kodi na ushuru kwenye soya umelenga kuongeza upatikanaji wa bidhaa hiyo ili kuziba pengo lililopo sasa. Aidha, kuongezeka kwa matumizi ya soya kwa ajili ya mifugo kutasababisha mahitaji ya soya kuwa makubwa na hivyo kunufaisha wakulima.

(c) Kama nilivyoeleza katika jibu la (a) na (b) hapo juu, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa maamuzi ya Serikali kuhusu wafugaji wa kuku na wasindikaji wa vyakula vya kuku kuzingatia viwango hayataathiri wananchi wa mikoa iliyopo ukanda wa Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria. Matumizi ya dagaa katika utengenezaji wa vyakala vya kuku na mifugo mingine utaendelea. Kinachosisitizwa na Serikali ni kwa watengenezaji hao kuzingatia viwango vya kitaalam vinapendekezwa ili kulinda soko la bidhaa za mifugo ndani na nje ya nchi.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi. Nashukuru pia majibu ya Naibu Waziri. Kwa kuwa sera ya sasa ni kuondoa umaskini hasa ifikapo 2025 na kwa kuwa wavuvi hawa wa dagaa wako katika vita vya kuondoa umaskini isipokuwa hawana teknolojia nzuri ya kuwezesha dagaa hao waweze kuuzwa kama ambavyo makusudio yapo, je, Serikali haiwezi ikawapa nyenzo na ufundi na utaalam wa kufanya ili soko la dagaa lisiweze kuanguka nchini na kuondoa umaskini ifikapo 2025?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali inaazimia kuondoa umaskini ifikapo mwaka 2025. Jitihada za Serikali ambazo zinafanyika ni pamoja na kusaidia wavuvi wa dagaa kwa kuwapatia utaalam kupitia vyuo vyake mfano Chuo cha Nyegezi ambacho kinafundisha uvuvi wa kisasa na maeneo mengine. Kama tunavyofahamu Sera ya Serikali sasa hivi sio kujihudisha moja kwa moja katika biashara.

Hivyo, Serikali haitafikia wakati ikawapa watu wavu au boti kwa sababu siyo Sera yetu. Sera yetu ni kwamba maeneo hayo yanafanywa na wananchi kwa kutumia nguvu zao wenyewe binafsi au katika vikundi.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuuliza swali la nyengeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa imedhihirika duniani

sasa kitaalam kwamba soya ni zao moja ambalo linaweza likatoa maziwa mazuri na yanayotumika na hayana magonjwa yoyote na nchi nyingine sasa wanaanza kuanzisha mamlaka ya zao kama hilo. Je, Serikali haioni sasa umefika wakati wa kuhimiza zao hili katika nchi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoonyesha kwenye jibu la msingi, soya sasa hivi inalimwa sehemu nyingi sana. Ni karibu Tanzania nzima, ila sehemu nyingine sikuzitaja, kwa sababu ndiyo wanaanza tu na ni kweli maziwa yanaweza kutengenezwa kutokana na soya.

Lakini kama inavyoeleweka hivi vitu vinaongozwa na *demand* na *supply.* Kwa sasa hivi kidogo ukimwambia mwananchi maziwa haya ni *re-consitituted* anakuwa kidogo na wasiwasi, bado tunataka tunywe maziwa asilia ya nyombe.

Kwa hiyo, *demand* itakapoelekeza hivyo nina hakika matumizi ya soya kwa kutengeneza maziwa na kadhalika yatafuata. Kwa hiyo, tusubiri soko lihitaji aina hiyo ya mazao na hivyo wananchi wataongeza bidii katika kuzalisha *soya beans.*

Na. 64

**Barabara ya Mwanza-Dar es Salaam-Mtwara**

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA (k.n.y. MHE. MARIA D. WATONDOHA)** aliuliza:-

Kwa kuwa tangu tupate Uhuru kumbukumbu za *Hansard* zinaonyesha kwamba Mradi wa barabara kwenda Kusini ulijulikana kama barabara ya Dar es Salaam-Kibiti-Lindi-Mingoyo, lakini Serikali ya Awamu ya Tatu katika kipindi cha pili imebadili mradi huo na kuitwa Mradi wa barabara wa Mwanza Dar es Salaam-Mtwara:-

(a) Je, ni sababu gani zimeifanya Serikali ibadili mradi huo wa maeneo ya Kusini na sasa uanzie Mwanza-Mtwara?

(b) Je, Serikali inapobadili kauli zake haioni kwamba inawachanganya wananchi hasa wa Kusini ambao hawana usafiri wa uhakika kwa zaidi ya nusu ya mwaka?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maria Watondoha, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jina la mradi wa barabara ya Dar es Salaam-Kibiti-Lindi-Mingoyo kama ilivyo miradi mingine halijabadilika kwani unatajwa kwa kuzingatia majina ya miji inayounganishwa na mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2001 kwa kupitia Waraka Na. 5 wa 2001 wa Baraza la Mawaziri, Serikali ilipitisha mpango wa kutekeleza mradi maalum wa barabara kuu unaohusisha sehemu ya barabara ya Somanga-Masaninga-Nangurukuru-Lindi Mingoyo ambayo ni sehemu ya mradi Dar es Salaam-Kibiti-Lindi-Mingoyo na vile vile sehemu ya Dodoma-Manyoni-Singida ambayo ni sehemu ya barabara ya Dar es Salaam-Mwanza.

Aidha, kwa kipindi hicho hicho Serikali imekuwa ikitekeleza miradi mingi iliyopo kati ya Mingoyo na Mwanza kama vile Dar es Salaam - Mlandizi-Morogoro, Morogoro-Dodoma, Singida-Shelui, Shelui-Nzega, Nzega-Tinde-Shinyanga-Ilula na Ilula-Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia mafanikio makubwa ya kutekeleza mradi mkubwa kama huo unaounganisha sehemu mbili za nchi zilizo mbali kwa urefu, Serikali imekuwa ikunganisha miradi yote hiyo kama mradi wa barabara wa kutoka Mwanza hadi Mtwara au Mtwara hadi Mwanza ambao unalenga kukamilika mwaka 2006/2007 na hii haibadilishi ratiba ya utekelezaji wa mradi wa Dar es Salaam-Kibiti-Lindi-Mingoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanahitaji barabara na ndio kazi inayofanywa na Serikali sasa na si namna majina ya mradi wa barabara yanavyotamkwa inaweza mradi ukawa Mwanza-Mtwara au Mtwara-Mwanza maana yake inabaki ile ile na wala Serikali haijabadili kauli yake na kuwadanganya wananchi. *(Makofi)*

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mhshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa chimbuko la mradi huu wa barabara ya Mwanza-Mtwara ni barabara ya Mingoyo-Kibiti-Lindi.

Je, Serikali haioni kwamba itatenda haki barabara hii ikianza kujengwa Mtwara-Dar es Salaam halafu baadaye kwenda Mwanza?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu la msingi la Mheshimiwa Naibu Waziri ilikuwa inazungumzia ujenzi wa barabara. Suala hapa si barabara ya Dar es Salaam-Kibiti-Lindi. Suala ni barabara kujengwa na ni barabara za Tanzania nzima.

Kwa hiyo, ningependa nimweleze Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara ya Kibiti-Lindi inajengwa na hadi sasa kuna makandarasi kutoka Dar es Salaam hadi Mtwara. Sasa anapozungumza barabara ianzie Mtwara wakati mkandarasi kutoka Mingoyo hadi Mbwemkuru kuna Mkandarasi yuko pale kutoka Nangurukuru hadi Mbwemkuru kuna Mkandarasi. Somanga-Matandu kuna Mkandarasi, kwa hiyo, sifahamu ianzie wapi.

Mimi ningeomba suala hapa la kuzungumza na wananchi wa Tanzania wote wanahitaji barabara. Wananchi wa Tunduma-Sumbawanga-Kigoma wanahitaji barabara, wananchi wa Iringa kwenda Arusha wanahitaji barabara. Kwa hiyo, tuache ya kwamba

inaanzia Mtwara, inaanzishwa Lindi, inaanzia Mingoyo, wananchi wanahitaji barabara, hilo ndilo suala la msingi. Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. *(Makofi)*

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Nakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kunipa nafasi hii niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nilitaka kuuliza swali moja la nyongeza ambalo linatokana na mkutano wetu wa mwanzo wa kikao hiki cha Bunge. Tuliarifiwa kwamba inavyoonekana kutokana na ukame Serikali itabidi iwe inatenga shilingi bilioni 17 kila mwezi kwa ajili ya kugharamia mafuta kwa ajili ya umeme. Sasa nilitaka kuuliza kwa kuwa tulikuwa tumekwishaahidi tutakuwa tunatenga shilingi bilioni 1.8 kila mwezi kwa ajili ya ujenzi wa barabara kutoka Mingoyo mpaka huko Mwanza, je, hii haitaathirika na Serikali inatoa kauli gani kuhusu fedha hizi ambazo haki yake ziwe zimepangwa kwa ajili ya kujenga barabara hii?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yanayotekelezwa sasa hivi ni pamoja na ujenzi wa barabara ambao ulipitishwa na bajeti na ukapitishwa na Wabunge hapa katika Bajeti ya mwaka 2002/2004 na Serikali kwa ujumla huwa haibadilishi maamuzi yaliyopitishwa na Wabunge yakiwemo maamuzi yaliyopitishwa na Mheshimiwa Raynald Mrope.

Kwa hiyo, fedha zinazotengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya karibu kilomita 500 ambayo itahusisha barabara za Kusini na barabara zingine katika nchi nzima ambazo zina urefu wa zaidi ya kilomita 35,000 ziko pale pale. *(Makofi)*

Kwa hatua zinazoendelea sasa hivi kandarasi katika barabara hizo za Kusini yupo na wamekwishalipwa fedha na fedha zitakazotengwa kwa mradi mzima ni bilioni 210 na katika mafanikio ya makusanyo mazuri yanayofanywa sasa hivi katika mwezi ulioyopita, makusanyo kwa mwezi yaliyokuwa ni bilioni 126 ambapo Serikali imevunja rekodi ukilinganisha na makisio. *(Makofi)*

Kwa hiyo, fedha za barabara zipo na barabara zitaendelea kutengenezwa na katika mwaka 2005/2006 barabara hiyo itakuwa imekamilika kutengenezwa kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Na. 65

**Ujenzi wa Barabara ya Chanika-Mvuti-Mbande**

**MHE. RICHARD M. NGASSA (k.n.y. MHE. DR. MILTON M. MAHANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa wakati Serikali ilipokuwa ikijibu swali langu Na. 85 Bungeni hapo tarehe 6 Februari, 2002, pamoja na barua ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kwangu yenye kumbukumbu namba *BC.128/565/01/03* ya tarehe 2 Oktoba, 2002, Serikali iliahidi kuijenga barabara ya Chanika-Mvuti-Mbande kwa kiwango cha lami?

Je, Serikali inaweza kuwahakikishia wananchi wa Jimbo la Ukonga, kwamba barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami na kukamilishwa ifikapo Oktoba, 2005?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga, Mbunge wa Ukonga, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati najibu Bungeni swali la Mheshimiwa Mbunge Na. 85 tarehe 6 Februari, 2002, nilitamka wazi kuwa Wizara yangu itaendelea na juhudi za kutafuta fedha kwa ajili ya kuijenga barabara ya Chanika-Mvuti-Mbande kwa kiwango cha lami.

Katika swali la nyongeza ambapo Mheshimiwa Mbunge alitaka kupatiwa ufafanuzi zaidi juu ya hizo juhudu za Serikali katika kutafuta fedha za kuwekea lami kwenye barabara hii niliweka bayana vyanzo vya mapato vya Serikali ambavyo ni pamoja na kodi za wananchi, mikopo, misaada ya wahisani na kadhalika.

Aidha, hata katika barua yangu kwa Mheshimiwa Mbunge yenye Kumb. Na. *BC.128/565/01/3* ya tarehe 2 Oktoba, 2002, nilisisitiza msimamo huo huo wa Serikali kwamba matengenzo ya barabara hiyo kwa kiwango cha lami yatafanyika kadri fedha itakavyokuwa inapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa barabara hii ni mkubwa, ndio maana Wizara yangu kupitia wakala wa barabara *(TANROADS)* Mkoa wa Dar es Salaam imeendelea kuifanyia matengenezo ya viwango mbalimbali ili kuhakikisha inapitika muda wote.

Aidha, kama nilivyosema awali, barabara hiyo imepangwa kujengwa kwa kiwango cha lami na Serikali imeanza kuchukua hatua zifuatazo:-

(i) Katika mwaka wa fedha 2002/2003, kiasi cha shilingi milioni 300 kilipangwa na kutolewa kwa lengo la kuanza kujenga barabara hiyo kwa lami.

(ii) Katika mwaka huu wa fedha 2003/2004, kiasi cha shilingi milioni 120 kilichopangwa tayari kimekwishatolewa kwa ajili ya kuendelea na kazi hizo ambazo zinaendelea hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaona kuwa Serikali inayo nia na dhamira ya kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami lakini tatizo kubwa ni ufinyu wa Bajeti. Endapo fedha zitapatikana barabara hii inaweza kukamilika katika muda mfupi sana.

**MHE. ATHUMANI S.M. JANGUO:** Nakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi kuliza swali la nyongeza, baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri na kwa kuwa barabara ya Chanika-Mbande ni mwendelezo wa barabara inayotoka Pugu-Chanika mpaka Mbande ambayo kutoka Chanika inagawanyika kwenda Msimbu na Masaki katika Wilaya ya Kisarawe.

Je, zitakapopatikana fedha yuko tayari sehemu hii ambayo ni barabara hiyo hiyo kuijenga kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kila siku nia yake ni kuhakikisha kwamba barabara nzuri zinatengenezwa kwenye nchi hii na kwa hakika kama tungekuwa na pesa nadhani Waheshimiwa Wabunge hata wasingetuomba juu ya barabara hizi, tungezitengeneza kwa dhamira nzuri kabisa.

Kama nilivyosema barabara hii sasa hivi tunayotengeneza ina ufinyu wa Bajeti. Kama pesa zikipatikana na uwezekano wa kutengeneza barabara hiyo ipo mpaka Kisarawe tunamhakikishia Mheshimiwa Janguo, tutafanya hivyo endapo Bajeti itakuwa nzuri.

Na. 66

**Uendelezaji wa Viwanda Vidogo Vidogo vya Nguo Nchini**

**MHE. JANET B. KAHAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa nchi yetu ni miongoni mwa nchi za Afrika zinazozalisha pamba nyingi, na kwa pamba hiyo huuzwa nje kama malighafi:-

(a) Je, ni lini Serikali itahimiza na kuhakikisha kwamba, wadau wanaohusika wanaandaa na kutekeleza mpango kabambe *strategic master plan* wa kutumia pamba yetu kutengeneza nguo na bidhaa nyingine zitokanazo na zao hilo, ili tuuze bidhaa za viwandani kuliko kuendelea kuuza pamba ghafi na kupoteza mapato makubwa ya nyongeza ya thamani, na kama utaratibu huo upo, je, Wabunge wanaweza kupatiwa nakala yake?

(b) Je, Serikali ina fahamu kwamba, mpango unaotumiwa na nchi za Asia, kama vile Thailand, China, India na kadhalika wa kutengeneza nguo na vitambaa unatokana na kuanzishwa kwa viwanda vidogo vidogo *small and medium handlooms/powerlooms* kwa wingi kwa mauzo ya bidhaa zao ndani na nje?

(c) Je, Serikali inafahamu kwamba, nguo ni bidhaa mojawapo inayouzwa kwa wingi kwenye soko la *AGOA* na kwamba Tanzania inaweza kufaidika na soko hilo kwa kuchukua hatua za makusudi za kutengeneza bidhaa za pamba kwa wingi kwa ajili ya soko hilo na kwamba kama viwanda vya *Handlooms/Powerlooms* vikianzishwa kwa lengo la kutengeneza bidhaa za kuuza nje/ndani pia vitasaidia kutoa ajira kwa wingi hasa

kwa vikundi vya akina mama wengi wanaohangaika na utengenezaji wa vikapu na mikeka tu?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumjibu Mheshimiwa Janet Kahama, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali mara zote imekuwa ikihimiza utumiaji wa pamba yetu kutengeneza nguo na bidhaa nyingine zitokanazo na pamba, na hii ili kuzuia uuzaji wa pamba ghafi nje. Ni kwa sababu hii Serikali iliwekeza katika viwanda vingi vya nguo kwa madhumui ya kutumia pamba yetu. Aidha, sera endelevu ya maendeleo ya viwanda *(Sustainable Industrial Development Policy)* inatoa kipaumbele katika viwanda vya kusindika bidhaa za kilimo ikiwa ni pamoja na viwanda vya nguo.

Katika kutekeleza mpango huo wa sera endelevu ya maendeleo ya viwanda, wawekezaji wamehamasishwa kununua viwanda vya nguo vilivyobinafsishwa ili wavifufue na kuviendeleza. Kutokana na juhudi hizo za Serikali viwanda 8 vilivyokuwa vya umma tayari vinafanya kazi na kutoa ajira. Viwanda hivyo ni *Mbeyatex, Mutex, Mwatex, Sunguratex, Kiltex, Morogoro Canvas* Kiwanda cha Mablangeti na Kiwanda cha Mwana ambacho sasa kinakarabatiwa. *(Makofi)*

(b) Serikali inafahamu kuwa nchi kadhaa za Asia zimeweza kutengeneza nguo na vitambaa kwa kutumia teknolojia ya useketaji kwa kutumia *Handlooms/Powerlooms.* Pia Tanzania imekuwa ikitumia teknolojia hii. Aidha, watalamu wetu wamepata mafunzo katika baadhi ya nchi zenye utaalamu huo na kuwa wana ujuzi wa kutengeneza *handlooms* zenyewewe.

Aidha, kwa sasa utaalam wa kutumia *handlooms* umeenea na tayari waseketaji wako mbioni kuanzisha ushirika wao utakaojulikana kama, *handloom weavers of Tanzania.* Ushirika huu utatumika kukusanya na kuuza bidhaa zao ndani na nje ya nchi.

(c) Serikali inafahamu kwamba nguo ni bidhaa mojawapo inayouzwa kwa wingi kwenye soko la *AGOA* na ndio saabu Serikali imekidhi masharti husika na kuhakikisha Tanzania tunapata viza au fursa ya kupeleka nguo Marekani katika utaratibu wa *AGOA.* Pamoja na hayo Serikali imewahamasisha wawekezaji kutoka nje ili waanzishe viwanda vya nguo na tayari viwanda viwili vimeanza ambavyo ni *NIDA Textile Mill* na *Star Apparel* ambayo ipo Ubungo. Aidha, kiwanda cha *Sunflag Ltd.* cha Arusha tayari kinauza bidhaa zake katika soko la *AGOA.*

**MHE. JANET B. KAHAMA:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, bado ninaomba kumshauri Naibu Waziri na Wizara yake ili waweze kukubaliana na mimi kuwa pamoja na hayo hivyo viwanda vidogo vidogo basi wangejitahidi kuhakikisha kuwa wanaweza kuweka nguvu zaidi na hasa katika maeneo ambayo wanalima pamba na vile vile katika maeneo ya miji mikuu kama vile Jiji la Dar es Salaam, Tanga, Mwanza na kadhalika. *(Makofi)*

Swali la pili, kwa kuwa mpango huu wa kumkwamua mwanamke na vijana ni mpango ambao unashirikisha sio Wizara ya Viwanda na Biashara tu, lakini pia kuna Wizara nyingine kama Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na hata Ushirika na Masoko. Je, Waziri anaweza akahakikisha kuwa Wizara hizo kwa pamoja ziweze kukaa na kwa nguvu moja waongeze viwanda vidogo vidogo hivi kuwasaidia wananchi kwa kuwakwamua waweze kupata ajira? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naona kama maswali yake yote yamekuwa ni ushauri na ninashukuru sana kwamba Serikali ijaribu kuweka mkazo katika maeneo yanayozalisha pamba kuanza viwanda vidogo vidogo.

Naomba kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba huo ndiyo mpango maalum wa Serikali na sasa hivi viwanda vidogo vidogo vimepata fedha kiasi cha shilingi milioni 500 na tunataka tuzielekeze katika maeneo kama hayo ya *powerlooms* pamoja na maeneo mengine ya vyakula kama nilivyoongea wiki iliyopita.

Isipokuwa nawaomba Waheshimiwa Wabunge maeneo yote wawahamasishe akina mama, vijana kujitokeza katika maeneo ya *SIDO* ili kuweza kupata ushauri kuhusiana na hizi *handlooms.*

Pia kwa kuongezea ni kwamba tumefanya maonyesho kanda zote za nchi nzima na zilikuwepo bidhaa mbalimbali zilizotengezwa na handlooms hasa Mkoa wa Morogoro umetoa bidhaa nzuri sana na hii ni juhudi mojawapo ya Serikali kuhakikisha kwamba zinapata masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali la (b) kwa kuunganisha na sehemu ya (a) ni kwamba Serikali ni moja isipokuwa tutaongeza mkazo kuwaomba Wizara ya Maendeleo ya Jamii, kutusaidia kwa fedha ambazo walizo nazo kuwakopesha hawa wawekezaji wadogo wadogo na pili tutawaomba Wizara ya Ushirika na Masoko kutusaidia kupata masoko kwani vikoi vinavyotengenezwa ni vizuri sana na soko ndilo linalokosekana. Nashukuru Mheshimiwa Mwenyekiti.

Na. 67

**Ukodishaji wa Kiwanda cha Ndege - *KIA***

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imekodisha kiwanja cha ndege cha *KIA* kwa kampuni ya nje kwa mkataba wa kukiendesha:-

(a) Je, Serikali inaweza kutueleza kwamba ni kampuni gani iliyokodishiwa kiwanja hicho?

(b) Je, kiwanja hicho kina aina gani za vyanzo vya kukiingizia mapato na viwanaweza kuingiza kiasi gani cha fedha kwa mwaka?

(c) Je, kampuni hiyo inalipa kiasi gani kwa mwaka, na mkataba huo ni wa miaka mingapi?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya, Mbunge wa Kwela, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni iliyokodishiwa kiwanja cha ndege cha *KIA* ni *Kilimanjaro Airports Development Company Ltd. (KADCO)*. *KADCO* ni kampuni iliyoandikishwa chini ya Sheria ya Makampuni *(Cap.212)* na imepewa hati Na. 33616 ya tarehe 11 Machi 1998. Wenye kumiliki hisa kwenye kampuni hii ni Serikali ya Tanzania 24%, *Mott MCDonald International* 41.4%, *Inter Consult Ltd* 44.6% na *South African Infrastructure Fund* 30%.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya ukodishaji kiwanja cha *KIA* kilikuwa kinategemea ruzuku kutoka Serikalini. Baada ya ukodishaji kiwanja kimekuwa kinajiendesha chenyewe kwa kutumia vyanzo vyake mbali mbali. Vyanzo hivyo ni pamoja na:-

(i) Mapato yanayotokana na kutua na maegesho ya ndege *(landing and parking fees).*

(ii) Malipo yanayotokana na tozo kutoka kwa abiria malipo ya huduma ya mawasiliano na mitambo ya anga.

(iii) Ada wanazolipa wapangaji kutokana na kukodisha maofisi na sehemu za biashara.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, *KADCO* kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2001 imelipa Serikali Kuu na Tawala za Mitaa jumla ya shilingi milioni 344.6 milioni 334.6 na mwaka 2002 jumla ya shilingi 163.9 milioni zimelipwa kama kodi iliyotokana na mapato yake mbalimbali kama vile *Withholding tax, Value Added Tax (VAT), Payroll tax* na kadhalika.

Kiwango hiki cha kodi kinatazamiwa kuongezeka baada ya Wizara ya Ardhi, Maendeleo ya Makazi ikishirikiana na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege watakapokamilisha zoezi linaloendelea la kuweka viwango vya kodi ya ardhi *(Land Rent)* itakayotozwa ardhi ya viwanja vya ndege nchini. Mkataba huo kati ya Serikali na *KADCO* ni wa miaka 25 kuanzia mwaka 1998.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza katika swali langu nilikuwa nimependa kujua je, Serikali imeingia mkataba na kuwa na kiwango kimoja kitakacholipwa mwaka hadi mwaka kama hawa wanapata faida au hawapati faida lakini serikali inapata malipo hayo?

Pili, anaweza kutufafanulia kwa nini takwimu zimetofautiana kati ya mwaka na mwaka, kwa mfano kuna wakati zimelipwa shilingi milioni 334 na tena mwaka mwingine zikalipwa 169. Hiyo tofauti yake inakujaje?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwa sababu makubaliano yaliyoingiwa ni yale ambayo hayakuhusisha faida au hasara inayopatikana kwa sababu tumekubaliana kiwango kiwe kile kinacholipwa, ni kiwango hicho hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tofauti tunayoiona ya milioni 334.6 na milioni 163 inatokana na mapato yanayotokana na kutua kwa ndege, inawezekana wakati huu wa pili utuaji wa ndege ulikuwa sio wa kuridhisha kwa hiyo mapato yatokanayo na kutua kwa ndege maegesho yalipungua.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni miaka miwili sasa tangu nilipomwandikia Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi kuhusu upungufu mkubwa wa mkataba wa Kiwanja cha *KIA* hatua iliyopelekea mimi na Mheshimiwa Waziri kutembelea kiwanja hiki na mkataba ambao ulikuwa umesababisha kero kubwa ikiwepo kutoa eneo la ardhi la zaidi ya kilomita za mraba 109 na hivyo kutoa usumbufu mkubwa kwa wananchi wa Vijiji vya Tindigani, *Sanya Station,* Mtakuja, Chemka na Chekimaji, je, ni lini sasa Mheshimiwa Waziri atatoa taarifa rasmi kuhusu ukweli na upungufu mkubwa wa mkataba wa *KIA* ambao umekwishalalamikiwa katika Bunge hili mara kadhaa lakini usiri mkubwa umekuwepo kwenye mkataba huu? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dosari zilizojitokeza katika mkataba huo hazikugunduliwa na Mheshimiwa Freeman Mbowe, bali na Serikali yenyewe katika taratibu za kawaida za kufanya mapitio ya mikataba. Kutokana na hilo, Wizara iliagizwa kufanya majadiliano upya, kupitia na kudurusu huo mkataba wa *KADCO.* Tukaainisha mapungufu 48 na kutoa mapendekezo kwa *KADCO* na kati ya hayo 48 mapungufu 46 tayari tumekwishakubaliana namna ya kuyatatua. Haya mawili yaliyobaki yanahusu jibu la swali la nyongeza la Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, kuhusu malipo ya kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni namna ya kudurusu huo mkataba katika vipindi vya kila miaka kumi na namna gani tutakamilisha huo mkataba ifikapo mwisho wa uhai wa mkataba wenyewe.

Kwa hiyo, hakuna usiri wowote, Mheshimiwa Freeman Mbowe, anaweza kuniona, nina huo mkataba na jinsi tulivyoudurusu, aupitie na ninao hapa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongezea tu kidogo juu ya majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri. Eneo ambalo nataka kuongezea ni hili la ardhi kwa sababu Mheshimiwa Freeman Mbowe amezungumza kana kwamba kuna ardhi ya wanavijiji imechukuliwa na kampuni hiyo ambayo inakodisha kiwanja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi hiyo ambayo inahusika ndilo eneo lililokuwepo la Kiwanja cha *KIA*. Kwa hiyo, hakuna ardhi mpya iliyochukuliwa, ni ardhi ile ile ambayo ilikuwa ni eneo la Kiwanja cha *KIA*. *(Makofi)*

Na. 68

**Huduma ya Simu Wilaya ya Serengeti**

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA** aliuliza:-

Kwa kuwa Huduma za Simu za *TTCL* katika Wilaya ya Serengeti zinapatikana katika Mji wa Mugumu na katika *Institutions* zilizoko katika Hifadhi ya Serengeti:-

(a) Je, Serikali kupitia Kampuni ya Simu Tanzania *(TTCL)* ina mpango gani wa kupeleka huduma ya simu kwenye Miji mingine midogo ya Isenye, Natta, Nyakitono, Nyichoka, Burunga, Kisangura, Machochwe, Rug'abure, Kibachebache, Ring'wani, Iramba, Kemugesi, Majimoto, Bulenga na kadhalika?

(b) Je, kazi ya kuipatia Miji hiyo simu itaanza na kumalizika lini na itagharimu fedha kiasi gani?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Mbunge wa Serengeti, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Serengeti huduma ya mawasiliano ya simu hupatikana Mjini Mugumu na katika Taasisi zilizoko katika Hifadhi ya Serengeti. Mpango wa uboreshaji wa huduma ya mawasiliano ya simu Miji midogo na Vijiji upo ila utekelezaji wake unategemea upatikanaji wa fedha. Fedha zitakapopatikana Miji midogo yenye mwelekeo wa kibiashara itafikiriwa kwanza.

Hivyo, Miji midogo ya Isenye, Natta, Nyakitono, Nyichoka, Burunga, Kisangura, Machochwe, Rugabure Kibachebache, Ring'wani, Kemugesi, Iramba, Majimoto na Bulenga, itapewa huduma ya simu za kisasa kama itakidhi masharti ya kibiashara.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kuipatia Miji hiyo simu itaanza baada ya kufanya tathmini ya kibiashara kwa Miji aliyoisema na tathmini hiyo itafanyika mwaka huu. Ikionekana inakidhi masharti ya kibiashara Miji hiyo itaingizwa katika mpango wa maendeleo na kazi itaanza kutekelezwa.

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, Serengeti ni sehemu ambayo utalii umeshamiri sana na Jimbo hilo bado halijapata simu za mkononi kama vile *Vodacom, Mobitel* na *Celtel,* je, Serikali inaweza kutusaidia kuyashawishi makampuni hayo ili yaweke simu za mkononi katika Jimbo letu la Serengeti? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inakubali kwenda kuwashirikisha na kuwahamasisha *Mobitel* na *Celtel* au Makampuni haya yote ya simu waone umuhimu wa kupeleka simu katika maeneo haya.

Tumwombe tu Mheshimiwa Mbunge na yeye aendelee kuwahamasisha wananchi wake ili watakapokwenda wenye huduma hizi za *Mobitel* wakute wako tayari wanahitaji huduma hizi.

Na. 69

**Usambazaji wa Umeme Vijijini**

**MHE. SAMWEL M. CHITALILO (k.n.y MHE. DR. WILLIAM F. SHIJA)** aliuliza:-

Je, baada ya Shirika la Ugavi wa Umeme *(TANESCO)* kubinafsishwa, ni utaratibu gani utakaotumika katika kupeleka huduma za umeme Vijijini kama vile Vijiji vya Buyungu, Nyancheche, Ngoma A, Nyancheche Sekondari, Nyamililo, Kitunguru, Nyamatongo na Kamanga Wilayani Sengerema?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. William Shija, Mbunge wa Sengerema kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu la kusambaza umeme Vijijini ni jukumu la Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini ingawa utekelezaji wake bado unafanywa na Shirika la Umeme nchini yaani *TANESCO.* Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Sweden kupitia Shirika lake la Maendeleo la *SIDA,* inaandaa taratibu za kuanzisha Taasisi ya kuratibu miradi ya kupeleka na kusambaza nishati ya kisasa Vijijini *(Rural Energy Agency)* na Mfuko wa kugharamia mradi huo au miradi hiyo *(Rural Energy Fund).*

Utaratibu wa Taasisi na Mfuko ndio utakaokuwa unatumika kuratibu na kugharamia shughuli za kupeleka umeme Vijijini vikiwemo Vijiji ambavyo vimetajwa na Mheshimiwa Mbunge Dr. William Shija. Uanzishwaji wa Taasisi na Mfuko unategemewa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2004.

**MHE. SAMWEL M. CHITALILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba, je, Serikali kupitia Wizara yake ya Nishati na Madini, ni lini itahakikisha umeme unakwenda kwenye Majimbo yote ya uchaguzi kama vile Buchosa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwa kuwa umeme wa kutoka Sengerema Mjini unakomea Kijiji kinachoitwa Nyamazugo na hapo ndipo mpakani mwa Jimbo langu la Buchosa na Sengerema; je, ni lini sasa Serikali itahakikisha kwamba umeme huu unatoka hapo kupelekwa kwenye Vijiji vya Nyakasungwa, Nyehunge, Nyakalilo hadi Buhindi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tuna Wilaya 16 nchini ambazo hazijapata umeme katika Makao Makuu na katika hizo nne tayari zimo katika utaratibu wa kupatiwa umeme kwa maana ya kwamba fedha zimepatikana na Wakandarasi wako katika maeneo husika. Tumepeleka programu yetu ya kusambaza umeme kwenye maeneo yaliyobaki na bado tunaendelea kuwasiliana na wafadhili na tulikwishaahidi hata kwenye Kamati inayohusika ya Bunge kutoa taarifa mara tutakapokuwa tumekamilisha kufanya mawasiliano hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sengerema na kufikisha umeme kwenye eneo ambalo Mheshimiwa Mbunge amesema, kama nilivyojibu katika swali la msingi ni kwamba upelekaji umeme huu utakuwa ni wa uhakika zaidi hapo Mfuko maalum utakapokuwa umeanzishwa.

Kwa hivi sasa siwezi kuahidi ya kwamba umeme huo unaweza ukafikishwa katika hayo maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge amesema kwa sababu kwa Sengerema peke yake, kwenye maeneo ambayo Mheshimiwa Dr. William Shija ameyataja, yalikuwa yanahitaji siyo chini ya shilingi bilioni 2.4.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mahitaji ya umeme Vijijini yamekuwa ni makubwa na Serikali imekuwa ikitambua jambo hilo; na kwa kuwa katika miaka miwili iliyopita Serikali ilisema ya kwamba ilikuwa na mpango wa kukopa fedha katika Benki ya *ADB* ili kusaidia mpango mzima wa upelekaji wa umeme Vijijini; na katika jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri, suala hili halikujitokeza, je, mpango huu umefikia wapi mpaka sasa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miaka miwili iliyopita, Serikali imefanya kazi kubwa ya kusambaza umeme Vijijini pamoja na matatizo ambayo yamekuwa yakitajwa wakati hadi wakati ya upatikanaji wa fedha za kusambaza umeme kwa nchi nzima. Kazi ya kusambaza umeme ni gharama kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo ambalo limefaidika sana katika kipindi hicho cha miaka miwili, ni eneo la Mheshimiwa Benito Malangalila, ambalo limesambaziwa umeme katika maeneo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao mpango kama nilivyosema hapo awali wa kuhakikisha ya kwamba maeneo mengine nchini yanapatiwa umeme, si kwa *ADB* tu lakini tumepeleka pia maombi ya maeneo kwa wafadhili wengine. Kila wakati tunapokuwa tumepata majibu ambayo ni ya kuridhisha kwa maana ya kupata fedha, usambazaji wa umeme unaendelea kama ambavyo hivi sasa unaendelea katika Wilaya za Serengeti, Urambo, Ukerewe, Biharamulo na maeneo mengine.

Na. 70

**Ukosefu wa Mita za Umeme**

**MHE. HAROUB SAID MASOUD** aliuliza:-

Kwa kuwa hivi sasa wananchi wengi Mijini na Vijijini wameshafanya *fittings* kwenye nyumba zao ili waweze kuungiwa umeme na Shirika la Ugavi wa Umeme *(TANESCO)* lakini jambo ambalo limekuwa tatizo ni ukosefu wa *meter:-*

(a) Ikiwa jambo hilo lilitokea au linaendelea hadi hivi sasa, je, ni nini sababu yake?

(b) Je, kama ulikuwepo upungufu au upungufu huo unaendelea hadi hivi sasa ni nini mahitaji ya kila Mkoa wa Tanzania Bara?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mbunge wa Koani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kabisa kuwa kuna wananchi wengi Mijini na Vijijini wameshafanya *fitting* au wameshasambaza nyaya kwenye nyumba zao ili waweze kuingiziwa umeme. Katika kipindi cha hapo nyuma kabla ya mwezi Juni, 2002, kulikuwa na upungufu kubwa wa mita kutokana na sababu za kifedha ndani ya Shirika la Umeme yaani *TANESCO.*

Takwimu za Shirika hilo zinaonyesha kwamba hadi kufikia mwezi Machi, 2003 kulikuwa na wateja 5,420 waliokuwa wanasubiri kuvutiwa umeme yaani kujengewa *service line* na wateja 15,839 waliokuwa wameshawasilisha maombi ya kuwekewa

umeme lakini walikuwa bado hawajalipia, wengi wao ikiwa ni kwa sababu wako mbali sana na umeme ulipo na wachache kwa vile hawana fedha za kulipia. Kati ya hao 5,420 wapo wateja 2,250 ambao wanasubiri kufungiwa mita tu wakati wateja 3,170 waliobaki wanasubiri nyaya za umeme zijengwe au zivutwe hadi walipo ndio waweze kujengewa *service line.*

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na tatizo la mita, kati ya mwezi Mei hadi Septemba, 2002, Shirika lilinunua mita za kawaida zipatazo 30,000 pamoja na vifaa vingine vya kufungia mita hizo.

Vile vile Shirika liliendelea kukarabati mita zote za zamani ambazo bado ziko katika hali nzuri. Mita nyingi hivi sasa zinatumika kubadili mita zilizowekwa kwa wateja ambao ni mbovu au zimesimama kwa vile zimeshakaa muda mrefu. Kwa kawaida inabidi mita ikarabatiwe kila baada ya miaka kumi au kumi na tano kutegemea na aina ya mita.

Pia katika kipindi cha kuanzia Januari, 2003 hadi Juni, 2003 Shirika lilipokea jumla ya mita zifuatazo:-

(i) Mita 18,000 za njia moja yaani *single phase* za kawaida zinazotengenezwa na Kampuni ya *M/S Nansen* ya Brazil;

(ii) Mita 600 za njia tatu *three phase* za kawaida zinazotengenezwa na Kampuni ya *M/S Hexing Electrical* ya Uchina;

(iii) Mita za njia moja za *LUKU, (single phase)* 12,000 kutoka Kampuni ya *M/S Landis & Gyr* ya Afrika ya Kusini; na

(iv) Mita za njia tatu za *LUKU* yaani *three phase* 7,000 kutoka Kampuni ya *M/S Conlog* ya Afrika ya Kusini.

Vile vile Shirika limeshaandaa mahitaji ya mita kwa kipindi cha Julai, 2003 hadi Desemba, 2003 na hatua mbalimbali za manunuzi zinaendelea.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu za Shirika za mwezi Machi, 2003 zinaonyesha kuwa, iwapo Shirika litaweza kuvuta umeme pale ambapo hakuna umeme na *service line* zote kujengwa kwa wakati mmoja, mahitaji ya mita kwa kila Mkoa wa Tanzania kwa hivi sasa ni kama ambavyo nitampatia Mheshimiwa Mbunge kwa kuwa orodha ni ndefu na kwa kuzingatia utaratibu wa kujibu ni kwamba jumla ya mita kama 5,420 zitahitajika.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali yafuatayo ya nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri ametamka hapa kwamba mikakati na mahitaji ya mita kuanzia mwezi Julai mpaka Desemba, 2003

yametayarishwa, je, atakubaliana na mimi kwamba ni kweli suala hili ni la zamani kwa sababu sasa hivi tuko mwezi Novemba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kwamba wateja ambao wanasubiri mita ni 2,250 ambapo wateja hawa *automatically* wanalipa fedha kutoka Mfukoni mwao wenyewe ili kuzinunua mita hizo au kuweka *deposit* ya mita hizo, je, Mheshimiwa Naibu Waziri kwa nini Serikali haiweki *system* ya *revolving fund* kwamba wanapoleta mita 20,000 wanazozichukua wale wengine fedha zile ziweze kuletwa nyingine ambapo usumbufu huu utakuwa haupo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba mahitaji ya mita na vifaa vingine vya kufungia umeme vinaagizwa wakati hadi wakati na Shirika letu linafanya kazi kubwa sana ya kuhakikisha ya kwamba linatimiza wajibu wake. Tukumbuke ya kwamba hili Shirika linafanya biashara kwa hiyo, haliwezi kufanya makusudi lisiwe na vifaa isipokuwa tu pale ambapo uwezo wa kifedha wa Shirika hauendani na mahitaji ambayo yapo wakati fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuhusu suala la kuweka *fund* maalum kwa ajili ya kuagiza vifaa kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, nadhani napenda kurejea kama yale niliyoyasema awali kwamba Shirika lina mpango maalum wakati hadi wakati wa kuagiza vifaa kulingana na taratibu zake ndani ya Shirika na kama nilivyosema awali kwa kweli ni kutokana na mahitaji ya kibiashara na wao wanaagiza ila pale tu ambapo upungufu wa fedha unawazuia.

Na. 71

**Kurugenzi ya Ukaguzi wa Shule**

**MHE. JOHN E. SINGO** aliuliza:-

Kwa kuwa Kurugenzi ya Ukaguzi wa Shule katika Wizara ya Elimu na Utamaduni ni sehemu muhimu ya kutathmini mafanikio na mapungufu ya elimu nchini; na kwa kuwa kuiweka Kurugenzi hiyo chini ya Wizara ya Elimu na Utamaduni kunaifanya kuwa na nafasi finyu ya kutoa tathmini halisi inayojitegemea *(independent evaluation)* hasa kwa shule zinazoihusu Wizara:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha huduma ya kazi ya ukaguzi wa shule nchini?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuifanya Kurugenzi hiyo kuwa Taasisi inayojitegemea chini ya Ofisi ya Rais?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS - MHE. ARCADO D. NTAGAZWA (k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa John E. Singo, Mbunge wa Same Magharibi, naomba nitoe maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Ukaguzi wa Shule iliyoko chini ya Wizara yangu, ni idara muhimu inayohakiki na kutathmini ubora wa elimu nchini. Idara hii huipa Wizara marejesho yaani *feedback* ya ufundishaji na utekelezaji wa sera, Sheria na kanuni zilizopo kwa lengo la kuboresha elimu. Idara hukagua shule na vyuo vya ualimu ambavyo viko chini ya Idara nyingine (Idara ya Elimu ya Msingi, Idara ya Sekondari na Idara ya Ualimu) za Wizara pamoja na shule binafsi na shule za mashirika yasiyo ya Kiserikali.

Aidha, Wakaguzi wanatakiwa kufanya kazi bila woga na taarifa zao zisionyeshe upendeleo wowote. Taarifa zinazotolewa na Idara ya Ukaguzi wa shule, zinapaswa kuelezea kinagaubaga mafanikio na matatizo yanayojitokeza kwenye asasi zilizokaguliwa na kutoa ushauri kwa wanaomiliki shule kwa lengo la kuboresha elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa John Singo, Mbunge wa Same Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Serikali wa kuboresha huduma ya kazi ya ukaguzi wa shule ni kuajiri kila mwaka jumla ya wakaguzi wapya 127 waliopatiwa mafunzo ya awali ya ukaguzi mpaka tufikie lengo la kuwa na wakaguzi nane katika kila Wilaya na aidha kuendelea kununua magari mpaka kila Wilaya iwe na gari kwa ajili ya wakaguzi.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haina mpango wa kuifanya Idara ya Ukaguzi wa Shule kuwa wakala kwa sababu utaratibu wa sasa wa kuwa na Idara ya Ukaguzi yenye wakaguzi walioteuliwa na Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni baada ya mafunzo maalum bado unaonekana unafaa.

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa Hakimu hawezi kujihukumu; na kwa kuwa Kurugenzi ya Ukaguzi iko chini ya Wizara ya Elimu na Utamaduni; je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba ndio kimekuwa kikwazo cha Wakaguzi kushindwa kutoa taarifa sahihi za shule za umma ambazo zina mapungufu ya elimu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS - MHE. ARCADO D. NTAGAZWA (k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kukubaliana naye kwamba ni kweli Hakimu si rahisi kujihukumu, lakini hapa Wakaguzi wameajiriwa na wamekubali kufanya kazi ya kutumikia umma. Kwa hiyo, wanapotimiza wajibu wao hapa ni suala la kutimiza wajibu

wa kazi zao katika kulitumikia Taifa letu, si suala la kujihukumu kwa sababu tu wanakuwa chini ya Wizara ya Elimu na Utamaduni.

Na. 72

**Shule ya Sekondari Ngimu**

**MHE. JUMANNE H. NGULI (k.n.y MHE. LAZARO S. NYALANDU)** aliuliza:-

Kwa kuwa Tarafa ya Mgori katika Wilaya ya Singida Vijijini bado haina Shule ya Sekondari hata moja; na kwa kuwa juhudi za wananchi wakishirikiana na Mbunge wao wameweza kujenga Shule ya Sekondari ya Ngimu:-

(a) Je, Serikali itatuhakikishia kwamba shule hiyo itafunguliwa mwaka 2004?

(b) Je, Serikali itanihakikishia kwamba itafikisha umeme katika Sekondari hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS - MHE. ARCADO D. NTAGAZWA (k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu, Mbunge wa Singida Kaskazini, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imeweka utaratibu wa kutaka Mikoa iwasilishe Wizarani idadi ya sekondari zinazotarajiwa kufunguliwa mwaka mmoja kabla ya kufunguliwa ili gharama za uendeshaji wa shule hizo ikiwa ni pamoja na kuandaa walimu na zana za kufundishia na kujifunzia ziweze kuingizwa kwenye Bajeti.

Aidha, taarifa za ukaguzi wa shule hizo ziwasilishwe Wizarani kabla ya Septemba ya kila mwaka. Ili shule ya sekondari iweze kupata kibali cha kuanza, inahitajika kutimiza mambo yafuatayo:-

- Shule iwe na jengo la utawala, vyumba vya madarasa 8, nyumba za walimu 8, maabara 2, maktaba, stoo, samani za kutosha darasani na ofisini na vyoo vya kutosha.

- Majengo yote yawe ya kudumu na ujenzi wake ufuate ramani inayokubaliwa na Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mbunge wa Singida Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ukaguzi uliofanyika mwezi Septemba, 2003 katika shule ya sekondari tarajiwa ya Mgori, hali ya utekelezaji ilikuwa kama ifuatavyo:-

(i) Majengo: Jengo moja la utawala, madarasa 2, nyumba za walimu 2, hosteli moja ya wasichana na vyoo matundu matatu kwa wavulana, matatu kwa wasichana na mawili (2) kwa watumishi.

(ii) Samani: Madawati 100, viti vya wanafunzi 100, meza 25, viti vya Ofisi 20, kabati nne, kasiki au sefu moja, mabenchi matatu na sofa nusu seti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo sehemu iliyobaki itakuwa imekamilika ifikapo mwezi Desemba, 2003 upo uwezekano wa shule hiyo kuanza mwaka 2004.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza wananchi wa Tarafa ya Mgori pamoja na Mheshimiwa Mbunge kwa jitihada walizoonyesha za kujenga shule ya sekondari. Hata hivyo, jukumu la kufikisha umeme katika sekondari hiyo ni la wananchi wenyewe wakishirikiana na Halmashauri yao ya Wilaya na Shirika la *TANESCO. (Makofi)*

**MHE. JUMANNE H. NGULI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa shule hizi zinazojengwa na wananchi wakati mwingine hujikusuru mpaka wakafika mahala wakashindwa kuendelea; je, kwa hatua ya Shule ya Mgori ilivyofika, isingekuwa busara kwa Wizara kuiruhusu ianze ili sehemu nyingine inayobakia iweze kumalizwa kwa michango ya wanafunzi watakaokuwa wanaingia katika shule hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS - MHE. ARCADO D. NYAGAZWA (k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu ya msingi nimetaja kwamba kama juhudi za wananchi zitaendelea kukamilisha yale yaliyobakia kwa vyovyote shule ile itafunguliwa mwaka kesho.

Lakini vile vile tukubaliane kwamba wanafunzi waruhusiwe kwenda shule yaani shule ifunguliwe lakini madarasa hayatoshelezi, vyumba vya walimu na samani hazitoshelezi, sasa hata hiyo juhudi ya kusema tutumie michango ya wanafunzi watakaokuwa wameruhusiwa inaweza ikatupa mgogoro kwa sababu thamani ya fedha watakayokuwa wanatoa wanafunzi watakuwa hawaipati.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naona tumebikiwa na Wizara moja, maswali mawili yatapangiwa muda wake, swali la Mheshimiwa Mariam Mfaki na Mheshimiwa Jenista Mhagama.

Kuna matangazo, kwa kawaida tumezoea kuwaona vijana wa Shule za Msingi, leo vijana 70 pamoja na Walimu wao kutoka Sekondari ya Mazengo wametutembelea kuja kuangalia mijadala yetu. *(Makofi)*

Pia kuna vijana 20 na viongozi wao kutoka Mikoa mbalimbali ambao wameletwa na Shirika la Vijana linaloitwa *TAYOA.* Hawa watakaa na Bunge hili kwa muda wote, wanajifunza shughuli za Bunge. *(Makofi)*

Tangazo lingine, wale wanaotoka Mikoa inayolima Korosho, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Rita Mlaki, anawatangazia waonane naye chumba namba 432, ghorofa ya nne, saa tano kamili.

Waheshimiwa Wabunge, kuna haya makabrasha wanagawa, hii imeandikwa kwa Mheshimiwa Pius Msekwa, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano. Kuwasilisha makala mbili za taarifa ya sensa ya watu na makazi ya mwaka 2002. Pamoja na barua hii, napenda kupitia kwako kuwakabidhi Waheshimiwa Wabunge, makala mbili ambazo ndio hizo zimeandikwa kwa Kiingereza za Taarifa ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2002 ya kwanza ni *Methodology Report* ya pili ni *Age and Sex Distribution.* Lakini wanachosisitiza ni kwamba, wanaomba katika Kikao cha Kumi na Nne, mwezi Februari, 2004 watengewe angalau muda kuja kutoa ufafanuzi zaidi juu ya masuala mbalimbali yanayohusu hizo taarifa. Kwa hiyo, kila mmoja atapata zimewekwa kwenye bahasha yake.

Tangazo lingine ni kuhusu vikao, kikao cha Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kukutana, haiwezi kuwa saa tano kwa sababu mimi mwenyewe ni Mwenyekiti. Kwa hiyo, kitafanyika kesho saa tano pengine Naibu Spika atakuwa amesharudi.

Kikao kingine, ni kikao cha Wabunge wa Mikoa ya Ruvuma, Iringa, Mbeya na Rukwa saa tano, sasa nitabaki bila watu hapa, chumba Namba 231 jengo la utawala, imeandikwa na Dr. Chrisant Mzindakaya. *(Kicheko)*

Wajumbe wa Kamati ya Maliasili na Mazingira, nao wanaombwa kukutana saa tano.

Waheshimiwa Wabunge, naomba vikao hivi vifanyike muda mwingine kwa sababu Bunge litakuwa halina watu hapa na tunapitisha Muswada muhimu sana. Kwa kweli naomba sana vifanyike muda mwingine kuanzia saa saba au saa nane maana watu wote wanaondoka, tunapitisha Muswada muhimu sana wa Ushirika na Masoko, naomba sana pasiwe *empty,* naomba vifanyike wakati mwingine, mnaweza kutaja saa nyingine nikawatangazia hapa wakati tunaendelea na mambo haya labda cha dharura sana hicho naruhusu. Haya nayasema kwa mamlaka mliyonikabidhi ninyi wenyewe.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo!

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI:** Ngoja kwanza kabla ya mwongozo. Nadhani matangazo ya vikao yamekwisha, sasa mwongozo, Mheshimiwa Ponsiano Nyami.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na nia nzuri ya matangazo uliyotoa, kwa kuwa kikanuni baadhi ya matangazo uliyoyatangaza kufanya vikao kuanzia saa tano hayahusiani na shughuli za Bunge, je, mwongozo huo kutoka kwako umebadilisha Kanuni au inabakia vipi? *(Makofi)*

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI:** Haujabadilisha Kanuni yoyote ni kujenga tu *precedence* kwamba wakati fulani Spika akiona sasa watu wote hawapo, maana yake tumwambie Mheshimiwa Kahama, aje ahitimishe peke yake hapa kwa sababu asubuhi hii tukishajadiliana kuna kupitisha sheria hapa na haiwezi kupitishwa na watu wawili, ndio maana yake. Kwa hiyo, nafikiri tukubaliane tupitishe sheria hii halafu baadaye tuwe na mambo mengine. *(Makofi)*

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI:** Mwongozo umekwisha.

**MHE. HAROUB S. MASOUD:** Mheshimiwa ....

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI:** Sijakuruhusu Mheshimiwa Haroub.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Ahsante.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI:** Sasa nakuruhusu.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa maelezo ya Mheshimiwa Ponsiano Nyami, nilivyoelewa mimi na Waheshimiwa Wabunge wengine ni kwamba Kamati za Kudumu za Bunge ndio zina uwezo wa kukutana wakati ambapo Bunge linaendelea. Lakini kwa mujibu wa maelezo yako Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba radhi sana umesema “nawaombeni Waheshimiwa kusiwe kutupu” kwa kusema hivyo ina maana umewaruhusu.

Sasa alichouliza Mheshimiwa Nyami, je, Kanuni za Bunge zimetenguliwa leo kwa sababu kinachokubalika ni Kamati za Kudumu lakini wengine wote wanatakiwa wakutane baada ya kuahirishwa Bunge kama Chama cha Mapinduzi kimesema kitakutana lakini baada ya Bunge. *(Makofi)*

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI:** Mimi nafikiri maelezo yangu yameeleweka, nafikiri yameeleweka kabisa, ahsante sana, tunaendelea, Katibu!

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

**Muswada wa Sheria ya Vyama vya Ushirika wa Mwaka 2003**
***(The Cooperative Societies Bill, 2003)***

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kuunga mkono Muswada huu wa kuimarisha ushirika nchini. Kwa idhini yako, naomba kwanza hawa wanaotoweka watoweke kusudi nizungumzie suala kwa usalama zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia kujenga ushirika katika nchi yetu. Nchi hii kabla ya kupata Uhuru ilielewa umuhimu wa ushirika ikajenga ushirika ikawa ni nchi ya mfano katika Afrika lakini baadaye tuliyumba kwa sababu mbalimbali na leo inakuwa ni kazi ngumu kufufua ushirika katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusema kwamba kuimarisha ushirika katika Tanzania ni kuimarisha demokrasia kwa sababu watu maskini hawawezi kuifurahia demokrasia kwa sababu watanunuliwa, watakuwa wanyonge na pia watauza haki yao. Kwa hiyo, mkakati wowote wa kupambana na umaskini usioambatana na mikakati ya kuimarisha ushirika, mkakati huo hauwezi kufanikiwa. Mkakati wowote ule wa kujenga demokrasia katika nchi yetu usipoambatana na mkakati wa kujenga ushirika, demokrasia hiyo itakuwa ni ya watu wachache wenye mali, fedha na kazi ya mtu maskini itakuwa ni kupiga kura tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia hizi zikiimarishwa zitazua maana ya demokrasia kwa sababu hata kujenga Vyama Vingi vya Kisiasa hakutakuwa na maana. Maana lengo moja la kuwa na Vyama Vingi vya Siasa ni kuimarisha demokrasia lakini kama demokrasia itakuwa ni ya kununua yaani mpiga kura anauza kura yake kwa fedha ndio akupigie kura itakuwa haina maana. Naogopa kwa sababu mwelekeo huu sasa umeanza kuwa wazi mtu anaomba fedha ili akupigie kura. Sasa tukifika hapo, tumekwisha. Ninaogopa kwa sababu dalili hizi zipo.

Kwa hiyo, nasema mkakati wa kuimarisha ushirika ni mkakati wa kuimarisha demokrasia kwa maana ya kwamba unawapunguza hawa maskini na kujenga utu na heshima yao kama watu huru wanaoweza kutumia uhuru wao kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo na kwa mtazamo wangu hivi sisi kama Wabunge tunatunga hii sheria kwa ajili ya nani? Wabunge wangapi hapa ni wanaushirika? Wabunge wangapi hapa wana *SACCOS?*

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mawaziri, Madiwani wangapi hapa ni wanaushirika au wana *SACCOS?* Tusipofanya hivyo tutakuwa tunafanya *lip service* katika ushirika kwa sababu tunamwambia nani? Kama kila Diwani, Waziri, Mbunge, *Regional Commissioner, DC* angekuwa mwanaushirika ushirika ungekuwa hai. Tunahubiri ushirika lakini tunatepetea ubepari na hili ndio tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kwa macho yetu na akili yetu tukitazama tunapoelekea hivi kuna neema? Je, kuna siku *income per capita* ya Mtanzania itakuwa juu zaidi? Ni vizuri tukajibu swali hili kwa sababu *indicators* za madini za jana zinaonyesha kwamba baada ya muda madini yatakwisha, ardhi nzuri ya kilimo nayo hivyo hivyo kama ni biashara hali ndio hiyo. Tumekuwa ni dampo tu za nchi zilizoendelea. Wapi tuelekeze nguvu zetu? Kwenye madini, utalii, kilimo au viwanda?

Mimi nadhani ni kwenye kilimo. Kwa bahati mbaya kilimo cha Tanzania kilivyo labda uwe mwendawazi ndio utakwenda ku-*invest* huko kwa sababu mazingira yote yako kinyume kabisa. Mtu unasubiri miezi tisa ndio ukauze mazao yako na bila uhakika. Ndiyo maana sasa Taifa hili limekuwa ni Taifa la wachuuzi tu, wakala tu yaani kila nyumba ni duka, kila mtu ni mfanyabiashara, kila mahali ni kijiwe. Sasa limeanza kuwa Taifa la kuunda watu wa vijiweni, wafanyabiashara na wengine wa kukaa tu. Wanashangaa kwa nini hawaendelei. Huwezi kuendelea bila kutii misingi na miiko ya maendeleo yaani kufanya kazi. Sasa sisi tunataka tuendelee kwa miujiza tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kwamba Wakuu wa Mikoa, Mawaziri, Madiwani na Wabunge wawe ni kichocheo cha Ushirika. Vinginevyo tunadanganyana tu. Kama ushirika ni sera ya Chama Tawala (CCM) na ndicho kinachotawala, Mtendaji hana uhuru wa kuchagua kutekeleza sera hii mpaka Chama kingine kije kitawale. Leo tunasema kuingia ushirika ni hiari sawa lakini ukishaundwa kazi ya Mtendaji ni ku-*facilitate* utekelezaji wa sera ya Chama hicho Tawala. Leo tunasema kwamba Mkuu wa Mkoa awe *neutral,* ahubiri ubepari kwa maana binafsi na ushirika. Ni wazi kuwa atapendelea kule ambako ni rahisi kwa sababu mtu binafsi anakujia kwa urahisi anakuambia mzee, mzee kunywa moja sasa huyu mwanaushirika atafanyaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajenga ushirika wenye miguu, mimi hapa ni mwana *SACCOS* ya Makambako. Ushirika huu wa sasa ni mgumu. Kwa hiyo, hoja hapa ni namna ya kujenga ushirika katika mazingira ya utandawazi na soko huria sio ushirika wa kulindwa, sio ushirika ule wa zamani. Sasa nani atakuwa *champion* wa ushirika huu mpya katika mazingira haya mapya? Namfahamu Mheshimiwa George Kahama na Naibu Waziri wake, ni wanaushirika wa siku nyingi nao watahitaji kuwa *transformed* ili wa-*fit* katika mazingira haya mapya ya mashindano ya utandawazi ambapo bila kufanya hivyo hauwezi ukaishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye maduka yetu utaona bidhaa zote ni za kutoka nje, maziwa yanatoka Zimbwabwe, nyama inatoka Botswana, pilipili inatoka Nigeria, matunda yanatoka *South Africa* na Waswahili ndio wanauza mazao hayo mitaani. Nashukuru na naipongeza Serikali kwa kuamua kufuta baadhi ya mitumba hata nguo za ndani zilikuwa zinauzwa tu mitaani. Watanzania wanasubiri watu wafe ndio wanunue nguo zao za kuvaa ndani?

Nashukuru Serikali imechukua baadhi ya hatua hizo lakini katika shughuli za kilimo tusipokuwa na mkakati wa kufufua kilimo, hatuwezi tuka-*survive.* Tusizungumzie ushirika wa kuuza mitumba au ushirika wa kuwa wakala wa hizi bidhaa za mitumba

katika nchi yetu. Naupongeza Muswada huu kwa sababu unazungumzia kuimarisha Ushirika katika ngazi za chini.

Kule Hungary hakuna *Unions* kuna Vyama vya Msingi vya Ushirika, wanapotaka kuzungumzia mambo yao ya pamoja basi wanamchagua Mwenyekiti wa muda na ndio ushirika ninaozungumzia hapa. Ushirika ulioua ushirika nchini ni ushirika wa juu unaounda Meneja wa Ushirika ngazi ya juu ambaye anapiga tai, kila siku ofisini ameweka viyoyozi, amenunua magari. Huu wote ni ulaji tu hawa wa ngazi za chini, wanavaa kandambili ndio wanahangaika kulima pamba lakini huyu anakula tu. Sasa nasema nashukuru Wizara imeona umuhimu wa kujenga ushirika kwa maana ya kujenga ushirika wenye miguu, *base* na wenye *grass root.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo, natumaini hatutengenezi mvinyo mpya kwa kuweka kwenye chupa za zamani *(new wines in old bottles)* tunatengeneza *new wine in new bottles* (mvinyo mpya katika chupa mpya). Kwa maana hiyo, itabidi hata sisi wenyewe tubadilishe mtazamo wetu, Mameneja wa ushirika wajue ni biashara, wajue wanaishi katika mazingira magumu ya mashindano. Nani wana-*sabotage* ushirika katika dunia hii?

Amerika imestawi kwa sababu ya ushirika, *Nordic countries* zimestawi kwa sababu ya ushirika, ushirika ni dhana ya lazima sio ujamaa tu hata mabepari lazima waishi kwenye makundi ya watu utanyonya wapi kama uko peke yako, nenda porini kanyonye, huwezi. Maendeleo ni matokeo ya watu kufanya kazi kwa pamoja kwa faida ya pamoja. Ni lazima kushirikiana kwa sababu vipaji vinatofautiana, *resources* haziko kila mahali kwa hiyo kwa kushirikiana ndio unaweza kugawana vile vichache mlivyonavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ubepari ndio jibu la matatizo yetu ya kiuchumi? Hata ubepari una *limitations* zake maana *resources* ni *limited.* Huwezi kuendelea tu hivi hivi hata kama dhana kwamba ubepari unachochea mtu binafsi kutumia vizuri uwezo wake alionao lakini nao una mwisho.

Kwa hiyo, mimi natazama ubepari kama ni *temporary phase* lakini ujamaa *in my view* ndio jibu. Bila kushirikiana *we are doomed to failure.* Hawa maskini hawawezi kuendelea kututazama tu. *We are digging our own graves.* Tunachimbia makaburi yetu wenyewe. Maadamu wanyonge na maskini wanazidi kuongezeka na hawa wanyonyaji wanazidi kunyonya zaidi lakini wachache jeshi la maskini wanaonyonywa siku moja litatuasi.

Kwa hiyo, tukitaka amani na maendeleo ushirika ndio njia na ubepari ni *temporary phase.* Ni mfumo wa mpito. Kama *resources* ni chache ni lazima tuweke mikakati ya namna ya kugawana kile kidogo kilichoko vinginevyo hawa hawawezi kukubali kufa kwa urahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Lenin mkongwe wa ujamaa aliwahi kusema: *"Workers of the world unite, you have nothing to loose except your chains."* Hii ndiyo lugha ya

wakulima wadogo wadogo *they have nothing to loose* isipokuwa unyonge na umaskini. Lenin alikosea, hakutizama vizuri, alidhani wafanyakazi wa nchi zilizoendelea na wa nchi maskini wangeungana. Mabepari walipogundua *threat* au tishio hilo waliwaangamiza wafanyakazi wa nchi zilizoendelea katika kundi la wanyonyaji. Ndio maana huko Ulaya mwisho wa mwezi hata usiye na kazi unaweza kwenda kupokea chochote kwenye dirisha lakini hawa wa kwetu wameachwa bila kitu. Wafanyakazi wa Ulaya ni sehemu ya wanyonyaji wa wafanyakazi wa nchi maskini.

Naomba nimalizie mchango wangu kwa kusema kwamba Taifa lolote linalopuuzia ushirika Taifa hilo linajikana lenyewe, *that Nation can't exis. That Nation is denying, its own existence. The future of this country lies* katika ushirika *and sharing of resources.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Muswada ulio mbele yetu. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na timu nzima ya Wizara kwa kuleta Muswada huu mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikiri na niungane na wenzangu kusema kwamba ushirika ndio mkombozi wa wananchi maskini. Kama tunalenga kupiga vita umaskini na tunataka kuondoa umaskini katika nchi yetu kazi moja kubwa ambayo tunatakiwa kuifanya ni kuhimiza, kukuza na kulea ushirika kwa kila njia inavyowezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda kuzungumzia mafungu yenyewe na napenda kuanzia Kifungu cha 24(1) pale ambapo wanaushirika tarajiwa wanapeleka maombi ya kutaka kuandikishwa. Ninaogopa kwa sababu kipengele tulichokiweka ni kigumu na hakisaidii kusukuma jitihada tunazotaka kuzifanya za kuhimiza wananchi kujiundia ushirika wao. Kifungu cha 24(1b) kinataka wananchi kule vijijini watengeneze na wapeleke kwa Waziri: *"A report of a feasibility study or project write-up."*

Kwa uzoefu wangu hiyo ni ngumu sana kwa kikundi chochote cha wananchi kule kijijini kuandika *write-up* wala *feasibility study.* Hiki kitu hawajui na hawana wataalam kwa kweli hiki kitakuwa *counter productive* kama tutaendelea kukisisitiza hapa labda kuwe na kipengele kingine cha kumtaka Afisa Ushirika wa Wilaya kwa lazima akisaidie kikundi chochote kinachotaka kuandikisha ushirika kuandaa kipengele hiki vinginevyo Mrajisi atakuwa hajafanya kitu cha maana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni dhana iliyopo katika kipengele hicho, Kifungu cha 24(1c) kinataka: *"Such other information as regard to the society as the Registrar may require."* Nafikiri kufuatana na Kifungu cha 5, tunachotaka ni *Registrar* au huyu Mrajisi kwa kutumia Wasaidizi wake Mkoani na Wilayani wasaidie kuhimiza uandikishwaji wa ushirika lakini wasifanye kuwa ngumu. Dhana iliyopo hapa ni kwamba

yeye anataka masharti yake yatekelezwe sasa hii ni kutengeneza *bureaucracy* (umangimeza) ambao sio wa lazima na hautatusaidia katika lengo la kujenga upya ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda kwenye Kifungu cha 25(4), kipengele kikubwa ambacho kitamfanya Mrajisi akubali ni kuangalia *volume of business* yaani shughuli zitakuwa nyingi kiasi gani. Kwa hiyo, ameangalia faida kuliko kuangalia manufaa mengine ya ushirika. Manufaa ya ushirika vijijini sio tu kwamba biashara yao itakwenda sawa au vipi lakini pia ni kwamba wajenge uwezo wa pamoja wa kuweza kuhimili mashindano yanayotokana na biashara huria. Ukiangalia kipengele cha faida tu ambacho ndicho kitamfanya Mrajisi awasajili nafikiri pia tutakuwa hatujafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaangalia watu wangu kule Mangola wanaozalisha vitunguu kama watabaki wakiangaliwa faida itakayopatikana itakuwa kiasi gani wale wa Kenya wanaokuja huko wameshaingia kwa wingi wananunua vitunguu na kawaida vitunguu vinaweza kupanda mpaka shilingi 30,000/= kwa gunia lakini inafika mahali wale wa nje wanavishusha mpaka shilingi 2,500/= mpaka vitunguu vinakosa nguvu. Ninachoangalia pale ni ushirika ule uweze kuwasaidia kurudisha bei katika bei ambayo inaweza kuwa ya manufaa. Kwa hiyo, kipengele kikubwa ni ile *bargaining power* ambayo ndio lengo la ushirika duniani kote tusiangalie tu kipengele cha faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele cha 48(4) kinanistua kidogo kinataka mahesabu ya Vyama vya Ushirika yakaguliwe. Naomba hili nilisema kutokana na uzoefu wa huko nyuma, tulikotoka Vyama vyetu vingi vya Msingi vimekufa kwa sababu ya mlolongo mzima wa mawasiliano kati ya Vyama vyenyewe na Mrajisi. Kumekuwa na *control* kubwa sana katika Ofisi ya Mrajisi na hata ikitokea tatizo kwa mfano mtu ameiba ilikuwa haiwezekani hata kumpeleka Mahakamani bila kupata kibali cha Mrajisi. Lakini Mrajisi yuko mbali sana na wao wengi hata hawajui watampataje hata anuani yake hawajui, neno lenyewe Mrajisi linaonekana kama ni dudu fulani lenye Miguu mingi, kule vijijini ukisema Mrajisi watu hawajui ni kitu gani.

Sasa kifungu cha 48 kilivyokaa na kusema: *"The accounts of every registered society shall be audited at least once in a year"* sina tatizo, *"by the corporation or such competent and registered Auditor appointed by the General Meeting,"* sina tatizo lakini unaposema: *"and approved by the Registrar."* Mpaka kupata hiyo *approval* ya yule *Auditor* sielewi kwa nini iende mpaka kwa *Registrar*. Nafikiri hapa tunatengeneza mlolongo ambao hauna ulazima. Kama *General Meeting* ime-*approve* nafikiri *Registrar* apate taarifa lakini isiwe tena suala la *approval* unapongojea *approval* maana yake unaendelea kuchelewesha na matokeo mahesabu hayaendelei kukaguliwa. Nafikiri hilo ni *counter productive* na tunachokitaka sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kipengele cha 48(6) anazungumzia suala la miezi sita ya *appeal* kama makosa yamegundulika katika mahesabu na hiki ndicho kilichotusababishia Vyama vyetu vifilisike. Kwa sababu kama kumetokea tatizo una *appeal* kule kwa Mrajisi, sasa hivi nashukuru kwamba kule chini wao wanaweza kuchukua hatua za msingi lakini kama kosa limetokea umetoa ni miezi sita, miezi sita

kule vijijini *by the time* unapata taarifa, *by the time* wanagundua mahali pa kumpelekea Mrajisi miezi sita imekwisha.

Napenda hapa wapate muda kwa sababu hapa una-*deal* na fedha za watu na ambao wako vijijini, watu ambao *communication* ni tatizo, watu ambao wakati mwingine Posta iko Makao Makuu ya Wilaya tu lakini kijiji kiko kilomita 70 au 80 nje ya Makao Makuu ya Wilaya.

Nafikiri muda huu ungeongezwa badala ya miezi sita wapewe muda angalau mwaka mzima ili makosa yoyote yanayotokea kwenye mahesabu yao, wasipoteze haki yao kwa sababu tu wamepewa muda wa miezi sita na wajanja watatumia kipengele hiki cha miezi sita watachelewesha kuipeleka huko kwa Mrajisi halafu watasema kwamba inaanza kuhesabika sijui kutoka lini *by the time* wanapeleka sasa na wao muda umepata, kwa hiyo, haki itakuwa imepungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele cha 51, huwa nina matatizo makubwa unapopata hivi vipengele vinavyozungumzia: *"Shall submit an annual return to the Registrar."* Sina tatizo la msingi, sina tatizo na *principle* ya taarifa kila mwaka zipelekwe kwa Msajili. Lakini lazima tujue tuna *Administrator General of Trustees* anataka hizi taarifa zipelekwe kila mwaka, kuna *Registrar of Societies* anapelekewa hizi taarifa kila mwaka lakini hakuna hata mmoja anayezifanyia kazi sasa tunazipeleka iwe nini?

Kwa hiyo, sipingi kipengele kuwepo lakini ninataka iwe *in records* kwamba yule Mrajisi akipelekewa taarifa kwanza ajenge uwezo wake wa kuzifanyia *analysis* kama Mrajisi hatakuwa anafanya *analysis* makosa yametokea na hakuna hatua inayochukuliwa basi hiki kipengele cha sheria tunacho kitakaa kwenye makabati hakitakuwa kinafanya kazi na hakitawasaidia wananchi wetu.

Kwa hiyo, napenda sana Mrajisi apate taarifa hizi lakini Mrajisi azifanyie kazi na awe na uwezo wa kuzi-*analyze* na awarudishie wananchi. Pia *mechanism* ya kupeleka taarifa iwe *designed* sio kuwapelekea wale wale ambao wanaonekana wamehujumu. Hiyo mara nyingi inaonekana kwamba taarifa zinakwenda kwa wale wale viongozi, taarifa zile zitafichwa hazipelekwi kwenye bodi au Kamati zinazohusika matokeo yake tunaingia kwenye ubadhirifu mkubwa sana wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina *comment* ndogo tu kwenye kipengele cha 67 sijaona kwenye *schedule of amendments,* Waziri atanisaidia labda imenipita pale unasema: *"Notwithstanding the provisions of section 67."* Sasa 67 ndio hiyo inaongelewa, kwa kuangalia nafikiri inazungumzia kipengele cha 66. Kwa hiyo, kama kimekosewa naomba kiangaliwe nafikiri kuna tatizo la *editing* au wakati wa uchapaji *flow* haikuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele cha 71 kinanipa tatizo kubwa zaidi tunazungumzia biashara ya ushirika katika ulimwengu wa soko huria, tunazungumzia *competition* ambayo ni pana na kwamba ushirika sasa nao utashindana na hawa wafanyabiashara binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unaposema: *"A registered society shall not make a loan to any person other than a member,"* sielewi kinazungumzia nini.

*Provided that subject to the provisions of its by-laws a registered society may with the approval of the Registrar and in accordance with any conditions which the Registrar may prescribe, allow normal business".* Sasa hata biashara tukitaka zidhibitiwe na Mrajisi mwenyewe, mimi nafikiri tutaingia mahali hivi Vyama havitafanya kazi. Biashara ya sasa inataka tangu unapopata taarifa, *wihin 24 hours* uwe ume-*decide* ili uweze kushindana na wenzako. *By the time* unashindana na Mrajisi, upeleke taarifa, *competition* imeshakushinda, imekutoa nje, *cooperative* itakuwa imekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri *internal mechanism* zitumike kwanza na Mrajisi atumike tu pale ambapo kuna malalamiko na aingie kama chombo cha *appeal* lakini isiwe hatua ya kwanza kwa kila *decision* kubwa ya kibiashara, tunamtaka Mrajisi ndiye awe chombo cha kutoa maamuzi. Mimi sina tatizo na udhibiti na nafikiri Waziri anajua, sasa hivi mimi mwenyewe nina tatizo, lakini ningependa Mrajisi asiwe wa kwanza awe katika hatua za *appeal* na katika hatua za *appeal* pia na yeye awe na *timeframe within which* anaweza kufanya kazi, siku sitini zinazotolewa saa nyingine ni nyingi na inakuwa ni vigumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, wanasema tena: *"Except with the permission of the Registrar".* Sasa kila kitu kimekwenda *except with the permission of the Registrar a society shall not lend money on the security of any movable property".* Hiyo inahusiana na kile ambacho tumekuleteeni lakini ninachosema ni kwamba, *in terminal mechanism* kwanza ziwe *designed* na labda *regulations* zi-*state* kabisa hizo *internal mechanism* ni zipi na taratibu za kuzitumia ni zipi, zikimalizika ndiyo tuondoke sasa twende kwa *Registrar.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele cha 73, mimi nakiona pia ni *dangerous* kwa sababu kinazungumzia *a registered society may invest its funds.* Sasa sisi ni Chama. Tuna fedha zetu za kutosha, tunataka kuziweka kwenye *investment,* tunatakiwa mpaka tupate *approval* ya *Registrar* lakini hizi fedha ni za kwetu na sisi tuna *Board* iliyo *competent*, tuna watu ambao wana uelewa, tuna wataalam tumewaajiri, bado tunatakiwa kwenda kwa *Registrar*. Mimi nilifikiri *Registrar* daima aingie katika hatua za mwisho, lakini pale ambapo sisi tunaweza kusukuma vitu vyetu atupe madaraka, *regulations* zieleze kabisa taratibu za kufuatwa, yeye aje tu katika kutusaidia ku-*control* na kudhibiti pale ambapo sisi tunakiuka utaratibu wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifikiri vile vile kwamba, katika kipengele cha 82, kuna tatizo pale, nikilinganisha na kipengele kile cha 82(c) anasema: *"To a fine not exceeding one thousand shilling".* Siamini kama wanataka kuzungumzia *one thousand shillings*, sikuiona kwenye *schedule of amendments,* inawezekana ile *schedule* iliyokuwa *technical* sikuiona lakini nadhani kama ilivyo kwenye 89(2), ambapo anazungumzia *not*

*exceeding one hundred thousand shillings* hata pale pia wanazungumzia kitu cha namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijagongewa kengele, nina kitu cha mwisho ambacho nilifikiri ni muhimu nikiseme. Ni kipengele cha mwisho kabisa cha 133(4). Mimi nisingependa kuona Waziri apewe mamlaka ambayo matokeo yake ni kwenda kutunga sheria nyingine bila kupitia Bungeni. Sina tatizo na Waziri kutunga kitu kinachoitwa *consequential* au *traditional,* lakini anapofika mahali anatunga *supplementary provision,* hii ni sawa na kutunga sheria nyingine. Sasa Waziri asipewe mamlaka, anatunga *supplementary provision* hazijapita Bungeni, kwa kweli ni Bunge kukwepa madaraka yake na kumpa Waziri madaraka ambayo mwisho wa yote ni kama ilivyotokea hapa Bungeni, tutaambiwa Wabunge mliruhusu na mkaachia kipengele hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nimalizie kwa kusema kwamba, kipengele kile cha 17 nafikiri kimekaa vibaya, kama kimerekebishwa sikukiona, kinazungumza, *the following reasons on ground shall not be considered when appointing an Executive Staff* halafu *condition* yenyewe *illegal means to induce a decision for the appointment.* Kinaelekea kwamba, ndiyo kimeruhusu hicho, sasa kama kimerekebishwa mahali, basi naomba radhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwa dhati kabisa, kutambua kazi nzuri ambayo imefanywa na Serikali kupitia kwa Waziri wa Ushirika na Masoko na msaidizi wake. Kwa kweli *competence* yao ni kubwa, namfahamu ndugu yangu Mheshimiwa Chibulunje, tumekulia kwenye ushirika na ninaamini anamsaidia sana Waziri. Sasa kwa sababu wengi wamechangia katika vifungu mbalimbali ambavyo na mimi nilitaka kuchangia, lakini kwa sababu kanuni zetu haziruhusu kurudia rudia, nitajielekeza zaidi katika maeneo ambayo hayajachangiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kifungu namba 130 ambacho kinampa mamlaka Waziri kutengeneza *rules*. Sasa tatizo langu ni dogo sana. Tatizo lipo katika kifungu kidogo cha tatu kwamba, Waziri atatunga *rules* (sheria ndogo ndogo) na kwamba,Waziri anaweza kuelekeza ziandikwe kwa Kiingereza au Kiswahili. Kule mwisho katika kifungu hicho cha tatu kinasema, kama kutakuwa na mgogoro, tafsiri sahihi itakayochukuliwa ni ile ya Kiingereza. Mimi nasema hapa tumekwenda mbali, namwomba Waziri kama halikufanywia *amendment* lifanyiwe hivyo maana mimi nafikiri lugha kuu ya nchi hii ni Kiswahili, hakuna sababu kabisa tafsiri ya Kiingereza ichukuliwe ndiyo tafsiri halisi katika lugha ambayo siyo lugha yetu ya Taifa na tukijua kabisa kwamba, wanachama wetu wengi kwa kweli Kiingereza hawakijui, sasa unapomwambia tafsiri ya Kiingereza ndiyo sahihi, unamfikisha mahali pabaya. Naomba kifungu hicho kiangaliwe vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kingine ambacho naomba kiangaliwe pia, ambacho mzungumzaji aliyemaliza sasa hivi kuchangia alikizungumzia lakini hakijaelezwa kwa ukamilifu, hiki ni kifungu cha 66(3), pale ambapo Msajili anapochunguza na kupendekeza Kamati ivunjwe *(suspension of a committee),* yeye inapofika kwenye *Special Annual General Meeting* na kama wanachama hawakubaliani na maamuzi ya Msajili, wana uwezo wa kukataa lakini walipe *liabilities*. Sasa sijui unaposema walipe *liabilities* kwanza itatekelezwaje, mtafilisi mali zao? Hakuna kifungu kinachoeleza utekelezaji wake, hiki kitakuja kuwekwa katika *regulations*, maana uzoefu umeonyesha kwamba, wakati mwingine Wajumbe wa Kamati wanakwenda kuwarubuni wanachama na inafika mahali wanakubaliana kwamba, Kamati ina haki ya kuendelea. Sasa inapofikia hapo na wanaruhusiwa waendelee walipe madeni, sasa watayalipaje, kwa kufilisiwa au kwa utaratibu gani wa sheria? Hilo nataka lipewe ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo limezungumzwa pia ni suala la ukaguzi. Suala la ukaguzi limetamkwa vizuri katika kifungu cha 48, pengine tu ninalolizungumzia hapa ni uzoefu. Vyama vingi havikaguliwi kwa sababu havina uwezo wa kulipa ada za ukaguzi. Je, Serikali inalionaje hili? Saa nyingine ni kikwazo, Shirika linashindwa kuvikagua Vyama hivi kwa sababu havijalipa madeni ya ukaguzi uliopita. Inapofikia hali hii wanachama wabaki tu na wadanganywe tu? Ni vizuri tungetafuta *provision* ambayo ikifika mahali, msajili awe na uwezo kutoka fungu la Ushirika kuagiza ukaguzi ufanywe ili tujue maovu yaliyoko kule ndani. Hilo ni pendekezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho katika kuchangia ni kama ilivyosemwa, nafikiri ni kifungu cha 90, *inspection of affairs*. Hii ni kama *Management Audit,* nafikiri hili lisiwekwe kwamba, Msajili *may* kwa kweli ni vizuri kila mwaka au kila baada ya miaka miwili kuwe na *Management Audit* ya Vyama hivi, maana wengine wanaweza kujificha, wanachama hawana uwezo wa kuwatambua na kwa sababu hakuna *Management Audit,* wanabaki kulalamika tu kwa kujificha kwa sababu wanaogopa viongozi wao. Mimi nafikiri nimeliona kwenye *amendment* lakini nilitaka nilisisitize kwamba, *Management Audit* ni kitu muhimu sana kisisitizwe katika sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuchangia *point* kwa *point* hasa kutegemea sheria ilivyo, labda nije sasa katika mambo ya ujumla, nizungumzie suala la utandawazi na ushirika. Ni kweli kwamba, kama hatutachukua hatua dhahiri ya kulinda Vyama vya Ushirika katika utandawazi, tunajidanganya hata kama tungetunga sheria nzuri namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii haitamki mahali popote kwa dhati kuvilinda Vyama vya Ushirika na suala la kulinda Vyama vya Ushirika ni la Serikali. Vyama vingi leo havina uwezo na ushirika unakufa kwa sababu Vyama vyenyewe vinaongozwa na maskini, matokeo yake hakuna mtu anayevisimamia Vyama hivi. Sasa tukiachia tu tutazungumzia suala la ushirika katika maneno, lakini si katika matendo. Mimi kwa bahati nzuri ni mmoja wa wafanyakazi wa mwanzo mwanzo wa Vyama vya Akiba na Mikopo na wakati tunaanza tulifika mahali ambapo Serikali yenyewe ilitusaidia hata kutufungulia ofisi. Mimi nilikuwa mwakilishi Kanda ya Ziwa, nilifanya kazi nzuri Mkoa wa Kagera, Kigoma na Mwanza na ni kweli Serikali ilikuwa inatoa msaada mkubwa sana

hata ofisi zangu zilikuwa kwenye ofisi ya Serikali wakati mimi nilikuwa nafanyia kazi *SCULT* (Muungano wa Vyama vya Akiba na Mikopo).

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila misaada hii, nina uhakika kipindi hiki cha utandawazi ni kibaya zaidi na ndiyo wakati ambapo Serikali sasa inapaswa kusimama kidete kusaidia Vyama vya Ushirika, vinginevyo litakuwa ni jambo la kihistoria tu na ushirika utashindwa na utandawazi. Sioni mahali popote ambapo mtu binafsi ataingia katika Kijiji akataka kununua mazao ashindane na ushirika, ni mahali ambapo pengine hata kama elimu imepita kwa nguvu nyingi sana, lakini pia watu wao wawe na uwezo. Watu wetu wanarubuniwa na vitu vidogo, mtoto hajakwenda shule, ana kahawa yake, asubiri Chama cha Ushirika kikakope fedha, mtu anakuja na hela, atauza kahawa yake hata kwa shilingi mbili ampeleke mtoto wake shule. Sasa kama Serikali haikusaidia na kuhakikisha kwamba, kuna fedha za kutosha kwa wakati, Vyama vya Ushirika vinapata msaada, uwezo wa Vyama vya Ushirika kuendelea hapa nchini kwa kweli itakuwa ni historia tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ambalo ningependekeza ni Vyama vya Akiba na Mikopo ambavyo sasa hivi vimeanza kuonyesha uwezo mkubwa sana. Hivi Vyama vingeanza kuwa chimbuko la kuanzisha Benki ya Ushirika, wanazo fedha nyingi, ni kweli ni ushirika wao, lakini mimi nafikiri wakipewa miongozo, wanaweza kabisa kuwa ni Vyama vya mwanzo vya msingi vya kuanzisha Benki ya Ushirika na bila Benki ya Ushirika sisi tunajidanganya. Maana bila mahali ambapo Vyama vitakwenda kusema na kuweza kupewa msaada kwa wakati, kweli ushirika huu tumeutungia sheria, lakini hii sheria ni karatasi tu, ni lazima tuweke *infrastructure* ambayo italea ushirika. Bila kuwa na *infrastructure* ya kulea ushirika ni kama nchi isiyo na barabara, reli, utaiita nchi, lakini uchumi hauwezi kufunguka bila kuwa na barabara. Sasa barabara ya ushirika ni fedha, hawa ni maskini walioamua kuunganisha nguvu zao kwa lengo la kufuta umaskini. Sasa kama wewe utawaachia tu bila kuwapa nguvu kama Serikali na hawana mahali pa kwenda kukopa ni ukweli kwamba, hawatakuwa na mtaji wa kuondoa umaskini wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, suala la kuanzisha Benki ya Ushirika hilo lipewe *priority* katika kuukomboa ushirika na Benki hiyo ifanye kazi kwa uhuru wa kibenki. Lakini ilelewe na itafutiwe misaada, hizi *grants* zinazozunguka zunguka tu zipelekwe huko. Wasimamiwe vizuri kwa sheria hii katika ukaguzi wa kila mara, nina uhakika ushirika utakua. *KNCU* au *BCU* zilifika mahali zikaunda Benki na zilikuwa na nguvu kwa sababu vilikuwa ni Vyama vilivyo na uwezo wa kifedha. Bila uwezo wa kifedha haiwezekani hata siku moja ushirika ukadumu. Kwa hiyo, nashauri hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningelizungumzia kwa ujumla, ni uhuru wa Vyama vya Ushirika. Ni kweli tumetamka kwamba, Vyama vipewe uhuru, lakini Chama cha Ushirika ni kama mtoto ukimpa uhuru uliozidi kiasi hatakuwa na uwezo wa kuendelea vizuri, lakini na wewe ukimbana sana utakuwa baba ambaye kwa kweli unaleta matatizo katika kumlea mtoto. Lakini moja ambalo ningependa sana katika suala hili la uhuru wa Vyama hasa katika Vyama vya Mazao ni Vyama kuruhusiwa kuuza bidhaa zao kokote wanakotaka. Kupewa nguvu za uwezo wa kusaidiwa ili wauze bidhaa zao au mazao yao mahali ambapo bei ni nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili linatokea zaidi katika Mikoa ya mipakani, mtu amelima mahindi yake kwa sababu bei ni nzuri huko Zambia wewe unamwambia asiuze ni kosa. Kitu kikubwa ni kumwambia nitanunua kwa bei ya Zambia, kwa hiyo, usipeleke Zambia. Hapo utakuwa umemtendea haki, lakini ukimkataza asiuze kahawa yake Uganda wakati anapata bei nzuri huko, hii kwa kweli ni dhuluma. Nunua hiyo kahawa kwa bei wanayonunua Uganda, usikataze utakuwa umemtendea haki na yeye atakuwa ni mtu mjinga sana na ana sababu zake kama ataamua bei ya shilingi pengine elfu moja anaweza kuipata Bukoba aamue kupeleka akauze mpakani, basi huyo ana tatizo na ambalo si la kawaida kama bei hiyo hiyo anaweza kuipata Bukoba, anasafirisha kahawa aende kuuza mpakani Mutukula, atakuwa ni mtu wa ajabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosisitiza Vyama vya Ushirika vipewe haki ya kuuza mazao yake na tuwe na vyombo vya kusaidia ku- *rebuff prices*. Tatizo ni kwamba, hatuna *Price Stabilization Fund* katika nchi hii. Kwa hiyo, bei zinaposhuka tunamwachia mwananchi anaumizwa, lakini kwa kweli tungekuwa na mfumo kwamba bei zinaposhuka tunaongeza bei zifikie viwango ambavyo vitamvutia mnunuzi au mwanaushirika, mimi nina uhakika tutaweza kuwa-*control* watu wetu kwa haki na Vyama vya Ushirika vita-*flourish* na nina uhakika kwamba maendeleo yatapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia hayo, naomba nimshukuru tena Waziri kwa kazi nzuri na naamini kama mtu aliyekulia katika ushirika na msaidizi wake ambaye naye amekuwa mlezi wa ushirika, naamini sheria hii itamsaidia katika kuusaidia ushirika, lakini nasisitiza ushirika lazima upewe msaada wa Serikali wa kifedha ili uweze kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuongea machache kuhusu Muswada huu ambao ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wenzangu waliopita walivyoongea, umuhimu wa sheria hii kwa Taifa letu unajulikana sana. Kwa kipindi kirefu watu Vijijini wamekuwa wakinung'unika kwa jinsi ushirika ulivyozorota na kuwasababisha wapate hasara sana. Naongelea haya hasa ninapofikiria Jimbo langu huko Musoma, wao kila wakati ninapokwenda wanazungumza juu ya *Mara Cooperative* ilifilisika wakaenda na fedha zao. Popote unapokwenda kama ni Mbunge swali la kwanza unaulizwa tutalipwa lini fedha zetu baada ya *Mara Cooperative* kufilisika. Sasa kwa sababu hiyo ningependa kuuchambua Muswada huu kipengele hadi kipengele kuona ni mambo gani yanaweza kuleta utashi, ni mambo gani tunaweza kuyarekebisha yakawa angalau yana unafuu kwa wale wadau hasa huko Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, sina matatizo na jinsi hii *society* inavyoundwa, uandikishaji nadhani umewekwa bayana. Tatizo linajitokeza uendeshaji wa hizi *cooperatives* hasa kuweka ankara zao. Ushirika lazima utengeneze faida,

ushirika lazima ufanye biashara nzuri kwa *members* wao ili angalau wafaidike, kama ushirika unaleta hasara kwa watu haufai kuitwa ushirika, siyo mategemeo yao ni lazima watu wafaidike na unono wa faida wanayoipata kutoka kwa kazi zao wanazozifanya. Sasa ukiangalia kipengele cha uwekaji wa ankara tuseme Januari moja, ndiyo ushirika umeandikishwa, wamefanya biashara kwa miezi kumi na mbili, sasa sheria hii inasema lazima wafanye ankara kila mwaka.

Sasa unajiuliza kwa kipindi cha miaka mingapi, kipindi cha miezi kumi na mbili hiyo au mtawapa ingawa miezi mitano baada ya kutimiza mwaka mzima, maana kama ni *annual account* lazima zifanyike kuanzia Januari mpaka Desemba *then* hawa *auditors* lazima wazifanyie kazi hizo hesabu walinganishe kama zinasema ukweli na inawezekana kama wakiwa *fast enough,* wanaweza kufanya kwa kipindi cha miezi mitatu. Haiwezekani kabisa hawa watu wafanye hesabu ifikapo Desemba na hesabu ziwe zimekamilika, hii haiwezekani. Ni lazima wapewe kipindi cha miezi kadhaa baada ya kumalizika kwa mwaka. Ningeshauri Serikali wachunguze tena upya hiyo *requirement* ya kufanya *audit* za *accounts* kwa kipindi cha miezi kumi na mbili.

Upande mwingine inakuwa ni wale viongozi wa ushirika, kama kuna viongozi lazima wafanye *returns* zao. Lakini *returns* wanazopeleka kwa Msajili ziwe ni *returns* za shughuli walizozifanya kwa kipindi cha miezi kumi na miwili. Kwa mfano, kama wamepitisha hesabu zao zile ankara itakuwa ni kiambatisho cha ile *return* unayoipeleka kwa msajili ndiyo inaweza ku-*make sense*, vinginevyo hizo *annual accounts* hazina maana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalopenda kulizungumzia ni kuhusu kufilisika kwa hii *cooperative.* Nchi hii ina sheria tatu za ufilisi, ya kwanza inamhusu mtu binafsi, kama akifilisika lazima sheria ya *Bankrupt Ordinance* i-*apply* na sheria zake zinafanana sana sana na zile sheria zinazohusu kampuni ikifilisika. Muswada huu unajaribu kufanya ubaguzi ambao nadhani siyo vizuri, ukifanya Mfilisi chini ya *Cooperative* kuwa na madaraka tofauti na yale yanayomfilisi mtu binafsi, mimi nadhani siyo uwiano mzuri. Ni lazima sheria ya ufilisi ifanane. Kwa mfano, sheria ya ufilisi wa kampuni ni *Companies Ordinance,* ambayo tunaitumia leo *Cap. 212* na ile tuliyopitisha mwaka jana zinaeleza Mfilisi atakuwa na madaraka gani sasa ukilinganisha na Mfilisi wa *Cooperatives* unakuta huyu amebanwa sana hana madaraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa niseme kwamba, tuchukue madaraka ya Mfilisi wa Kampuni *Cap. 212* yafanane kabisa kabisa na yale ya Mfilisi chini ya *Cooperatives.* Hii itatupa angalau *certainty* huyu Mfilisi ana madaraka gani na huyu Mfilisi anafanya kazi gani, Mfilisi ni Mfilisi, ushirika umekufa lazima apate nguvu za kuweza kufanya hiyo kazi ya ufilisi bila kubabaika. Sasa ukiangalia ibara ya 102 inambana sana, inampa nguvu kwa maeneo kama sita hivi ukilinganisha na Mfilisi chini ya Sura 212. Mfilisi huyo ana mambo mengi anayoweza kuyafanya kwa mfano, anaweza kufungua kesi au kutetea kesi yoyote kwa jina na kwa niaba ya kampuni huku kuna tofauti kidogo. Anaweza kuendelea na biashara ya kampuni hiyo mpaka hapo atakapoona haiwezekani, kwa mfano, kwa kipindi cha miezi pengine mitatu kama majaribio, kweli *society* imefilisika ama tunaweza kuifanya nini, anaweza kuikarabati

ikaendelea. Hii sheria inasema una-*cancel* hapo hapo unamweka mfilisi, nadhani kuna upungufu sana, ningeshauri kipengele hiki kirudiwe tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chini ya Sheria ya Makampuni, inamruhusu Mfilisi kuteua Wakili kumsaidia, inamruhusu kuwalipa wadai wa daraja lolote lile la deni. Kwa mfano, ushirika unaweza kuwa umepata fedha kutoka Benki, inaweza kuwa ni Benki ya kawaida ama Benki ya Ushirika. Benki ina masharti yake, sasa hapo umembana hawezi kwenda kukopa na akikopa pia masharti ya benki yatakuwa magumu kwa kuwa benki haitakuwa na sababu za kutoa mkopo iwapo sheria yenyewe siyo *clear*. Ningeshauri kabisa hii sura ama ibara inayojadili kazi ya ufilisi iende sambamba na wakati, tusifanye kuwa walegevu na kupoteza lengo la ushirika, lazima wakope na lazima warudishe fedha, wakifilisika lazima kuwe na mfilisi ambaye anajulikana Kitaifa na pia Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande mwingine tunakuja ni kwa zile karatasi ambazo lazima zisajiliwe kwa msajili, kama amekopa lazima afanye *return* ya kuonyesha amekopa kiasi gani, kuna *debentures,* kama amefanya *debenture* lazima afanye *debenture* ambayo ni hati ya kuonyesha kwamba amekopa na anapolipa lazima asajili hiyo hati kwamba ameshalipa kwa msajili. Tatizo ninalolipata hapa ni kwamba, *control* ya mfilisi ipo kwa msajili pekee, *control* ya mfilisi chini ya Sheria ya Makampuni tuliyoitunga, ipo chini ya Mahakama.

Kuna maana yake kabisa, kama ipo chini ya Mahakama basi huyu mfilisi anatakiwa apeleke hati ama apate kibali kutoka Mahakamani, inaweza kuwa Mahakama ya Wilaya inamruhusu afanye mambo fulani. Lakini hapa tumembana tunasema hapana Mahakama ikifanya yeye msajili anaweza kubadilisha maamuzi ya Mahakama, nadhani siyo vizuri, Mahakama ni chombo kingine tofauti na msajili, msajili hawezi kuwa na madaraka makubwa kuliko Mahakama, haiwezekani, nadhani kuna matatizo hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya msajili iwe ni tofauti na ile kazi ya Mahakama lazima tutenganishe. Nadhani tukiboresha maeneo haya matatu makubwa, huu Muswada unaweza kuwa wa maana zaidi, ukatulinda na ukasaidia wananchi wengi ambao wanataka kuwa na hizi *cooperatives.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Wajumbe ambao wamesema sheria hii iandikwe kwa Kiswahili, mimi niko tofauti kidogo. Bunge tunatunga Miswada yote kwa Kiingereza, Mahakama inapotoa hukumu, hukumu zile zinakwenda kwenye *record* na huwa zipo kwa Kiingereza, ndiyo utaratibu wetu, kuna *certainty* lazima sheria iandikwe kwa Kiingereza maana Sheria ya Makampuni imeandikwa kwa Kiingereza.

Sasa anasema Sheria ya *Cooperatives* iandikwe kwa Kiswahili ili wananchi wengi waweze kuisoma, siamini kama hiyo ndiyo maana ama utaratibu tuliojiwekea. Sheria zote ziwe za Kiingereza, unaweza kutoa tafsiri, lakini tafsiri imara iwe ile ile ya Kiingereza kwa sababu ya utandawazi. Watu wa Kenya wanaweza kuja kufanya biashara hapa na watu wa Zaire wanaweza kuja kufanya biashara hapa, lakini ukianza kusema lugha iwe ya Kiswahili nadhani unaanza kubana zaidi na Ushirika unakuwa hauna maana. Kwa hiyo, ningependelea kwamba, lugha ya Kiingereza ibaki hivyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa machache hayo niliyosema, naunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika Muswada huu mzuri ulioweza kuwasilishwa na Mheshimiwa Waziri wetu wa Ushirika na Masoko. Kwa kweli mimi nianze kwa kusema kwamba, naunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia moja kwa sababu ni mzuri kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza yeye Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji wengine wote walioweza kushiriki katika maandalizi ya Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona niseme hivyo, kwa maana tu ya kwamba, Muswada huu umejadiliwa na watu wengi zaidi hasa katika kipindi hiki. Tumeanza mapema kabisa na Mheshimiwa Waziri katika Kamati ya Kumshauri Rais, tukapata mawazo mbalimbali ambayo nina imani kabisa Mheshimiwa Waziri, ameyaweka katika Muswada huu na ndiyo maana Muswada unaonekana hauna upinzani mwingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimeshuhudia hii ni safari tuseme ya nne ya mimi kushiriki katika Muswada kama huu baada ya kushiriki nikiwa kama mdau. Kulikuwa na Mkutano mkubwa sana na niliweza kuhudhuria Arusha kwenye Mkutano wa wadau mpaka tulifikia hatua ya kupiga kura ili nani aonekane ameshinda. Lakini kwa busara za Mheshimiwa Waziri na Watendaji wake, wameyarekebisha na kila mmoja anajisikia kwamba ameshirikishwa ipasavyo na hana kigugumizi katika sheria hii. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nakupongeza sana kwa jinsi ulivyouleta Muswada huu ukiwa na picha kama hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana tu ya Ushirika, Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia na wanajua kabisa kwamba, bila Ushirika kwa kweli kuumaliza umaskini itakuwa si kazi rahisi. Sifa za Ushirika ziliishia katika miaka ya 1976, baada ya vurugu za kuvunjwa kwa Vyama vya Ushirika bila utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuseme ulikuwa kama uvamizi, mtu unakutwa uko ofisini, unaambiwa tupishe anaingia mtu mwingine anaanza kuongoza mpaka kuja kufikia kwenye mwaka 1984 ndiyo anarudisha bila *interest* yoyote ile. Ni tatizo kubwa hilo na ndilo lililowafanya wanaushirika wayumbe mpaka leo hii, jinsi wanavyoyumba inatokana na utaratibu uliovurugwa mwaka 1976, wangekuwa mbali sana. Lakini baadaye wakawa wamerudi katika utaratibu huo. Sheria iliyorudishwa ya mwaka 1984 ilikuwa bado ina mapungufu na sheria ya mwaka 1991 ilikuwa vilevile na mapungufu ya kiasi fulani. Lakini katika sheria hii, kwa jinsi tulivyowashirikisha wadau, nina imani Ushirika sasa utafufuka kwa kasi kubwa zaidi, hasa tukianzia kwenye Vyama vya Msingi. Vyama vya Msingi ndiyo *source* ya Ushirika wenyewe, tuwape nafasi ya kutosha wanaushirika wenyewe kujiamulia mambo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti,Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba, wapewe kila linalowezekana wanaushirika hawa waweze kufanya kazi yao. Mheshimiwa Waziri, umerekebisha yaliyo mengi na niseme kwa niaba ya wadau ambao tuliweza kuhudhuria kwenye Kamati ya Bunge ya Mheshimiwa William Shellukindo, wanasema kwamba, Kamati hiyo wanaipongeza kwa jinsi ilivyoweza kuwapokea na kuwasikiliza kwa heshima ya hali ya juu. Ni picha ambayo kwa kweli hawakutegemea kwamba wangetendewa mema kama jinsi ambavyo walitendewa siku ile, walitoa michango yao kwa uhuru na baadaye ilipokelewa na ikawa imefanyiwa kazi. Nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge wote mliohusika na zoezi hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nizungumzie machache kwa vile mengi nilishayazungumza katika vikao mbalimbali. Ili tuweze kufanikisha sheria hii basi, Wizara inayohusika na ajira za watumishi iajiri Maafisa Ushirika hasa katika ngazi za Wilaya ili waweze kusimamia sheria hii kikamilifu, bila watumishi ni sawa na kazi bure. Kwa sababu sheria hii inabidi ifuatiliwe na watendaji wa Serikali. Sasa hivi Wilaya zilizo nyingi utakuta kuna Afisa Ushirika mmoja. Mfano, Mkoa wa Mwanza sasa hivi, hatuna Afisa Ushirika wa Mkoa ili kusajili hata kama ni *SACCOS* inabidi uende Mkoa wa Mara au uende Mkoa wa Shinyanga, ni mwaka mzima sasa hatujapata Afisa Ushirika wa Mkoa. Kwa hiyo, tunahitaji basi nguvu za ziada ziwekwe kwenye Wizara ya Ushirika na Masoko, waweze kuajiri watumishi ili waweze kufanya kazi zao vizuri na sheria hii iweze kutekelezeka. Hilo ni jambo la msingi ambalo naona kwamba, ili sheria yetu isiwe na ugumu wa kuitekeleza, basi Maafisa wa Ushirika waajiriwe kwa wingi kama jinsi ambavyo tumekuwa tukiuliza maswali mengi hapa Bungeni tukiahidiwa kwamba, wataajiriwa watumishi katika Wizara hii mpya ambayo inaendelea vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeeleza kwamba, sheria hii imejadiliwa na watu wengi na walikuwa wanaisubiri kwa hamu sana na nina imani baada ya Bunge hili itakuwa imepitishwa na baadaye Mheshimiwa Rais, atapata nafasi ya kuiwekea saini. Tunaiomba Wizara ya Ushirika na Masoko, sheria hii isibaki kwenye *shelves,* ipelekwe mpaka kwa wahusika. Wapelekewe wadau wenyewe waione na nikubaliane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu ambao walisema kwamba ni vyema basi ikapata tafsiri ya Kiswahili ili angalau washirika kule waweze kuipata kwa njia hiyo ili iwe rahisi wao kuelewa kwamba tufanye nini? Kwa hiyo, lengo si kwamba labda yenyewe iandaliwe kwa lugha ya Kiswahili, ni vema tu iendelee kwa Kiingereza lakini ipate tafsiri ya Kiswahili kama alivyofanya Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, kwenye ardhi sasa hivi watu wanaona haki yao vizuri na wanaweza kuitekeleza kwa njia nzuri tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nirudie tena kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko na Watendaji wote, kwa jinsi walivyoweza kutuandalia Muswada huu tuliokuwa tunausubiri kwa hamu na kwa muda mrefu na sasa umekamilika. Sasa nimwombe Mheshimiwa Waziri, kwa sababu yeye ni mzoefu wa Ushirika, basi aisimamie sheria hii tuweze kufufua Ushirika wetu ambao ni mkombozi wa wanyonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, narudia tena kusema kwamba, naunga mkono Muswada huu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii nami niweze kuchangia hoja hii ya Muswada wa Sheria ya Vyama vya Ushirika ya Mwaka 2003.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda nitamke kwamba, naunga mkono hoja na ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote, tuunge mkono Muswada huu upitishwe iwe Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kuchangia kwa kumsaidia Mheshimiwa Waziri kupitia na kujibu baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kusema humu Bungeni na wale waliochangia kwa maandishi, ambao wote watatambuliwa rasmi na Mheshimiwa Waziri mtoa hoja, atakapokuwa anahitimisha hoja yake hapo baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umevutia wachangiaji wengi ambao wote kwa ujumla wao, wamesaidia sana kuuboresha Muswada huu, pamoja na kuisaidia Wizara na Serikali kwa ujumla, ili iweze kusimamia vyema utekelezaji wa sheria mpya na maendeleo ya Ushirika hapa nchini kwa ujumla. Nawashukuru sana kwa michango yao. Baada ya utangulizi huo, sasa naomba nijielekeze kwenye baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko hoja ambayo ilijitokeza kuhusiana na suala la uchaguzi na muda wa uongozi katika Vyama vya Ushirika. Suala hili lilichangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi kiasi wakiwemo Mheshimiwa Edson Halinga, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Isaac Cheyo, Mheshimiwa Dr. James Msekela, Mheshimiwa Leonard Derefa na asubuhi hii Mheshimiwa Jackson Makwetta, naye vilevile amezungumzia suala la uchaguzi ndani ya Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria tunayoipendekeza sasa hivi juu ya utaratibu wa uchaguzi imejitahidi sana kuangalia suala zima la demokrasia kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wengi walivyosema. Pamoja na suala la kuendeleza uzoefu yaani ile *continuity* ya uongozi ndani ya Vyama vya Ushirika. Katika mapendekezo ya hivi sasa, katika kifungu cha 63 inatamkwa wazi kwamba, kipindi cha uongozi au uchaguzi utakuwa unafanyika kila baada ya miaka mitatu, tofauti na sasa ambavyo uchaguzi unafanyika kila mwaka ambayo kusema kweli ni gharama kubwa. Kwa hiyo, katika kukwepa suala hili la gharama za uchaguzi kwa kila mwaka, sheria ya sasa inapendekeza kwamba, uchaguzi ufanyike kila baada ya miaka mitatu.

Lakini vilevile katika kuchagua kila baada ya kipindi cha miaka mitatu, pendekezo linasema wakati huo wa uchaguzi theluthi moja ya Wajumbe itajiuzulu na inajiuzulu kabisa kabisa tofauti na sasa ambapo sheria ilikuwa inasema kwamba, theluthi moja inaweza ikajiuzulu, lakini vilevile wanaweza wakapata fursa ya kuchaguliwa tena. Lakini sheria sasa hivi inasema kwamba, wajiuzulu watoke moja kwa moja ili watoe nafasi kwa wengine waliochaguliwa waingie. Lakini kwa sababu zile theluthi nyingine mbili zitakuwa zinaendelea kubaki pale, basi suala la uzoefu na

*continuity* litakuwa linaendelea pale. Kwa hiyo, hili limezingatiwa. Lakini hata hivyo, ni kwamba, hii haiwazuii moja kwa moja hawa ambao wameondoka katika ile theluthi yao ya kujiuzulu. Baada ya kipindi kingine cha miaka mitatu wanakuwa na nafasi ya kuweza kugombea na kuweza kuchaguliwa tena endapo wanachama watapenda wanaweza wakawarudisha. Kwa hiyo, hapa demokrasia bado imezingatiwa kwa ukamilifu kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hapa niseme tu kwamba, uchaguzi wote utasimamiwa kwa mujibu wa taratibu na kanuni ambazo zitatungwa hapo baadaye na zitazingatia zaidi masharti na kanuni zitakazokuwa zimewekwa kwa mujibu wa Kanuni za Maadili ya Uongozi ambazo zimependekezwa chini ya sheria, yaani ile *code of conduct.* Kwa hiyo, suala la upigaji kura kwa mfano, kura kwa njia ya siri na masuala ya wagombea kujieleza mbele ya Wajumbe, haya yote yamezingatiwa. Kama huko nyuma utaratibu wa uchaguzi ulikuwa unafuata mtindo wa kiholela tu, kusema huyo huyo apite na kadhalika, hayo yalikuwa ni makosa, kusema kweli yalikuwa siyo makusudio. Lakini sasa hivi kwa sababu tutakuwa na hizi *code of conduct,* pamoja na kanuni na taratibu zitakazotungwa tutahakikisha kwamba, zinasimamiwa kwa ukamilifu ili uchaguzi ufanyike kwa utaratibu wa heshima na wa kuzingatia taratibu na sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya pili, ambayo iliongelewa vilevile na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, ilikuwa inahusu madaraka ya Mrajisi kuwa makubwa hasa kwenye masuala makubwa mawili, ambayo nadhani waliyagusia. Moja, lilikuwa katika suala la kuunganisha Vyama kwamba, kwa nini Mrajisi awe na mamlaka ya kulazimisha Vyama viunganishwe wakati kuna uhuru wa wanachama kujiunga?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia na madhumuni kusema kweli ni kuvisaidia Vyama vyenyewe. Vyama hivi ambavyo vinatakiwa viunganishwe si kwa kutaka tu Mrajisi mwenyewe aseme kwamba, basi viunganisheni, kuna vipengele kadhaa na vigezo vya kuzingatia. Kubwa zaidi ni ule uwezo wa kiuchumi kwa hiyo, inapofika mahali ambapo Vyama vya Ushirika vilikuwa vimeshaandikishwa vikaendesha shughuli zake bila ufanisi, vikaonekana sasa vimekuwa dhaifu kiuchumi, hapo ndipo Mrajisi anawajibika sasa kuvisaidia ili viweze kupata nguvu ya kiuchumi kwa kuvitaka kuungana kwa pamoja.

Kwa hiyo, kama vitakataa maana yake ni kwamba, vitakuwa sasa vinafanya kazi kwa misingi tofauti na mtazamo na mwelekeo mzima wa kuviendesha Vyama vya Ushirika kwa misingi ya kiuchumi, hapo ndiyo inafikia Mrajisi anasema kwamba, basi vinginevyo hamtaendelea kwa utaratibu huu ambapo mko dhaifu. Kwa hiyo, hapa siyo kulazimisha tu kwa Mrajisi kwa kutaka. Kwa hiyo, inapokuwa imetokea kwamba, Vyama hivi vimekuwa dhaifu na kwa kweli nia ni kuvisaidia. Lakini vilevile suala hili liliongelewa kwa sura nyingine na Waheshimiwa Wabunge waliozungumzia suala hili alikuwa ni Mheshimiwa Paschal Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, Mheshimiwa Aggrey Mwanri na Mheshimiwa Isaac Cheyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuteua Mjumbe katika Kamati za Halmashauri, kuna mahali ambapo Waheshimiwa Wabunge wamesema kwamba, inakuwaje huyo Mjumbe awe na kauli ya juu zaidi ama ya mwisho kushinda maamuzi ya Wajumbe wengine wa Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kusema kweli suala hili linajitokeza pale tu ambapo kwenye Chama cha Ushirika kuna maslahi ya Serikali kwa maana kwamba, labda kuna fedha za Serikali zimewekezwa pale au maslahi ya namna nyingine yoyote ambayo Serikali inayo ndani ya Chama hicho cha Ushirika na huu ni utaratibu wa kawaida tu hata katika vyombo vingine, ambapo pengine chombo kitakuwa kimekopeshwa, basi ili mkopo ule uweze kusimamiwa vizuri, chombo kile kilichokopesha kinateua mtu wake anakuwepo pale. Sasa mnapojadili masuala yanayohusiana na usimamizi au *management* ya zile fedha au maslahi ya Serikali , hapo ndipo inajitokeza kwamba, huyu mwakilishi wa Mrajisi lazima awe na sauti au kauli ya juu na kwa vyovyote vile basi Mrajisi lazima apate maamuzi ya juu kutokana na kulinda *interest* ama maslahi ya Serikali, ambayo yako kwenye Chama hicho cha Ushirika. Kwa hiyo, si kila wakati lazima kuwe na Mjumbe pale, Mjumbe huyo atakuwepo tu kama kuna dhamana ya Serikali imewekezwa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya tatu ama inayofuata kwenye mtiririko wangu hapa inahusiana na rushwa ndani ya Vyama vya Ushirika na hili limeongelewa na Waheshimiwa Wabunge wengi kwa namna mbalimbali akiwemo Mheshimiwa Edson Halinga alizungumzia kwa nguvu sana suala la rushwa, Mheshimiwa Lekule Laizer na hivi asubuhi hapa Mheshimiwa Jackson Makwetta, naye kwa namna fulani, ameligusia suala la rushwa hasa kwenye uchaguzi na mahali pengine hata katika uendeshaji wa Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu niliseme hili kwa kifupi sana kwamba, rushwa ni tatizo linaloonekana katika sekta zote za Umma zikiwemo pamoja na Taasisi za Ushirika. Napenda niwashukuru baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wengine, ambao kwa kweli wametusaidia sana kutoa mwanga mzuri katika hili. Wakati mwingine kuna mazoea ya kunyooshea vidole Vyama vya Ushirika kwamba, Vyama vya Ushirika wezi, kuna rushwa na kadhalika, lakini baadhi ya wazungumzaji hapa kusema kweli wametoa maelezo mazuri kwa kusema kwamba, haya masuala ya rushwa, ubadhirifu wa fedha za Taasisi, yapo kila mahali kwenye Mashirika ya Umma na kwenye Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunachotaka kusema ni kwamba, pamoja na mkakati wa Kitaifa wa kupambana na rushwa, pamoja na ubadhirifu mwingine, Muswada huu umeainisha jinsi ya kukabiliana na mianya ya rushwa kwa kipitia vipengele vya kanuni za maadili, yaani *code of conduct,* vifungu vya *surcharge* na kuwepo kwa Maafisa maalum wa kuendesha kesi, navyo vilevile vimewekwa kwa makusudi ya kuhakikisha kwamba, suala hili linajaribu kuziba mianya mbalimbali iwe ya rushwa ama ubadhirifu wa namna mbalimbali. Hilo tunadhani kwamba, tunaweza tukalikabili kwa namna hiyo, lakini ni lazima kukitilia maanani kwamba, suala hili ni la Taifa nzima kwa ujumla na linahusu Taasisi nyingi za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya nne, inazungumzia habari ya Vyama Vikuu vya Ushirika vya mazao vihimizwe kufanya miradi mingine zaidi ya ukusanyaji wa mazao. Hili lilizungumziwa sana na Mheshimiwa Leonard Derefa, Mbunge wa Shinyanga Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, jambo ambalo nataka kulizungumzia ni kwamba, Vyama vya Ushirika, viwe Vyama Vikuu, viwe Vyama vya Msingi au Vyama vingine vya aina yoyote, vinapojiunga pamoja huwa na makusudio fulani. Kwa hiyo, vinakuwa na ile *co-function* ya kutekeleza madhumuni ya wanachama waliosababisha vyama hivyo kujiunga. Kwa hiyo, tunadhani jukumu la msingi ambalo Vyama vya Ushirika vinawajibika kutekeleza ni lile ambalo lilisababisha Vyama hivi vikaundwa. Kama ni Chama cha Mazao basi kinaundwa kwa makusudio pengine ya kuwatafutia masoko wakulima, pembejeo za kilimo na kuendeleza kilimo kwa ujumla na biashara. Kwa hiyo, hii ndiyo shughuli ya msingi na kwa hiyo, tunadhani kwamba, itakuwa ni vizuri na nitoe tu wito kwa Vyama vyote vya Ushirika vitakavyoanzishwa, kusema kweli vizingatie shughuli ya msingi kwanza hiyo ndiyo itekelezwe. Hizo shughuli zingine kwa bahati mbaya zinapokuwa zinaanzishwa bila utaratibu, ndiyo zinakuja kudhoofisha hata zile shughuli za msingi, kwa hiyo, wanachama wanakuwa hawanufaiki na mategemeo waliokuwa nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano tu kwamba, baadhi ya Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo, vinaweza vikawa vimeanzishwa kwa ajili ya kukusanya akiba na hivyo vikatoa mikopo kwa wanachama wake. Lakini bahati mbaya unakuta kwamba, vinaanzisha shughuli nyingine za kuanzisha *Guest House* na kununua mabasi. Kwa hiyo, utakuta kwamba, Vyama hivi vinakosa fedha za kuweza kukopesha wanachama wake kutokana na hii miradi mingine mingine ambayo imeanzishwa. Kwa hiyo, uzoefu wetu umeonyesha kwamba, hata katika Vyama Vikuu vilivyokuwa vimeanzishwa huko nyuma, kwa kuanzisha miradi hii mingi sana imedhoofisha shughuli za msingi na kuendeshwa kwa utaratibu ambao haufai na mahali pengine kwa sababu ya uzoefu na *management* zao zilikuwa hazina uzoefu juu ya shughuli hizo walizozianzisha, kwa hiyo, shughuli hizo zilishindwa kuendelea. Kwa hiyo, tunashauri kwamba, kwa kuanzia, wanaushirika waendeshe shughuli zao kwa kuzingatia zile shughuli za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja inayofuata ni uhaba wa Maafisa wa Ushirika katika Halmashauri za Wilaya, Miji, pamoja na Manispaa. Hoja ambayo imezungumziwa na Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Mgana Msindai na asubuhi hii Mheshimiwa Jacob Shibiliti, ameizungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekwishabainisha mahitaji ya kuajiri Maafisa wa Ushirika wapatao 300 kwa wakati ule, lakini kuajiri hawa watumishi kwa awamu na katika mwaka wa 2002/2003, Idara ya *Management* ya Utumishi wa Umma, ilitoa kibali cha kuajiri Maafisa wa Ushirika 44. Baadhi ya Halmashauri zimeanza kujaza nafasi hizo zilizokuwa wazi na Wizara itaendelea kushirikiana na Halmashauri katika kukamilisha zoezi la kujaza nafasi za watumishi zinazohitajika kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa. Aidha, *Cooperative Reform Programme* itaanzisha utaratibu wa kuimarisha Mfumo wa Idara ya Ushirika, pamoja na mahitaji halisi ya Maafisa Ushirika

katika ngazi zote. Nadhani hii *Cooperative Reform Programme* itatusaidia sana hata kuweka Muundo wa Idara ambao utakuwa *more effective* katika kusimamia Vyama vya Ushirika hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja inayofuata ilikuwa inahusu tofauti ya idadi ya wanachama wanaotakiwa kuanzisha aina mbalimbali za Vyama vya Ushirika. Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja hii alikuwa ni Mheshimiwa Paschal Degera na Mheshimiwa Isaac Cheyo. Lakini vilevile ilijitokeza na hoja nyingine inayofanana na hii ambayo ilitolewa na Mheshimiwa George Lubeleje, juu ya utaratibu wa uanzishaji wa Vyama Vikuu vya Ushirika kwenye maeneo ambayo bado hayana Vyama Vikuu ukiwemo na Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kueleza hapa ni kwamba, idadi ya wanachama waanzilishi wa aina mbalimbali za Vyama inawekwa kwa kuzingatia mahitaji ya kuwa naVyama vyenye uhai wa kiuchumi. Kusema kweli hii ndiyo sababu ya msingi kwamba, jinsi mnavyokuwa wengi ndivyo mnavyoongeza uwezo wenu wa kiuchumi. Hii inatokana na utafiti, uzoefu na hata maoni ya wadau waliyotoa katika vikao mbalimbali kama alivyosema Mheshimiwa Jacob Shibiliti hapa, waliunga mkono kuhusu hili kwamba ili muweze kuunda nguvu ya pamoja, lazima muwe na idadi kubwa ya kutosha ya wanachama katika Vyama vya aina mbalimbali. Lakini hii pia inaepusha ile hatari ya kuwa na vikundi vidogo vidogo vya wanachama wachache unaweza ukaishia kuwa na Chama cha Ushirika cha familia moja tu au cha ukoo. Kwa hiyo, idadi hii kubwa inaepusha mambo kama hayo na vilevile inaongeza hilo suala la kuwa na idadi ya watu wengi wa kutosha kukidhi suala la *economic liability.*

Kuhusu hoja ya Serikali kusaidia uundaji wa Vyama Vikuu vya Ushirika, kwenye maeneo ambayo hayana Vyama Vikuu vya Ushirika hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa George Lubeleje. Nataka niseme tu kwamba, Mkoa wa Dodoma, pamoja na Mikoa mingine katika suala zima la uanzishwaji wa Vyama. Kama tulivyokuwa tumesema kwamba, wataingizwa katika hii *Cooperative Reform Programme,* ambayo itawezesha wanachama wahamasishwe kuweza kuanzisha Vyama wanavyovihitaji. Kuanzia Vyama vya Msingi, Vyama Vikuu na kuendelea. Kwa hiyo, aina na mahali vitakapokuwa vinahitajika Vyama, utakuwa ni uamuzi wa wanachama wenyewe. Lakini hapa msingi mkubwa au msisitizo mkubwa utakuwa Vyama vya Ushirika vya Msingi na Chama Kikuu cha Shirikisho kile cha *Federation*. Hapa katikati kama aina nyingine za Vyama vitahitajika, basi vitahitajika kwa matakwa ya wanachama wenyewe. Lakini kazi ya kuhamasisha na kuwashawishi wananchi waweze kutambua mahitaji yao, imekwishakuanza katika ile Elimu ya Ushirika Shirikishi. Nadhani hii *Cooperation Reform Programme* itakapoanza basi Waheshimiwa Wabunge, tuungane ili tuweze kusaidiana katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilikuwa ni Vyama vya Ushirika visaidiwe kuanzisha Benki zake. Hoja ambayo imechangiwa na Mheshimiwa Edson Halinga, Mheshimiwa Stanley Kolimba na Mheshimiwa Henry Shekiffu. Sasa kama ambavyo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamependekeza na sisi tunavyosema hivyo hivyo, kwamba hivi sasa wananchi wanahimizwa kuanzisha *SACCOS* katika maeneo ya

vijijini na mijini. Mathalani katika mwaka wa fedha uliopita wa *SACCOS* ziliongezeka kutoka 1,048 mwaka 2001/2002 mpaka kufikia 1,236 mwaka wa 2002/2003. Aidha, baadhi ya Vyama vya Ushirika vimeanzisha Benki zao kwa mfano, *Kilimanjaro Cooperative Bank, Kagera Farmers Coooperative Bank.* Aidha, wadau wa Ushirika wanaendelea na utaratibu wa kuanzisha benki ya Ushirika Kitaifa. Kwa hiyo, kimsingi tunakubaliana kwamba, hizi ni jitihada nzuri ambazo zitatuondolea tatizo la wanachama wetu kutafuta mitaji kutoka katika vyombo vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa labda niunganishe hapa mwisho mwisho, Mheshimiwa Henry Shekiffu, amezungumzia suala la Serikali kuvisaidia Vyama vya Ushirika na juu ya suala zima la utandawazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme tu kwamba, katika hili, Serikali imeji-*address* vizuri sana na kusema kweli ndiyo makusudio ya Muswada wenyewe kwamba, tusaidie Vyama vya Ushirika katika kuweza kujiendesha. Lakini kimahsusi kabisa kwenye kifungu cha 5 cha Muswada huu, kinazungumzia jinsi ambavyo Serikali imepewa jukumu la kuvisaidia Vyama vya Ushirika. Nataka ninukuu kifungu cha 5 kinasema: *"The Government shall provide and create conducive social, economic and legal environment for the development and prosperity of cooperative societies."* Kwa hiyo, tayari Serikali imeshajipatia jukumu, ni *commitment* ya kuvisaidia Vyama vya Ushirika kwa namna yoyote ile. Sasa upana wake ni katika hayo ambayo Mheshimiwa Henry Shekiffu, amekuwa akiyazungumza na yatakuwa yakifafanuliwa kadri mahitaji yatakavyokuwa yanajitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu madeni ya Vyama vya Ushirika kwa wakulima, ambayo Mheshimiwa Talala Mbise, Mheshimiwa Mgana Msindai na Mheshimiwa Nimrod Mkono, walizungumzia, juu ya madeni ya Vyama vya Ushirika kwa wakulima na hasa vile Vyama vya Ushirika vilivyofilisika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa maelezo ambayo nataka niyatoe ni kwamba, katika *Cooperative Reform Programme*, tunataka tuhakiki. Uhakiki wa madeni ya Vyama vya Ushirika kwa wakulima kwa lengo la kutafuta namna ya kuyashughulikia hayo. Kusema kweli hii hata sisi katika ile Kamati ya Mheshimiwa Rais, lilijitokeza waziwazi na kusema kweli tulikusanya baadhi ya *data* ambazo zinahusiana na suala hili. Hivi sasa pamoja na maandalizi ya *Cooperative Reform Programmes,* lakini *data* tulizonazo zitatusaidia kuangalia tatizo hili na kupendekeza utaratibu wa namna ya kulishughulikia. Kwa hiyo, ni suala ambalo ni la msingi na sisi tunatilia maanani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja inayofuata ni kuhusu vikundi vidogo vidogo vya uzalishaji mali vitambuliwe na visaidiwe. Idadi ya wanachama katika Vyama vya Ushirika iongezeke. Hii kusema kweli ndiyo *thrust* ya Muswada huu. Mheshimiwa Mgana Msindai, alilizungumzia sana kuhusu hili. Sasa Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya mwaka 2002 na Muswada huu vinatambua vikundi vya kiuchumi, kwa sababu hiyo baada ya kupitishwa kwa Muswada huu vikundi vitatambulika kisheria na hivyo vitaweza kusaidiwa na kuimarishwa. Ni kweli idadi ya wanachama katika Vyama vya Ushirika ni ndogo ikilinganishwa na idadi ya Watanzania wenye sifa ya kuwa wanachama.

Pamoja na kuwa kujiunga katika chama ni hiari ya mtu, mikakati mbalimbali itatekelezwa ya kuwaelimisha na kuhamasisha wananchi watambue umuhimu na faida ya Ushirika. Tunatoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge, washiriki kikamilifu katika kuwahamasisha wananchi kuanzisha na kujiunga na Vyama vya Ushirika katika Majimbo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti na hapa kusema kweli nataka niungane sana na Mheshimiwa Jackson Makwetta, ambaye alizungumzia asubuhi hii, suala la kujiunga na Vyama vya Ushirika. Mahali pengine uhamasishaji wetu unakuwa mgumu kwa sababu sisi wenyewe ambao tunawahamasisha hatuonyeshi mfano wa mahali popote ambapo tumejiunga na Chama cha Ushirika. Kwa hiyo, unaelezea tu kwamba, jiungeni na Chama cha Ushirika, wewe mwenyewe huna. Kwa hiyo, mwananchi wa kawaida anasema aah, sasa pengine hiki si kitu cha maana kwa sababu anatuambia tujiunge yeye mwenyewe hajajiunga mahali popote. Kwa hiyo, tunakushukuru sana Mheshimiwa Jackson Makwetta, kwa changamoto uliyotoa hapa. Nadhani kusema kweli itabidi tuanze sisi Waheshimiwa Wabunge hapa, pengine tunaporudi kwenye Majimbo yetu tupate mfano mzuri wa kueleza wananchi. Hata ndani ya Bunge hapa tuanzishe mfano wa kuanzisha Chama chetu cha Ushirika cha Kuweka na Kukopa cha kutuwezesha angalau kuwaambia wananchi kwamba, *SACCOS* ina faida hii na hii.

Kwa hiyo tunadhani kwamba, katika hili ni lazima sote kusema kweli tulivalie njuga suala zima la uanzishaji wa Vyama vya Ushirika ili tuwe mfano kwa viongozi wote, hii itasaidia sana wananchi wetu kuweza kuiga.

Hoja iliyofuatia ni Maafisa Maalum *(Special Prosecutors),* kufuatilia na kusimamia kesi za ushirika. Hoja ilikuwa imeulizwa hapa na Mheshimiwa Dr. Kamala kwamba, hivi kutakuwa na tofauti gani ambapo kesi hizi sasa zinasimamiwa na *Prosecutors* wa Serikali waliopo na sasa hivi tunadhani kwamba, tukiweka hawa *Special* pengine italeta unafuu fulani. Kwa hiyo, alikuwa anauliza kwamba tofauti yake itakuwa ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nataka niseme tu kwamba, tofauti yake moja kubwa itakuwa ni kwamba, hawa watakuwa ni *Prosecutors* maalum ambao watakuwa wameteuliwa kwa kazi hiyo tu ya kusimamia na kufuatilia kesi za Vyama vya Ushirika. Tofauti na sasa ambapo *Prosecutors* hawa waliopo wana kesi nyingi za aina mbalimbali. Kwa hiyo, ili atoe *priority* ya hizi kesi za Vyama vya Ushirika, inategemea na wakati mwingine upelelezi unachukua muda mrefu sana kwa sababu takwimu zinakuwa ziko mbali. Lakini hawa kwa sababu watakuwa wako ndani ya chombo cha ushirika, hizi takwimu zitakuwa mikononi mwao na kwa hiyo itakuwa ni rahisi kufuatilia.

Lakini vile vile lilikuwepo suala la kuwahamisha hawa *Prosecutors*. Sasa hawa kwa sababu watakuwa wapo moja kwa moja kwa kazi hii tu, tunadhani kwamba, watafanya kazi yao kwa ukaribu zaidi na kuzifuatilia hizo kesi za Vyama vya Ushirika na kuhakikisha kwamba, zinafikia tamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla tu nataka nirudie tena kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge waliochangia Muswada huu. Kama nilivyokuwa nimesema kwamba, wamejitokeza kwa wingi kwa kuainisha na kuonyesha jinsi ambavyo Muswada huu ulivyo na umuhimu wa kipekee kwa Taifa na hasa hasa kwa wakulima na wananchi wote kwa ujumla. Sisi tunachukulia michango yenu kama ni changamoto ambayo itatusaidia sana katika kusimamia sheria hii na vile vile kusimamia maendeleo ya ushirika hapa nchini.

Lakini niombe tu kwamba, ushirikiano wenu utakuwa ndio ngao ya kutusaidia vile vile kutekeleza shughuli zetu. Kwa hiyo, pamoja na michango yenu hii mliyoitoa hapa, naiomba msiishie katika michango hii mliyoitoa hapa Bungeni, lakini muendelee kutushauri mara kwa mara kwa kadri itakavyokuwa inawezekana hasa baada ya kuwa Muswada huu umepitishwa kuwa sheria, basi sote sasa tuichukulie kwamba, ni *document* ambayo tumeipitisha kwa pamoja, basi tuendelee kusaidia kuwaelimisha wananchi ili waweze kuhamasika kuunda Vyama vya Ushirika imara vyenye nguvu na matumaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo ninaomba kuunga mkono hoja kwa mara nyingine. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. AARON D. CHIDUO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii nami nichangie machache katika kujadili hoja hii inayohusu Sheria mpya ya Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Waziri, pamoja na Wasaidizi wake na watalaamu wa Wizara, kwa kutuletea Muswada huu, wakati huu. Ushirika hivi sasa katika Wilaya ya Kilosa unaweza kufananishwa na mgonjwa aliye katika chumba cha wagonjwa mahututi. Unahitaji kuokolewa usife. Mimi naamini tukiupitisha Muswada huu na Sheria mpya ya Ushirika ikitekelezwa kama inavyokusudiwa, tutaokoa Ushirika hapa nchini. Hivyo, naunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mimi ni Mjumbe katika Kamati iliyoujadili Muswada huu, nitajaribu kusisitiza machache yaliyomo kwenye Muswada huu wenye lengo la kufufua, kuimarisha na kuendeleza Ushirika wakati ambapo kuna mabadiliko ya kiuchumi na kijamii katika uchumi unaoendeshwa kwa nguvu za soko la ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushirika una umuhimu wa pekee kiuchumi vijijini. Ushirika ndiyo taasisi iliyosaidia kuleta uchumi wa fedha maeneo ya vijijini. Katika shughuli za ununuzi wa mazao, Vyama vya Ushirika vimeweza kuwafikishia wananchi wa kawaida fedha nyingi katika maeneo yao, hata yale ambayo hayafikiki kirahisi. Hivi

ndivyo ilivyokuwa katika karne iliyopita katika maeneo ya Ziwa Victoria ya Kagera na Mwanza na huko Kilimanjaro na Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia Ushirika, tunazungumzia namna ya kuwafanya Watanzania walio wengi wawe wawekezaji katika uchumi na Ushirika ndiyo njia ya uhakika ya kuwawezesha wananchi wanyonge kiuchumi na hii inaendana na azma iliyotamkwa wazi katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2000. “Silaha ya wanyonge ni umoja”

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushirika tunaoufufua lazima utoe fursa ya ujasirishi na ujasirimali wa biashara kwa wanachama. Ushirika uhusishwe si kwa wakulima na wafugaji tu, bali pia katika nyanja mbalimbali, wavuvi na wauza samaki, wachimba madini wadogo wadogo, maseremala, waoka mikate, wauzaji maharage na viazi wa Gairo na hata vinyozi. Ili mradi watu waweze kuunganisha nguvu zao. Tuchukulie ushirika kama njia ya kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii mpya inavitambua vyama vidogo vidogo vya akiba na mikopo vyenye mwelekeo wa kuwa vyama imara vya *SACCOS.* Mfumo wa Vyama vya Akiba na Mikopo umedhihirisha kuwa ni endelevu na unaweza ukaanzishwa na wananchi vijijini na ukatoa huduma za kibenki huko huko vijijini. Tunashukuru kwamba, *SACCOS* kwenye Jimbo langu la Gairo, ambayo imeziba pengo Tawi la *NBC* lililofungwa Gairo katika muundo mpya wa *NBC*. Huo si tu kwamba ni ukombozi kwa wananchi wa Gairo, pia wananchi wa Kiteto na Kongwa wanahudumiwa. Hatua hii ya kuanzisha Ushirika wa Akiba na Mikopo nayo ni utekelezaji dhahiri wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma ukosefu wa Elimu ulikuwa ni kikwazo kikubwa cha maendeleo ya Ushirika. Ni ukweli usiopingika kuwa mtu asiye na elimu anakuwa mtumwa wa mazingira na atashindwa kujiletea maendeleo. Elimu ya Ushirika na stadi za binadamu ni kigezo muhimu sana katika juhudi za kufufua, kuimarisha na kuendeleza ushirika. Wanachama wa Ushirika wanahitaji elimu. Wanahitaji kuelimishwa. Wanahitaji elimu ya ujasiriamali wa biashara waweze kujenga uwezo wao kuwa wawekezaji na kuwa wajasiri katika kutafuta fursa za kufanya biashara kubwa na nzuri. Wanahitaji elimu ya uzalishaji mali na utafutaji wa masoko na elimu ya kuwapa uwezo wa kusimamia ushirika wao. Bahati mbaya suala la elimu ya ushirika kwa wanaushirika halijitokezi waziwazi katika Muswada huu, ingawa inagusiwa kidogo katika Ibara ya 74 (3).

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uongozi na mfumo wa madaraka ni mambo muhimu sana ya kuzingatiwa katika ushirika na yamezingatiwa kwa ukamilifu katika Muswada huu. Ushirika ni chimbuko la maongozi ya kidemokrasia na Utawala Bora. Haishangazi kwamba, viongozi wengi wa kisiasa walijifunza mbinu za uongozi katika ushirika. Tunayo mifano hai hapa Bungeni. Waziri mtoa hoja na Naibu wake na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, tulio nao humu Bungeni, ni wanaushirika waliobobea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hivi sasa tunachukulia kwamba, ushirika ni chombo cha biashara, tunahitaji aina mpya ya viongozi ambao hawaongozi kwa busara peke yake bali vile vile wanaongoza kwa uwezo wao kibiashara na uwezo wao kitaalam katika biashara. Tunachotaka kuona ni viongozi wanaokubali kuongozwa na wanachama wanaokubali kuachia madaraka kwa mzunguko, wanaongoza kwa kujasirisha kuwapa uwezo wanachama kujiendeleza kiuchumi na wanazingatiwa kwa ukamilifu misingi ya Utawala Bora, yaani uwazi, uwajibikaji, kutabirika na ushirikishwaji wa wanachama katika maamuzi muhimu ya vyama vyao.

Lazima tujiepusha na ushirika unaoundwa kwa kulazimishwa, kijiji kizima kiwe chama cha ushirika unaoundwa kwa faida ya watu wachache wanaotaka kutumia nguvu za walio wengi na ulio na viongozi wanaong'ang'ania madaraka, viongozi watawala na viongozi wa maisha na lazima tuhakikishe kuwa viongozi wabadhirifu na wasiofuata maadili hawapati nafasi ya kuongoza na baadaye kuuvuruga Ushirika. Naona haya yote yamezingatiwa katika Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho suala la Vyama vya Ushirika na vyama huru lazima lisisitizwe, visichukuliwe kama ni Idara za Serikali na lazima hili lizingatiwe na Maafisa wa Ushirika walioko Wilayani. Maafisa Ushirika wanaondokana na tabia ya kuwa vinara kusimamia sheria na miongozo bali wasaidie kujenga uwezo wa Vyama vya Ushirika kujikagua vyenyewe na Shirika la Ukaguzi, pamoja na kuwa mkaguzi wa nje, litoe fursa ya ripoti za ukaguzi wa uongozi zipelekwe moja kwa moja kwa wanachama ili ripoti hizo ziwaelimishe na kuwaongezea uwezo wao wa kuwasimamia viongozi na hasa kuzuia wizi na ubadhirifu.

Tunakumbuka kuwa Chama cha Ushirika ni Muungano wa watu waliojiunga pamoja kwa hiari, kwa madhumuni ya kufanikisha mahitaji yao kwa kuanzisha na kumiliki chombo chao kidemokrasia na kuchangia mtaji unoahitajika kwa usawa na kukubali kuyakabili matatizo na kupata manufaa kutokana na shughuli zake ambazo wao hushiriki kikamilifu.

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba, kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja ya Waziri wa Ushirika na Masoko.

Naomba nianze kwa kuangalia kifungu namba 63 na vifungu vyake cha kwanza mpaka cha nne, ambavyo vinazungumzia Kamati ya Chama cha Ushirika na Wajumbe wake, wanaopatikana pindi wakiwa madarakani na udhibiti wa vipindi ambavyo wanaruhusiwa kuongoza. Nia ya Muswada au sheria ni nzuri sana inalenga kudhibiti baadhi ya Wajumbe wa Kamati wajanja wajanja, kwa faida zao wasiendeleee kuhodhi madaraka. Ili hili liweze kufanikiwa vizuri, nashauri Serikali isaidie kutoa elimu kwa wananchi au wanachama juu ya elimu ya Ushirika kuhusu haki zao na wajibu wao na vile vile waondoe uwoga wa kudai haki zao. Hili tatizo lipo zaidi katika vyama vya mazao. Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo vinaenda vizuri nchini kwa sababu vingi vipo katika sehemu za kazi na wanachama wake wana elimu zaidi ukilinganisha na wanachama wa vyama vya mazao, ndiyo maana vinaenda vizuri kwa sababu wanachama

wake wana elimu na wana mwanga wa sheria za vyama vyao na wanajua nini wajibu wao na nini haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ambayo nataka kuzungumzia ni kifungu cha 67. Katika kifungu hiki kinasema Mrajisi kwa kushauriana na Waziri, kwa faida ya wanachama na umma, anaweza kuingilia kati kwa kuwasimamisha viongozi waliopo, kuweka uongozi wa muda na hatimaye kuweka uongozi mwingine. Vile vile kinaelezea wale waliosimamishwa wanavyoweza kudai haki zao. Kazi hii ya kuingilia kati itafanyika kama Maafisa Ushirika walio katika Halmashauri zetu za Wilaya, Miji na Majiji, watatengewa fedha za kufanyia kazi huko vijijini wanakotakiwa kutembelea Vyama vya Ushirika.

Bila kuwapatia fedha katika kasma zao kuwawezesha kutembelea Vyama vya Ushirika, vyama vingi vitaendelea kudorora ama kufanywa ni mali ya viongozi wachache wajanja. Kama Maafisa Ushirika hawakutengewa fedha na kulazimishwa kutembelea Vyama vya Ushirika, wanaweza kuwa wanafanya kazi kwa kufadhiliwa na Vyama vya Ushirika. Hali kama hii ikitokea, kuna hatari ya Maafisa Ushirika kurubuniwa na viongozi wabadhirifu. Hali hii inaweza kuzorotesha Vyama vya Ushirika. Katika baadhi ya maeneo baadhi ya Maafisa Ushirika, wameshirikiana *(collude)* na baadhi ya viongozi wasio waaminifu, kufanya ubadhirifu katika vyama na kushindwa kuondoa au kumaliza migogoro katika vyama. Naomba nishauri kuwa hali kama hii ikiweza kubainika, basi Maafisa Ushirika husika wachukuliwe hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Serikali imefuta baadhi ya kodi zenye kero na kodi ya maendeleo ni mojawapo. Kwa kufuta kodi hizi, sasa hivi Serikali inatoa fedha kwa Halmashauri kwa ajili ya kuendesha Serikali katika kutoa hiyo fedha, ihakikishe kuwa kila Idara ya Halmashauri na Ushirika ikiwa mojawapo inapata fedha zake za kufanyia kazi. Hii itaondoa tabia ya baadhi ya Maafisa Ushirika kufanya kazi kwa kufadhiliwa na Vyama vya Ushirika. Naomba hili lifanyike ili nia njema ya kuimarisha na kuendeleza Ushirika itekelezwe. Naomba kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mchango wa kuzungumza, naomba nipendekeze kuwa *Primary Societies* ziweze kudhibitiwa na Halmashauri, kwani ndiyo Mamlaka ya Kiserikali yenye mamlaka ya kusimamia shughuli zote za wananchi vijijini. Aidha, hata Afisa Ushirika wa Wilaya, anayesimamia Vyama vya Msingi anaripoti kwenye mamlaka hii.

*Secondary Societies* zidhibitiwe na Mkoa na *Apex Societies/Federation* ziwe moja kwa moja chini ya Waziri. Kama haiwezekani, *due to technical reasons* kubadilisha. Sasa hivi kifungu husika *section II, 7 (2)* basi Serikali ione uwezekano wa kuliingiza hili kwenye kanuni. Bado nalia na mashamba yaliyobinafsishwa na kumilikishwa Vyama vya Msingi. Utafiti wa kina ufanywe kubaini hali halisi ya mashamba hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa faida ya nchi na watu hao, mashamba hayo yarudishwe miliki yake kwa vijiji na Vyama vya Msingi vya Ushirika viwe *custodian,* kwani tatizo liko wapi? Wanachama 800 katika kila kijiji na wananchi 1,000 ni nani atastahili zaidi kufaidi mali iliyotaifishwa kwa faida ya nchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana suala hili lisipuuzwe.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko, pamoja mambo mengine mimi nimeshukuru sana kuhusiana na Muswada huu mpya, kwani ile iliyopita ya mwaka 1991 iliua kabisa Ushirika. Sasa naomba nijue kuhusu viongozi waliokaa zaidi ya muda wa miaka miwili hadi vipindi vinne ni nini hatma yao? Aidha, viongozi wa aina hii baada ya kupitisha sheria hii mpya, je, watalazimisha kuita mkutano wa uchaguzi au watakuwa wameondoka kwa kukosa sifa? Suala la kiongozi aliyemaliza muda wake kugombea tena ni jambo jema, lakini kuna madhara kiongozi anaweza kuamua kutumia fedha za wananchi/washirika kwa kuhonga Wajumbe, jambo ambalo limefanyika katika Muswada uliopita na kuharibu kabisa. Kama utawala umemaliza muda wake uondoke na hakuna sababu ya kung’ang’ania mbona anakuwa hajafukuzwa na bado maoni au ushauri wake utahitajika na bado ana uwezo wa kushauri uongozi mpya. Mbona Rais akimaliza muda wake huachia ngazi hata kama ni mzuri? Hivyo, napingana na maoni ya kamati ya kuhusu kugombea tena, labda nishauri endapo uongozi utamaliza muda wake uondoke aweze kugombea tena baada ya kipindi kinachofuatia kwisha mfano, muda wako umeishia 2003 hutagombea hadi *term* inayofuata kumalizika muda wake, *means that you can contest after the end of the following term.*

Hii itasaidia kwa *term* mpya kuweza kujua kwa undani, uchafu ambao utakuwa umefichika na kama hautakuwepo basi isiwe ajabu kwa yeye kugombea tena baada ya kuishi kwa kipindi kinachofuata. Nafikiri hapo nimeeleweka. Naunga mkongo suala la *STABEX* liwe wazi kwa Wabunge na wananchi wote, maana huu usiri sijui ni kwa faida ya nani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja maana nilisubiri hii hoja kama Waisraeli au Wayahudi walivyokuwa wakimsubiri Yesu Kristo.

**MHE. MUSA A. LUPATU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Waziri Waziri wa Ushirika na Masoko, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wote wa Wizara, kwa kuleta Sheria mpya ya Ushirika. Sheria hii mpya sasa inalingana na mabadiliko ya kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiteknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza katika sheria yapo mambo machache ambayo yanahitaji ufafanuzi na maelekezo ili utekelezaji wa sheria hii uwe na manufaa kwa maendeleo ya Ushirika nchini. Kwanza, lipo suala la *management* ya Vyama vya Ushirika kuwa uongozi na mamlaka ya uendeshaji utakuwa chini ya Bodi. Hii ni sahihi ili kuweka bayana utendaji wa kibishara katika Ushirika. Lakini katika *schedule of amendment* kifungu cha 63, kinachoelezea juu ya Bodi kimeingia bila kuunda Bodi yenyewe katika kifungu cha 62.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni juu ya viongozi watendaji. Sheria iko kimya juu ya ajira za watendaji na kuweka uhuru mkubwa kwa kusema vyama vitajiwekea utaratibu wa miundo. Ni vema sheria ikaweka angalau misingi ya miundo ya Ushirika na uendeshaji wake.

Tatu, sheria inaruhusu vikundi kujisajili kwa matarajio ya kuwa Vyama vya Ushirika kamili na kwamba, Vyama vya Ushirika vitakuwa na majukumu ya kuvilea vikundi kuelekea kwenye Ushirika kamili. Lakini sheria haionyeshi uhusishwaji wa Chama cha Ushirika, kinapaswa kulea vikundi wakati wa usajili wa kikundi hicho. Kwa mujibu wa sheria hii kinaomba usajiri moja kwa moja kwa msajili wa Vyama vya Ushirika bila kupitia kwa Chama cha Ushirika mlezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi juu ya masuala hayo matatu, yaani bodi, ajira za watendaji na vikundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Wizara yake, kwa kuleta Muswada huu kwa wakati huu. Ni Muswada muhimu katika juhudi za Taifa la Tanzania katika kuinua maisha ya wananchi kiuchumi na kupambana na umaskini. Kwa sababu hii naunga mkono Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuweka mambo wazi, Taifa hili lingefaidika sana kama Serikali ingetanguliza kwa kutuletea ripoti ya utafiti *(Post Evaluation Report),* ikielezea wazi nini kilichosababisha kusambaratika kwa Ushirika wa zamani miaka ya 1980.

Pili, Muswada huu ungeletwa mapema, mara tu baada ya kuunda Wizara ya Ushirika na masoko mwaka 2000/2001. Muswada huu unalenga kuleta mazingira imara ya kuanzisha Ushirika mpya ambao utazingatia hali halisi ya ushindani wa masoko, bei na uzalishaji katika sekta mbalimbali za kiuchumi. Katika uundaji wa Vyama vya Ushirika sasa sheria hii iweke wazi kuwa hakuna suala la kulindana na kupanga mienendo ya masoko na bei za mazao na bidhaa. Biashara ya faida itakayofanywa na vyama hivi vya ushirika itategemeaa ubora na ujasiri wa vyama na siyo vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Sheria ya Ushirika ya zamani ilielekeza Vyama vya Ushirika katika kupanga na kutafuta masoko nje na bei za mazao makubwa ya biashara kama kahawa, pamba na chai. Nashauri kwa sasa Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2003, ielekeze wazi kwenye kuzalisha mazao ya chakula na mazao mchanganyiko ya chakula na biashara kwa kusisitiza soko la ndani.

Pili, sheria ya mwaka 2003, ione umuhimu wa kuweka mazingira ya kuwawezesha kwa mikopo wakulima wadogo wadogo watakaojiunga katika Vyama vya Ushirika.

Tatu, sheria hii katika kuwawezesha wakulima wadogo, iweke mikakati ya kuwaingiza katika kilimo cha kisasa cha umwagiliaji na kilimo bora kikitumia nyenzo za kisasa.

Nne, katika kutimiza azma ya kuwaingiza wakulima wadogo katika mfumo wa kilimo cha kisasa, Sheria ya mwaka 2003, ione umuhimu na iweke wazi kuviwezesha vikundi vya wakulima watakaojiunga kwenye Vyama vya Ushirika vya kuvuna maji ya mvua kwa kuchimba na kujenga mabwawa ya maji na kuwauzia wakulima maji ya kumwagilia mashamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuwawezesha wana ushirika na vyama vyao liwekwe wazi katika Muswada huu. Kwa hapo nashauri kuwa, Mfuko Maalum uanzishwe kisheria kwa sababu pasipofanywa hivyo, Ushirika mpya chini ya Sheria ya mwaka 2003 utasambaratika kwani vyama hivi kwa sasa haviwezi kukopesheka na taasisi za fedha za sasa za kibiashara. Sheria iweke wazi kuwa wachangiaji katika mfuko huu iwe pamoja na Serikali, Taasisi za Kiserikali, *NGOs* na mifuko mbalimbali ya makundi mbalimbali kama vijana, wanawake na kadhalika. Pia Sheria iweke wazi kuwa Benki kama *CRDB,* ambayo kwa miaka mingi imetumia jina la Ushirika na Maendeleo Vijijini, pasipokutoa huduma kwa walengwa, basi sheria hii iwasiliane na *CRDB* kuona umuhimu wa kuchangia katika mfumo wa ushirika. Uwezekana wa Benki za *NMB and TPB* kuwa wakala wa Mfuko huu pia uwekwe kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazingira ya ushindani na uwazi, chini ya mfumo wa uchumi wa soko huria, uanzishwaji wa Vyama vya Ushirika kuzingatia sheria ya mwaka 2003, suala la elimu kwa wananchi kujiunga na Ushirika mpya ni muhimu sana. Ningeshauri kuwa elimu ya Ushirika ielekezwe na Halmashauri za Wilaya ambazo ndiyo zipo karibu sana na wananchi kiuchumi na kimaendeleo. Suala zima la kusimamia ushirika liwe chini ya Halmashauri na siyo Wizara. Nyenzo zote pamoja na uwezeshaji wa Vyama vya Ushirika usimamiwe kisheria na Halmashauri za Wilaya. Kwa kufanya hivyo, urasimu *(bereaucracies)* na kulindana kama ilivyokuwa wakati wa Ushirika wa zamani, kutaweza kuondolewa kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kuwa, kama Sheria ya mwaka 2003 isipoweka wazi na kusisitiza kuwa Vyama vya Msingi vya Ushirika ni vya washirika wenyewe na viendeshwe na kudhibitiwa na wanachama wenyewe. Sheria hii ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2003 itaanzisha Taasisi ambayo haitahimili ushindani na uwazi katika mfumo wa soko huria katika uchumi wa ulimwengu wa sasa.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kukupongeza sana kwa kuleta Muswada huu muhimu kwa wakulima. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Ushirika ndiyo mkombozi wa wakulima. Vyama vya Ushirika ndicho chombo cha wakulima kuuza mazao yao kwa bei ya uhakika. Katika soko huria, ni vigumu kupanga bei ya mazao yao na wakulima kupunjwa, hivyo ipo haja ya maeneo ambayo hayana Vyama vya Ushirika kuunda vyama hivyo ili vilete ukombozi kwao. Kwa mfano, Mkoa

wa Dodoma hatuna Chama Kikuu cha Ushirika, wakulima hupata shida ya mazao yao na hasa zao la biashara karanga, zabibu, alizeti na ufuta.

Mkoa wa Dodoma umeunda Vyama vya Ushirika, je, kwa nini Serikali isiruhusu Mkoa wa Dodoma kuunda Chama cha Ushirika katika Wilaya kama wametimiza masharti, kwa nini wasiruhusiwe kuunda Chama Kikuu cha Ushirika ikiwemo Wilaya ya Mpwapwa? Hii itasaidia sana wakulima kuimarisha/kuboresha kilimo cha mazao ya biashara kwa wananchi wa Mkoa wa Dodoma, kwa kuwa watakuwa na mahali pa kuuza mazao yao kuliko hali ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri na watendaji wote, kwa kuleta Muswada huu wa Sheria kwa wakati muafaka, hasa katika kipindi cha mfumo tofauti kabisa wa uchumi. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri kuwa kazi kubwa ya kuanza nayo ni kutoa elimu katika ngazi zote za Ushirika nchini, ili waielewe vizuri sheria hii na waione kuwa ni yao. Chuo chetu cha Ushirika kipewe kila aina ya msaada wa kifedha ili kifanye kazi hiyo barabara. Mwanzo huu ni muhimu tukubali kwa gharama yoyote ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kazi nzuri aliyoianza Waziri kwa kuwabana viongozi wote wa Ushirika waliopoteza fedha za wanaushirika waendelee kubanwa kisheria ili kuwarejeshea imani wale wote waliokata tamaa kutokana na wizi uliokithiri huko nyuma. Hatua hii ya pili itaendelea kurudisha imani kwa hatua ya kujenga ushirika huu mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi nyingine ambayo ni budi Wizara ikazanie ni suala zima la kusimamia upatikanaji na urejeshaji wa mikopo kwa ajili ya kununulia mazao yao muhimu. Naelewa kuwa suala hili ni nyeti na linahitaji utalaamu kati ya uongozi wa Ushirika katika kuamua jinsi gani wachukue mikopo na kwa sababu zipi na kwa faida ipi. Suala la masoko na upatikanaji wa pembejeo kwa ajili ya wanaushirika, lipewe umuhimu wake. Pawepo upendeleo maalumu kwa Vyama vya Ushirika kupewa pembejeo muhimu ili kuwavutia sana wale wasio wanaushirika. Hata mbolea ambazo zinaandaliwa kusambazwa nchini, kila aina ya msaada ifanyike ili mbolea nyingi ipitie Ushirika na inunuliwe kupitia huko. Hata kama safari hii tutakuwa tumechelewa, lakini mwaka ujao tuwaandae vizuri sana ili wawezeshwe kuifanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninashauri kuwa Mheshimiwa Waziri, aandae semina maalum, kwa Wabunge wote na Viongozi wetu Wakuu, ili sote tuwe na msimamo mmoja ili tusiwe na watu wanaotumia utandawazi kukwamisha jitihada hizi za Ushirika tunaotaka kuunda.

Ni vizuri sote tujue tunafanya nini. Mengi tutayasema kwenye semina hiyo. Ninaunga mkono hoja hii mia kwa mia na ninampongeza Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Uongozi wote wa Wizara kwa mwanzo huu mzuri.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yafuatayo ni maoni ya wananchi wa Siha, juu ya Muswada wa Sheria Mpya ya Ushirika Nchini *(The Cooperative Societies Act 2003):-*

Kwanza, Ushirika ni muungano wa watu ambao wana lengo moja la kukubaliana na matatizo yao na ambao wana amini katika mkakati wa kuondokana na unyonge wao. Kwa hiyo, sheria yoyote itakayotungwa katika nchi yetu ya Tanzania kuhusu Ushirika, lazima ihakikishe kuwa inawapa madaraka na mamlaka bila kuingiliwa na chombo chochote kile ikiwemo dola.

Pili, kwa ujumla Muswada huu hauoani na madhumuni ya sera ya maendeleo ya ushirika ya mwaka 2002 kifungu cha 1.5 (i).

Tatu, ukurasa wa 14 sehemu ya 7(3), Chuo cha Ushirika kitakuwa Chuo Kikuu. Waziri atakiagiza wakati kitakuwa na *senate* yake ya kukiongoza?

Nne, ukurasa wa 14/15 sehemu ya 10(1) Mrajisi na Naibu Mrajisi ndivyo vyeo vilivyotumika. Anayetajwa kwenye kifungu cha 12 (2) kama Kamishna Msaidizi ni nani?

Ukurasa wa 43 kifungu cha 70(2), Mrajisi amekuwa mtendaji wa Vyama vya Ushirika, kwa jinsi alivyopewa madaraka mengi mno ya utendaji juu ya vyama vinavyotakiwa kujidhibiti, kumilikiwa na kuendeshwa na wanachama wenyewe katika vifungu vya 73 (1) (a) na (d), Mrajisi ametakiwa atoe kibali chake kwa chama kitakachotaka kuwekeza. Vifungu (b) na (c) havikutaja hivyo.

Kifungu cha 73 (2) neno *"advise"* liwe *"direct"* au *"order",* kwa maana ya lazima, ya kutii, iliyomaanishwa na maneno *shall be, the duty of every registerd society to comply with such directions.* Kama kwa mujibu wa kifungu cha 73(3) na (4) kitakachoshindwa kutii ushauri wa Mrajisi kitaadhibiwa, basi Mrajisi akishauri chama kuwekeza na chama kikapata hasara, Mrajisi awajibike, *wrong directives should equally be punishable.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mrajisi ameonyeshwa na sheria hii kama mtendaji aliye na taaluma na uwezo mkubwa wa kibiashara kwa maamuzi makubwa ya kibiashara ambayo inambidi afanye kwa niaba ya Vyama vya Ushirika vinavyotakiwa kuendeshwa kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 81 (3) kinatamka faini ya shilingi 100,000/= kwa kila siku kwa Afisa wa Chama atakayeshindwa kutekeleza kifungu cha 80 cha sheria. Faini hii ni *unreastic* ikitiliwa maanani kipato cha watendaji katika Ushirika na Taifa kwa ujumla. Vifungu vya 94 (2) (c) na 96 (3) (d), Mrajisi akikataa mapendekezo ya wanachama kwa sababu yoyote ile, atakuwa amekiuka na kunyima uhuru, utashi na demokrasia ya wanaushirika. Ukurasa wa 86 sehemu ya 63 (5) haimo kwenye sheria ya zamani wala hii mpya.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa *Sir* George Clement Kahama, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje na Maafisa Wakuu wa Wizara yako kwa kuleta Muswada huu mzuri sana. Napenda pia nikushukuru Waziri kwa kutuma Ofisa Mwandamizi wa Ushirika kuja Mwanga kuongea na vyama vyetu vya Ushirika. Hili lilikuwa jambo kubwa kwetu hasa ikiwa ni kutekeleza ahadi uliyotupa ya kuvisaidia vyama hivi viweze kununua kahawa ya wakulima na kuiuza mnadani, pamoja na kuwasaidia wakulima wanunue pembejeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nataka niseme tu kwamba, tofauti yake moja kubwa itakuwa ni kwamba, hawa watakuwa ni *Prosecutors* maalum ambao watakuwa wameteuliwa kwa kazi hiyo tu ya kusimamia na kufuatilia kesi za Vyama vya Ushirika. Tofauti na sasa ambapo *Prosecutors* hawa waliopo wana kesi nyingi za aina mbalimbali. Kwa hiyo, ili atoe *priority* ya hizi kesi za Vyama vya Ushirika, inategemea na wakati mwingine upelelezi unachukua muda mrefu sana kwa sababu takwimu zinakuwa ziko mbali. Lakini hawa kwa sababu watakuwa wako ndani ya chombo cha ushirika, hizi takwimu zitakuwa mikononi mwao na kwa hiyo itakuwa ni rahisi kufuatilia.

Lakini vile vile lilikuwepo suala la kuwahamisha hawa *Prosecutors*. Sasa hawa kwa sababu watakuwa wapo moja kwa moja kwa kazi hii tu, tunadhani kwamba, watafanya kazi yao kwa ukaribu zaidi na kuzifuatilia hizo kesi za Vyama vya Ushirika na kuhakikisha kwamba, zinafikia tamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla tu nataka nirudie tena kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge waliochangia Muswada huu. Kama nilivyokuwa nimesema kwamba, wamejitokeza kwa wingi kwa kuainisha na kuonyesha jinsi ambavyo Muswada huu ulivyo na umuhimu wa kipekee kwa Taifa na hasa hasa kwa wakulima na wananchi wote kwa ujumla. Sisi tunachukulia michango yenu kama ni changamoto ambayo itatusaidia sana katika kusimamia sheria hii na vile vile kusimamia maendeleo ya ushirika hapa nchini.

Lakini niombe tu kwamba, ushirikiano wenu utakuwa ndio ngao ya kutusaidia vile vile kutekeleza shughuli zetu. Kwa hiyo, pamoja na michango yenu hii mliyoitoa hapa, naiomba msiishie katika michango hii mliyoitoa hapa Bungeni, lakini muendelee kutushauri mara kwa mara kwa kadri itakavyokuwa inawezekana hasa baada ya kuwa Muswada huu umepitishwa kuwa sheria, basi sote sasa tuichukulie kwamba, ni *document* ambayo tumeipitisha kwa pamoja, basi tuendelee kusaidia kuwaelimisha wananchi ili waweze kuhamasika kuunda Vyama vya Ushirika imara vyenye nguvu na matumaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo ninaomba kuunga mkono hoja kwa mara nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya kwanza ya kuwapa viongozi elimu imekamilika. Ninaomba ufuatiliaji wa kitaalam wa Vyama hivi vya Ushirika vya Msingi. Hivyo, tupelekee tena yule mtalaam wako ili afuatilie hatua zilizofikiwa baada ya kuwaelimisha Viongozi wa Vyama vya Ushirika.

Suala la tatu linahusu Vyama vya Kuweka na Kukopa *(SACCOS).* Niliwaletea maombi yetu kuwa mtusaidie kuviimarisha kwa kuwapa elimu vyama vyetu vya kuweka na kukopa. Mwaka 2001 tulianzisha vikundi 25 Wilayani Mwanga na kuvisaidia vifikie hatua ya kuandikishwa na kuwa Vyama vya Kuweka na Kukopa. Mpaka leo tunavyo vyama 12 vya kuweka na kukopa, lakini bado wana mitaji midogo mno, hawawezi kuwa na mitaji ya kukopeshana. Leo tena naomba mtafute utaratibu mtusaidie tuwe na mtaji mdogo hata shilingi 10,000,000/= tuwawezesha wakulima waweze kukopeshana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupewa nafasi hii. Uchambuzi wa sura ya kumi na nne, Uvunjaji wa Vyama vya Ushirika, sura hii ina jumla ya aya ishirini na tatu na inaanzia aya ya tisini na saba hadi Ibara ya mia ishirini, ikielezea ni wakati gani na ni utaratibu gani utumike kuvunja Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wangu, nitaongelea Ibara ya mia moja na mbili, inayoelezea nguvu na wajibu wa Mfilisi wa Vyama vya Ushirika. Mfilisi ni mtu atakayeteuliwa kukusanya mali na kulipa madeni ya Chama cha Ushirika kinachovunjwa. Ni muhimu kwa sababu ndiye anayekuwa na wajibu wa kukusanya mali za hiyo kampuni au Chama cha Ushirika kinachovunjwa au kufilisiwa na kulipa madeni yake na kugawa kwa usawa chochote kinachobakia kwa wadau wa kampuni au chama husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Muswada huu, Vyama vya Ushirika vitakavyosajiliwa chini ya sheria hii, vitaendelea kuwa na uwepo wa kipekee kama yalivyo makampuni. Uwepo huu wa kisheria utavifanya viwe kama mtu mbele ya sheria mwenye uwezo wa kushtaki na kushtakiwa, uwezo wa kumiliki mali na uwezo wa kurithi kwa jina lake chenyewe bila kuathiriwa na uwepo au kutokuwepo kwa wanachama wanaokiunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu huyu anayeundwa kisheria anapovunjwa ni lazima kuwepo na Mfilisi ambaye anatakiwa awe na mamlaka kamili ya kisheria, kufanya kile ambacho mtu huyu alishindwa kufanya kwa minajili ya kulinda wadau wa chama hiki. Kwa minajili hii basi, Mfilisi anateuliwa hapa inabidi awe na mamlaka na uwezo kama ule ule alio nao mfilisi anayeteuliwa kuifilisi kampuni iliyosajiliwa chini ya Sheria ya Makampuni (sura ya 212 ya Sheria za Tanganyika).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nguvu na mamlaka ya Mfilisi wa Makampuni yameainishwa vema katika aya ya 190 ya Sheria ya Makampuni (Sura ya 212 ya Sheria za Tanganyika), kurejewa katika sheria mpya ya makampuni ya mwaka 2002 aya ya 301kuwa kama ifuatavyo:-

(a) Kufungua kesi au kutetea kesi yoyote kwa jina la na kwa niaba ya kampuni.

(b) Kuendelea na biashara ya kampuni kwa kadri itakavyokuwa na manufaa kwa minajili ya ufilisi wa kampuni hiyo.

(c) Kuteua wakili kumsaidia katika kuendesha shughuli zake na kama mfilisi mwenyewe ni wakili, haruhusiwi kumteua wakili ambaye ni mwenza *(partner),* isipokuwa tu kama huyo mwenza amekubali kufanya kazi bila malipo.

(d) Kuwalipa wadai wa daraja lolote lile deni lote.

(e) Kufanya makubaliano na wadai na wadaiwa wa kampuni jinsi ya kulipa madeni inayodaiwa kampuni au inayodai.

(f) Kuuza mali za kampuni zinazohamishika na zisizohamishika kwa minada ya hadhara au kwa mikataba.

(g) Kufanya kazi ikiwa ni pamoja na kuingia mikataba na kusaini nyaraka mbalimbali kwa jina na kwa niaba ya kampuni.

(h) Kutoa na kupokea cheki pamoja na dhamana nyingine kwa niaba na katika jina la kampuni.

(i) Kuthibitisha na kudai na kupokea gawio katika shauri la wadaiwa wa kampuni.

(j) Kuweka dhamana mali za kampuni ili kupata mkopo unaohitajika.

(k) Kuchukua katika jina lake kama mfilisi, barua za usimamizi wa mirathi ya mdaiwa yeyote wa kampuni na kufanya kila liwezekanalo kukusanya madeni ya kampuni.

(l) Kuteua mwakilishi kufanya shughuli yoyote ambayo anashindwa kufanya yeye mwenyewe.

(m) Kufanya mambo mengine anayoona yanafaa kwa minajili ya kufanikisha uvunjaji wa kampuni na kugawa mali za kampuni kwa wale wote wanaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia nguvu alizopewa Mfilisi wa Makampuni kama ilivyoainishwa hapo juu na ukalinganisha na nguvu alizopewa Mfisili aliyeteuliwa kusimamia uvunjaji wa Chama cha Ushirika kama ilivyoainishwa katika aya ya mia moja na mbili ya Muswada huu, utaona kwamba, nguvu za huyu Mfilisi wa Vyama vya Ushirika zimebanwa mno.

Unapobana uwezo wa mtu anayeteuliwa kuwa Mfisili wa Vyama vya Ushirika na wakati huo huo kutarajia afanye kazi ngumu ya kukusanya mali na kulipa madeni ya Chama cha Ushirika kinachofilisiwa, ni kama vile kumpa mtu shoka bila mpini na kutarajia mtu huyo afyeke msitu, alime na kuleta mavuno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kukusanya madeni ya mtu aliyekufa au anayekaribia kufa ni ngumu sana. Ili kufanikisha hili, inapaswa anayepewa kazi hii apewe vitendea kazi vya kutosha. Sasa ukiangalia uwezo aliopewa Mfislii wa Chama cha Ushirika kinachovunjwa, kama ilivyoainishwa katika aya ya mia moja na mbili ya Muswada huu, utaona kabisa kwamba, nguvu zake hazifikii hata nusu ya zile alizonazo mtu anayeteuliwa kuwa Mfilisi wa Makampuni. Nguvu ya Mfilisi huyu zinaanishwa kuwa na kwa sababu hii ni vigumu kwake kutimiza wajibu wake ili kulinda maslahi ya wadau wa chama husika. Mamlaka yake yameainishwa katika aya hii ya 102 kuwa:-

(a) Kufungua na kutetea kesi yoyote kwa jina lake au ofisi yake na kutokea Mahakamani mwenyewe kwa niaba ya Chama cha Ushirika.

(b) Kupeleka migogoro kwa usuluhishi.

(c) Kuchanganua kiasi cha mchango kinachotakiwa kutolewa na wanachama waliopo na wa zamani kwenye mali za chama.

(d) Kuchunguza madeni chama kinachodaiwa na kuchambua suala la madeni yenye kipaumbele.

(e) Kuamua ni watu gani na kwa kiasi gani watabeba gharama za Ufilisi wa chama husika.

(f) Kuangalia na kuchambua madeni ambayo chama kitakuwa kinadai.

(g) Kuchukua na kuhifadhi vitabu, nyaraka na mali za chama.

(h) Kutoa maelekezo kuhusu ukusanyaji na ugawaji wa mali za chama na uondoaji wa vitabu na nyaraka za chama kama itakavyoonekana inafaa kwa ufilisi wa chama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kupendekeza kuwa, kwa vile mtu anayeteuliwa kuwa Mfilisi wa Vyama atakuwa anafanya kazi katika mazingira yaleyale ya Mifilisi wa Makampuni na kwa malengo yale yale, basi ni muhimu naye akapewa meno kama aliyonayo Mfilisi wa Makampuni. Ni pale tu huyu Mfilisi vya Vyama atakapokuwa na uwezo wa kufanya awezalo kufanya, Mfilisi wa Kampuni atakapoweza kufanya kazi yake ya Ufilisi wa Vyama kwa mafanikio na kwa faida ya wadau wote wa Ushirika. Mfilisi wa Vyama apewe nguvu kama alizonazo Mfilisi wa Makampuni.

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi hii ya kuhitimisha majadiliano ya hoja yangu kuhusu Muswada wa Sheria ya Ushirika wa Mwaka 2003.

Nashukuru pia kwamba, umeona inafaa kutoa muda zaidi wa kujadili hoja hii. Muda huo umetuwezesha na umewawezesha Waheshimiwa Wabunge wengi kutoa mawazo yao ambayo yatatusaidia sana katika utekelezaji wa hatua mbalimbali ambazo tumeziainisha katika sheria hii ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara, Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, kwa kuwasilisha maoni ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu tarehe 7 Oktoba, 2003. Maoni ya Kamati yatatusaidia kuandaa mipango ya kutekeleza majukumu yaliyo mbele yetu hususan katika kuandaa kanuni za Vyama vya Ushirika na mpango kabambe wa Mageuzi ya Ushirika, yaani *Cooperative Reform Programme.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kumshukuru Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Naibu Waziri wa Ushirika na Masoko, ambaye amefafanua vizuri masuala mengi ya Waheshimiwa Wabunge, waliochangia katika hoja hii. Vile vile napenda nichukue nafasi hii, kumshukuru Mheshimiwa Aggrey Mwanri, kwa kueleza kwa ufasaha na ufundi, faida za Ushirika dhidi ya mfumo mwingine wa Ubepari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya Waheshimiwa Wabunge 35 wamechangia hoja hii na kati ya hao 11 wamechangia kwa maandishi na 24 wamechangia kwa kuzungumza. Kwa heshima na taadhima, napenda kuwatambua kwa kuwataja majina yao wote waliochangia katika hoja hii kama ifuatavyo:-

Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuzungumza ni Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, Mheshimiwa Aisha Phillipo Magina, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, Mheshimiwa Isaac Cheyo, Mbunge wa Bariadi Magharibi, Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mbunge wa Hai, Mheshimiwa Talala Mbise, Mbunge wa Arumeru Mashariki, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mbunge wa Nkenge, Mheshimiwa Dr. James Msekela, Mbunge wa Tabora Kaskazini, Mheshimiwa Prof. Daimon Mwaga, Mbunge wa Kibakwe, Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge, Mheshimiwa Paschal Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mbunge wa Shinyanga Mjini, Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, Mbunge wa Gairo, Mheshimiwa Stanley Kolimba, Mbunge wa Ludewa na Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, Mbunge wa Kyerwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mbunge wa Siha, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, Mheshimiwa Edson Halinga, Mbunge wa Mbozi Mashariki, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mbunge wa Njombe Kaskazini, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mbunge wa Karatu, Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mbunge wa Lushoto, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mbunge wa Musoma Vijijini, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mbunge wa Misungwi na Mheshimiwa Chibulunje, Mbunge wa Chilonwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa kuandika ni hawa wafuatao: Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mbunge wa Siha, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, Mheshimiwa Leonard Shango, Mbunge wa Iramba Magharibi, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mbunge wa Moshi Vijijini, Mheshimiwa Musa Lupatu,

Mbunge wa Korogwe Magharibi, Mheshimiwa Ismail Iwvatta, Mbunge wa Manyoni Magharibi, Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, Mbunge wa Gairo, Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mbunge wa Hai, Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, Mbunge wa Mwanga, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini na Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mbunge wa Musoma Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge katika michango yao wamezungumzia masuala mbalimbali ambayo yanahitaji ufafanuzi, lakini pia yanayolenga katika kuboresha Muswada na kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Nawashukuru sana kwa michango yenu Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli si rahisi kujibu hoja zote ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezizungumzia. Lakini mimi na Naibu wangu, tumejitahidi kwa kadri tunavyoweza, kuyatumia mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge kwa kufanya masahihisho au marekebisho katika maeneo mbalimbali ya Muswada kama yalivyoainishwa kwenye jedwali la ziada la masahihisho *(Further Schedule of Amendments),* ambalo Waheshimiwa Wabunge, wamegawiwa leo asubuhi. Jedwali ni hili fupi ambalo tumelisambaza kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mapendekezo mengine ambayo hayahusiani moja kwa moja na Muswada huu, mbele yetu tumeyazingatia na tutayafanyia kazi kwa utaratibu wa kawaida wa shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningependa kupitia hoja mbali mbali ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia zaidi ya zile ambazo Mheshimiwa Naibu Waziri, amezielezea kwa ufasaha. Kwanza, ningependa kuzungumzia hoja ambazo zimetolewa na Kamati yetu ya Uwekezaji na Biashara halafu hoja ambazo zimetolewa kwa upande wa Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati alikuwa na hoja tatu. Kwanza, alikuwa na hoja kwamba, fedha zinazotolewa kwa wakulima chini ya mfumo wa *STABEX* na utaratibu wa matumizi yake kuwa wazi hivyo, Wizara ya Fedha iandike waraka wa maelezo ya matumizi ya fedha hizo na usambazwe kwa Wakuu wa Mikoa, Wilaya na Waheshimiwa Wabunge. Hoja hii imechangiwa na Mheshimiwa Talala Mbise na Mheshimiwa Thomas Ngawaiya. Nakubaliana na ushauri wa Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, pamoja na Waheshimiwa Wabunge waliochangia. Wizara yangu itawasiliana na Wizara ya Fedha na Wizara ya Kilimo na Chakula, ili waraka utoke mapema na usambazwe kwa wadau kusudi kila mmoja wetu aweze kuelewa ni sehemu gani ambazo fedha hizi zitatumika.

Hoja ya pili, ilikuwa kwamba, Serikali iwahamasishe wananchi na kuwapatia Elimu ya Ushirika ili waielewe sheria hii vizuri na kuitekeleza. Baada ya kupitishwa kwa sheria hii, pamoja na kukamilika kwa *Cooperative Reform Programme,* Wizara itaandaa semina ya kuhamasisha na kuelimisha viongozi na wananchi kuhusu sera, sheria na mikakati ya kutekeleza Programmu hiyo. *(Makofi)*

La tatu, ilikuwa kwamba, Maafisa Ushirika wapatiwe nyenzo za kufanyia kazi ili waweze kutekeleza majukumu ipasavyo. Serikali kwa kuanzia mwaka 2002/2003, imeanza kuwapatia Maafisa Ushirika nyenzo za kufanyia kazi ikiwa ni pamoja na pikipiki 18 na fedha shilingi 95,000,000 na jumla ya Maafisa 25 walipatiwa mafunzo ya Elimu ya Ushirika Shirikishi. Utaratibu huu utaendelea katika mwaka huo wa fedha.

Sasa ningependa kutoa maelezo machache kuhusu hoja zilizowasilishwa na Mheshimiwa Aisha Phillipo Magina, Mbunge wa Viti Maalum na vile vile Waziri Mwenza kwa upande wa Upinzani. Kwanza, napenda nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Mbunge, kwa kuunga mkono Muswada huo. Msimamo wake wa kuunga mkono Muswada huu umetia moyo sana. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Kivuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Magina, ametoa hoja muhimu tatu. Kwanza, alisema kwamba sheria haizungumzii hatma ya Watendaji Wakuu kama Meneja Mkuu, Mhasibu Mkuu wakati Bodi ya Menejimenti inaposimamishwa na Mrajis na kuwekwa Bodi ya Menejimenti ya Muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taratibu zinazotawala ajira ya Watendaji wa Vyama vya Ushirika zimewekwa kwenye Muundo wa Utumishi na Kanuni za Utumishi, pamoja na mikataba ya ajira ya vyama husika. Hatma ya Watendaji Wakuu huamuliwa na Bodi ya Menejimenti kabla ya Bodi hiyo haijawajibishwa. Kwa hiyo, Serikali haiingii katika jambo hili.

Hoja ya pili, ni kuwa sheria haitamki muda *(Time Frame)*, kwa kukaimu Watendaji wanaowekwa na Mrajis. Kwa kawaida Serikali haipeleki watumishi wake kwenda kukaimu kwenye Chama cha Ushirika, isipokuwa pale kinapoombwa na ikidhihirika kwamba, kuna umuhimu. Kwa mfano, Vyama vya *SHIRECU* na *Kagera Cooperative Union (KCU),* imewahi kuomba Watendaji wa Serikali, Serikali iliwakubalia kwa kipindi cha miezi sita. Hata hivyo, Vyama hivyo baadaye waliomba muda wa nyongeza kwa watendaji hao na Serikali iliwakubalia.

Wakati watendaji hao wameazimishwa chama husika, hutakiwa kutangaza nafasi za watendaji hao ili waweze kupata mafunzo kazini, kusudi wapatikane mapema halafu wawe kama ni *under study* kwa wale watumishi ambao wamepelekwa na Serikali.

Hoja ya tatu, ilikuwa kwamba, Elimu ya Ushirika itolewe katika ngazi zote za Ushirika na viongozi wa ngazi mbalimbali, wananchi na katika shule na vyuo. Hoja hii imeshachangiwa pia na Waheshimiwa Wabunge wafuatao: Mheshimiwa Leonard Shango, Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, Mheshimiwa Ismail Iwvatta, Mheshimiwa Prof. Daimon Mwaga, Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Edson Halinga, Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Paul Kimiti na Mheshimiwa Dr. James Msekela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Elimu ya Ushirika ni moja ya misingi muhimu katika Vyama vya Ushirika. Sheria imetambua hilo na Wizara imeandaa na imeanza kutekeleza Programmu ya Ushirika Shirikishi, yaani MEMCOOP kwa awamu.

Kuhusu uanzishaji wa somo la Elimu ya Ushirika shuleni, mawasiliano yamefanyika kati ya Wizara yangu, Chuo cha Ushirika Moshi, *VETA* na Wizara ya Elimu na Utamaduni, kwa lengo la kuandaa taratibu za kuingiza somo la Ushirika katika Mitaala ya Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo Vikuu. Tayari *VETA* wameridhia kuingiza somo la Ushirika katika mitaala yao. Mazungumzo na Wizara ya Elimu yanaendelea kutekeleza jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu unatambua kwamba, kuna umuhimu wa kuwa na ngazi mbili za ushirika, yaani Vyama vya Msingi na Shirikisho. Haulazimishi kuwepo kwa vyama vya kati na vyama vya kilele. Kama alivyoeleza Naibu Waziri, vyama hivyo vitakuwepo kutegemea na mahitaji ya wanachama na uwezo wa kiuchumi wa kuviendesha. Hapa ningetaka kuongeza kwamba, vitakuwepo kama kuna kazi ya lazima ya kufanya na kama kazi hiyo haiwezi kufanyika katika ngazi nyingine za Vyama vya Ushirika.

Hoja ya pili, ilikuwa kwamba, Halmashauri za Wilaya kuhusishwa katika kusimamia shughuli za Ushirika. Nadhani hii rai ilitolewa na Mheshimiwa Mbowe. Waheshimiwa Wabunge wengine waliochangia hoja hii ni Mheshimiwa Ismail Iwvatta, Mheshimiwa Leonard Shango na Mheshimiwa Dr. James Msekela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyama vya Ushirika, kama wote mnavyovifahamu, ni vyombo vya Kibiashara, vina Bodi za Menejimenti ambazo husimamia uendeshaji wa shughuli za vyama hivyo. Aidha, vyama vina wanachama ambao ndio wenye hisa *(shareholders)*. Hivyo, haitakuwa sahihi kuruhusu Halmashauri kuingilia usimamizi wa shughuli za Vyama vya Ushirika. Hata hivyo, Halmashauri zinaweza kushiriki katika uhamasishaji wa wananchi kuanzisha au kujiunga na Vyama vya Ushirika kwa pamoja na kuwapatia Elimu ya Ushirika. Kama kuna haja, unaweza kuandaliwa mkutano wa pamoja kati ya uongozi wa Halmashauri na uongozi wa chama kinachohusika, kutatua matatizo yanayoweza kujitokeza ambayo yanahusu sehemu zote mbili.

Hoja ya tatu, ilikuwa kwamba, Vyama vya Ushirika vya Msingi viruhusiwe kuuza mazao yao ndani na nje ya nchi bila kupitia vyama vikuu. Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja hii ni Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala na Mheshimiwa Isaac Cheyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari kuna baadhi ya Vyama vya Ushirika vya Msingi, vinavyouza mazao yao moja kwa moja bila kupitia vyama vikuu. Kwa mfano, Vyama vya Msingi katika Mikoa ya Arusha, Manyara, Ruvuma na Kilimanjaro, vinafanya hivyo. Kufuatia sheria mpya, majukumu ya vyama vikuu na vyama vya msingi, yataainishwa upya kwenye masharti yao *(bye-laws),* ili vyama vikuu vifanye shughuli zile tu ambazo vyama vya msingi haviwezi kuzifanya.

Kama Mheshimiwa Mutungirehi anavifahamu vyama katika Wilaya ya Karagwe, ambavyo viko tayari, vina uwezo wa kifedha na utaalamu, kuweza kuuza mazao moja kwa moja bila ya kupitia katika *union,* nitakuwa tayari kupokea mapendekezo yake na tutayatekeleza. *(Makofi)*

Hoja nyingine iliyotolewa ilihusu masoko ya mazao na kwamba, Serikali iandae sera na sheria ya masoko ili Serikali itoe upendeleo muhimu kwa Vyama vya Ushirika kuwa na ukiritimba katika ununuzi wa mazao. Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja hii ni Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Stanley Kolimba na Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera ya Masoko ya Mazao ya Kilimo ambayo inaandaliwa, itaainisha kanuni na taratibu za ununuzi na uuzaji wa mazao ili kuleta ushindani ulio sawa na wa haki kwa wahusika wote, yaani *level playing field*. Kwa sasa hivi hakuna *level playing field* ama katika kutafuta mikopo au katika uendeshaji wenyewe au katika uuzaji.

Aidha, mkakati wa kutekeleza *Cooperative Reform Programme,* unaoandaliwa utajielekeza katika kuviwezesha vyama kujenga uwezo unaohitajika katika Menejimenti na katika mitaji ili viweze kushindana.

Hoja ya tano, ilikuwa kwamba, wakulima waruhusiwe kuuza kahawa nje bila ya kupitia minadani. Waliochangia hoja hii ni Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi na Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala. Hivi sasa utaratibu wa kuuza kahawa ni kwa kupitia mnadani Moshi, kama wote mnavyojua. Lakini kuanzia miaka miwili iliyopita, watu ambao wana kahawa inayoitwa kwa lugha ya kitaalamu *speciality coffee* au *coffee* inayoweza ku-*qualify* kwa *standards* za kilimwengu, wamewekewa utaratibu maalum wa kuweza kuuza moja kwa moja bila ya kupitia kwenye mnada. Utaratibu huu unasaidia kulinda ubora wa kahawa na kurahisisha ukusanyaji wa kodi. Aidha, utaratibu wa kuuza kahawa mnadani Moshi unazingatia sheria ya zao la kahawa ambayo ilipitishwa hapa Bungeni.

Hata hivyo, suala hili litafanyiwa marudio katika Sera ya Masoko ya Mazao ya kilimo inayoandaliwa. Katika hii sera tunayoiandaa, tutaweka utaratibu ambao utaruhusu kutumia utaratibu wa kuuza kahawa nje ya *auction* ya Moshi, lakini kwa kuzingatia makubaliano kati ya Uganda na Kenya, ambao tunaungana katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Hoja ya sita, ilikuwa kwamba, Bodi za Mazao zina gharama kubwa na hazimnufaishi mkulima. Vikundi hulipa bei kubwa kuliko Vyama vya Ushirika, Kiwanda cha Kukoboa Kahawa cha Mbozi hakijatoa gawio. Hoja hizi zimetolewa na Mheshimiwa Edson Halinga. Sijui kama yupo, ningetaka asikilize majibu ninayotaka kutoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ni msimamizi wa maendeleo ya Kahawa katika usindikaji na uzalishaji. Usimamizi huu muhimu ni kama ulivyoanishwa katika sheria

zilizoanzisha Bodi hiyo. Aidha, Serikali inafanya pitio ili kuhusisha uendeshaji wa Bodi hizo kwa njia ya kumpunguzia mkulima gharama. Vikundi ambavyo amevizungumzia Mheshimiwa Halinga kwamba, hulipa bei kubwa kuliko Vyama vya Ushirika. Utafiti uliofanywa na mimi mwenyewe nimetembelea Wilaya ya Mbozi, umeonyesha kwamba, Vyama vya Ushirika vya Mbozi, vina rekodi nzuri ya kufanya kazi nzuri na mimi sijui kwa nini Mheshimiwa Halinga, hakujivunia suala hili. Vyama vya Wilaya ya Mbozi, yaani *MBOCU* na *ISAYURA,* ni miongoni mwa Vyama vya Ushirika katika Tanzania ambavyo vinafanya kazi nzuri sana. Hata kabla ya kuanzisha *Export Great Guarantee Scheme,* havijawahi hata siku moja kushindwa kulipa mikopo kutoka kwenye Benki. *(Makofi)*

Takwimu zilizopo zinaonyesha kuwa katika msimu uliopita wa 2002/2003, Vyama vya Msingi katika Wilaya ya Mbozi vimelipa kwanza shilingi 350/= kwa kilo kwa zao la kahawa kama malipo ya kwanza na shilingi 70/= kwa kilo kama malipo ya pili hivyo kufanya jumla ya fedha walizolipa kwa kilo kuwa shilingi 420/=, ikilinganishwa na wastani wa shilingi 400/= kwa kilo zilizolipwa na wanunuzi binafsi kupitia vikundi. Kwa hiyo, si kweli kwamba, vikundi vinalipa bei nzuri zaidi kuliko Vyama vya Ushirika. Vikundi hivyo kwa bahati mbaya havina mipango ya kulipa malipo ya pili. Ukisha wauzia basi umeachana na kahawa zako, chochote kitakachopatikana wewe huna lako katika hilo.

Aidha, vikundi hivyo kwa bahati mbaya havikuandikishwa kisheria, kwa hiyo, vikipotea na fedha zako, basi mkulima atakuwa amepoteza haviwezi kushtakiwa. Ametoa rai vile vile kwamba, Kiwanda cha Kukobolea Kahawa cha Mbozi hakijatoa gawio. Mimi ningedhani kwamba amefurahia jambo hili kwamba hatujatoa magawio. Kiwanda cha Mbozi cha Kukoboa Kahawa wanahisa wake ni pamoja na Serikali, *KNCU, Kagera Cooperative Union* na *Karagwe District Properties Union.* Wanahisa hawa wana moyo wa kizalendo, wameweka hisa lakini hawajadai hata siku moja kulipwa *interest* wala gawio.

Wamefanya hiyo kuwasaidia washirika wenzao. Ni matumaini yangu kwamba, Mheshimiwa Mutungirehi, baada ya kusikia hii taarifa, hatakwenda kuwachochea *KDCU* kuanza kudai gawio na riba. Uamuzi huu ulifikiwa na wanasiasa wenyewe na wanastahili kupongezwa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro na umiliki na matumizi ya mashamba ya Vyama vya Ushirika katika Mkoa wa Kilimanjaro. Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja hii ni Mheshimiwa Freeman Mbowe na Mheshimiwa Aggrey Mwanri. Serikali inalifahamu sana suala hili na mimi mwenyewe, nimewahi kushughulikia masuala haya katika Mkoa wa Kilimanjaro ilipolazimika kufanya hivyo. Lakini kwa kuzingatia kwamba migogoro hii inazihusu Wizara na wadau wengi zaidi ya Wizara yangu, tunataka kutumia utaratibu uliopo kwamba, nitawahusisha Wizara zinazohusika na naweza kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, muda si mrefu tunaweza kupata tatizo la suala hilo. *(Makofi)*

Suala si mashamba, suala ni namna wanavyotumia mapato yanayotokana na hayo mashamba. Hoja ya nane ilikuwa Waziri ataingilia vipi kuagiza Chuo cha Ushirika baada ya kuwa Chuo Kikuu na kwa nini chuo hiki kisiwe Chuo Kikuu kamili badala ya kuwa kuwa Chuo Kikuu Kishiriki? Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja hii ni Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Talala Mbise na Mheshimiwa Prof. Daimon Mwaga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengine wametoa hoja zifuatazo: Hoja ya kwanza ilikuwa kuwepo kwa ngazi nyingi katika muundo wa Ushirika. Waheshimiwa Wabunge, waliochangia hoja hii ni Mheshimiwa Edson Halinga, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa George Lubeleje na Mheshimiwa Isaac Cheyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele hiki kimekwisha rekebishwa katika Muswada na Waziri wa Ushirika anaweza kuagiza tu kutekeleza majukumu yanayohusiana na Ushirika kwa kuwasiliana na Waziri mwenye dhamana ya Chuo Kikuu. Kwa kuwa chuo kitaendelea kutoa mafunzo ya taaluma ya Ushirika na stadi za biashara, hivyo kitatekeleza sera ya maendeleo ya Ushirika ambayo inasimamiwa na Wizara yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Chuo cha Ushirika Moshi kuwa Chuo Kikuu kamili, kuna utaratibu wa Serikali ambao unatumika kuanzisha Vyuo Vikuu. Kwa utaratibu huo, sasa Chuo cha Ushirika kinapaswa kuwa Chuo Kishiriki kwanza kabla ya kuwa Chuo kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kuchangia hoja hii. Kupitishwa kwa Muswada huu kuwa Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2003, kutawezesha kuwepo kwa mazingira muafaka ya kufufua, kuimarisha na kuendeleza ushirika na hivyo kufanya ushirika ukidhi mahitaji ya wanachama, wadau wengine na umma wa Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Vyama vya Ushirika wa Mwaka 2003**
***(The Cooperative Societies Bill, 2003)***

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada huu una vifungu vingi kweli kama mlivyoona. Tukitaka kupitia kifungu kwa kifungu, tutachukua muda mrefu

kweli. Kwa hiyo, naomba tukubaliane tu kwamba, wasome kwa sehemu, lakini mtu anaweza aka-*note* eneo lile ili aweze kuhoji pale anapotaka kuhoji. Je, hilo limekubaliwa?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2
Kifungu cha 3
Kifungu cha 4

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 5

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika sehemu ya 4 kifungu cha 14: *"The structure of cooperatives shall be made up of Primary Societies, at the grass root level and the Federation at the top."*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mutungirehi, kile kifungu tulishapita, bahati mbaya kabisa hukusimama mapema. Kifungu hicho kimeshapitishwa, tuangalie kifungu kingine mbele ya safari.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 6

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 7
Kifungu cha 8

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 9

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo kifungu cha 74 anaposema: “Chama cha Shirikisho kitaanzisha Mfuko na kwamba Wanachama watachangia.” Niliuliza hapa jana na nilitaka kuuliza pale mwanzo, lakini muda ukawa umenipita. Kuna Chama cha Msingi, kuna Chama Kikuu na Chama cha Kilele na huko kote Serikali haitoi hata senti ya kuanzisha Vyama hivyo, inapokuja

kwenye hiki kifungu kwamba, hivi Vyama vichangie kwenye huo Mfuko; je, Waziri haoni kwamba, huko ni kuendelea kukata na kupunguza mapato ya kila kilo ya mkulima na ni kwa nini Mfuko huo usianzishwe na Serikali?

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Mheshimiwa Mbunge, atakuwa amepata *amendments* ambazo tumezisambaza kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba, kifungu hiki kimefanyiwa *amendment.* Hautakuwepo Mfuko wa *Central,* isipokuwa badala yake utakuwepo Mfuko wa Ukaguzi na Mfuko wa Ukaguzi kwa kawaida huwa unachangiwa sehemu zote mbili, Serikali inachangia na Wanachama wanachangia. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 10

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 11
Kifungu cha 12

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 13

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 14

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 102: *"A liquidator appointed under section 101 shall have the power, subject to the guidance and control of the registrar, and to any limitation imposed by the registrar."* Ningeshauri tubadilishe iwe ya kwamba: *"With consent of the Court."* Kwa sababu ukifanya Msajili ndiye awe ana-*control* hata Mahakama, itakuwa ni kinyume cha utaratibu tunaoufahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa kuwa kama nilivyosema kwenye hoja yangu ya msingi kwamba, ni lazima tujue mipaka ya Msajili na mipaka ya Mahakama. Kama kuna mambo ya Mahakama, *then* Mahakama ndiyo inaweza kufanya *control* hiyo. Kwa hiyo, ningeshauri kabisa Msajili awe ana madaraka hayo, lakini yawe *with consent of the Court,* ambavyo ndivyo tulivyoweka kwenye Sheria ya Kampuni tuliyoipitisha mwaka jana na mwaka huu kwa mambo ya *liquidator.*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kuna hii dhana nzima ya kutambua Vyombo hivi kwamba, ni vya Wanachama wenyewe na *scheme* inayopendekeza katika Muswada huu kwenye hii sehemu ya 14, maana vifungu tunavyovilenga kwenye 101 kabla ya kufika kwenye 102 ni hivi vya 97 na 98, pale ambapo palikuwa *'society'* inafutwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafikiria kwamba, ni vizuri utaratibu wa kufilisi ukasimamiwa na Msajili mwenyewe ili aweze kutoa maelekezo. Lakini katika kifungu hicho hicho, ambacho Mheshimiwa Mkono amesema, kifungu cha 102(2), ndiyo tunasema sasa kuanza katika *situation* fulani ambapo *scheme* hiyo aliyokuwa anaisemea inachukua sura hiyo na tunaiendeleza kwa kupambanua zile *rules* ambazo zinatengeneza hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema: *"The rules may provide for an appeal to a Court of a Resident Magistrate having jurisdiction over the area in which the headquarters of the society are situated from any decision made by a liquidator under this section and may provide for a further appeal to the High Court."*

Ndiyo *scheme* ambayo tunaiona *at least* kwamba, shughuli za kusimamia ufilisi ziwe chini ya Msajili, lakini kama yapo masuala mengine ambayo mfilisiwa au wenye *interest* na *asset* hizo hawaridhiki, *then* kanuni zinatengeneza ku-*provide* wapate haki katika mikondo hiyo ya sheria, lakini hatutaki Mahakama isimamie shughuli hizi katika ngazi hizi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 15

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naangalia hiki kifungu cha 124 ambapo kinasema: *"The Director of Public Prosecutions shall, by notice, published in the Gazette appoint Prosecutors who shall be responsible for prosecution of cases involving Cooperative Societies."* Kwa maoni yangu nadhani uzoefu umetuonyesha kwamba, Vyama vyote Vikuu vya Ushirika vimeliwa na waliovila wako nje wanacheka na wanafanya biashara zao kwa sababu ya kum-*involve* huyu *Director of Public Prosecution.*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, alikuwa anagombana na Mheshimiwa Chenge hapa kwamba, watu wote waliohujumu mbona hamuwakamati, badala yake tukaletewa lori la makaratasi hapa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama *bylaws* za Vyama vya Ushirika wanasema kwamba, hiki Chama cha Ushirika kinaweza kushtaki au kushtakiwa, ni kwa nini tusifike mahali tukasema ile Halmashauri ikam-*hire* Wakili wakaenda kushtaki ili kesi hizo ziishe? Vinginevyo, kuna *Public Prosecutor,* ambaye hana *public interest* za watu wa

Ushirika. Kwa hiyo, nilikuwa naomba hapa tubadilishe kwamba, wale wanaohusika wamshtaki kwa sababu ndiyo wenye mali, siyo mtu wanampelekea mtu wanaelezana naye halafu mambo yanaishia huko na ninadhani Mheshimiwa Waziri analijua hilo kwamba, kwa wale wote waliokula Vyama vya Ushirika, hakuna Mtanzania ambaye amekwishafungwa.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda niseme jambo moja la msingi kwamba, katika mfumo wa Mahakama zetu hao anaowataja Mheshimiwa Mutungirehi hata wangeenda wamefungasha mizigo wakijiita wao ni Waendesha Mashtaka, Mahakama hazitawatambua. Hata kama tungekuwa na u-*zealot* (ukereketwa), wa namna gani na masuala haya ya Ushirika ni vizuri tukaendelea kuheshimu taratibu tulizonazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kinasema hivi: "Mkurugenzi wa Mashtaka, ambaye ndiyo Sheria za Nchi zinaruhusu asimamie mashtaka yote, aanzishe kuyaondoa, kuyaendeleza au kuyafuta atateua hawa..."

Sasa, kwa maelezo ya Waziri, kama Mheshimiwa Mutungirehi amemsikiliza vizuri, tunasema sasa tunataka tujenge hii kada mpya ya hao Wasimamizi wa Mashtaka ambao watafundishwa kazi na watakuwa wanashughulikia masuala haya tu, kusimamia na kuendesha kesi zinazotokana na shughuli za ushirika. Tunadhani hii ni hatua nzuri sana kama tutaweza kusimamia vizuri kuondokana na malalamiko ambayo anasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kubwa zaidi ni kwamba, kesi yoyote inategemea jinsi uchunguzi ulivyofanyika na jinsi gani Wananchi/Wanachama wanaosikia kwamba mali zao zimeibwa watakavyoweza kushirikiana na huyu *Prosecutor* na hata Polisi watakaofanya uchunguzi ili kuweza kufanikisha hayo mashtaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Jedwali

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jedwali hili sehemu ya 3, *section 11(d)* kinasema: "Ili Mjumbe wa Kamati au Halmashauri aweze kuchaguliwa, atajaza fomu, lakini pale ataonyesha pamoja na mambo mengine kiwango chake cha elimu." Lakini huku hatukuweka ni elimu kiasi gani anapaswa kuwa nayo. Sijui kama hatuwezi kuweka kiwango cha elimu, maana yule wa msingi kwenye sheria ameambiwa awe anajua kusoma na kuandika Kiswahili na Kiingereza, lakini *level* haitajwi. Sasa hapa huyu anakwenda kwenye *union*, kwenye *Apex,* anataka kuzungumzia mabilioni ya pesa katika utandawazi, amekaa pale hajui. Je, huyu hatumuwekei awe na kiwango gani cha elimu?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Hoja aliyosema Mheshimiwa Mutungirehi ni nzuri, lakini kwa sababu tuna-*deal* na hii *schedule* inasimamiwa na maudhui ya Muswada wenyewe. Kwa hiyo, kule ambapo tumetaja kiwango cha elimu, inategemea sasa anapowasilisha maombi yake ajaze aseme wewe ni darasa la ngapi. Kama haikidhi matakwa ya sheria, *certainly* yuko nje ya utaratibu. Ndiyo tafsiri ninayoipata hii, badala ya kurudia kuisema huku kwenye kifungu husika ambapo kimeshatajwa. Kwa hiyo, hakuna tatizo *unless* nimeshindwa kumuelewa tatizo lake.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Siyo kwamba, Mwanasheria Mkuu wa Serikali hanielewi, isipokuwa anakataa kunielewa. Ninachosema ni kwamba, kule amesema ajue kusoma na kuandika Kiswahili na Kiingereza. Sasa, hiyo haisemi kiwango cha elimu na kwa kuwa hatapewa mtihani kwenye zile fomu kama sisi tunavyoona, huenda ikatumika mizengwe. Sijui tunachoogopa ni nini, tunaweka kwamba aanzie hapa kwenda huko na sijui kama hilo amelielewa au ...

**MBUNGE FULANI:** Atoe pendekezo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mutungirehi, pendekeza.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Awe kuanzia *form four* na kuendelea.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima Tanzania tuifahamu maana huko Vijijini kama kweli unataka uwapate watu waliomaliza darasa la 14 au 12, basi sheria hii itakuwa haina maana kabisa. Lakini tushughulike na hali halisi, hawa Wanachama wanafahamu wewe Chenge pamoja na kwamba umemaliza darasa la 4, uzoefu wako, uadilifu wako, *credibility* yako, yote haya yanakwenda pamoja. Kwa hiyo, wataona kwamba, wewe tunaweza tukukabidhi pesa yetu hapa. *(Makofi)*

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Vyama vya Ushirika wa Mwaka 2003**
***(The Cooperative Societies Bill, 2003)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada uitwao *The Cooperative Societies Bill, 2003,* pamoja na mabadiliko yake kifungu kwa kifungu na

kuukubali. Hivyo basi, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa *The Cooperative Societies Bill, 2003* sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijasitisha shughuli za Bunge, nina matangazo kwamba, tunasisitiza zile taarifa mbili zisije zikapotea, wakati wa kuja Bunge lijalo tuje nazo. Kwa hiyo, tusije tukazitupa kwani wametuomba sana wale watu. Nasisitiza kama hujapata zile taarifa mbili za sensa ni vema upate, kuna wengine wamepata na wengine bado, sijui kwa nini, lakini zitapatikana kila mmoja atapata.

Suala lingine ni kwamba, hatukuelewana wakati niliposema ni vema Wabunge wawemo humu ndani kwa sababu nilikuwa najua tutahitimisha Muswada huu adhuhuri hii na nilikuwa najua kwamba baadaye tutakuwa na muda. Kwa hiyo, tuliona tukae hivi. Ninawashukuru sana kwa kuheshimu kiti. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, shughuli ambazo zilipangwa kwa leo zimekwisha. Kwa hiyo, wale wenye vikao saa 10.00 waendelee na vikao vyao vya Vyama na kuanzia sasa ni huria mpaka mtakapomaliza ninyi wenyewe, huo ndiyo muda muafaka.

Baada ya hapo, sasa naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 6.55 mchana Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne Tarehe 11 Novemba, 2003 Saa Tatu Asubuhi)*